Uk.106 kuna problem

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI

SPIKA – MHE. PANDU AMEIR KIFICHO

1.Mhe. Kamal Basha Pandu	Naibu Spika/Jimbo la Rahaleo.
2.Mhe. Ali Mzee Ali	Mwenyekiti wa Baraza/Uteuzi wa Rais.
3. Thuwaibah Edington Kissasi	Mwenyekiti wa Baraza/Nafasi za Wanawake.
4.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	MBM/Waziri Kiongozi/ Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Jimbo la Mwanakwerekwe.
5.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Naibu Waziri Kiongozi/Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo/ Jimbo la Donge.
6.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	Kiongozi wa Upinzani/"Waziri Kivuli"–Afisi ya Waziri Kiongozi/Jimbo la Mgogoni.
7.Mhe. Haji Omar Kheri	Mnadhimu wa Upande wa Serikali/Jimbo la Tumbatu.
8.Mhe. Haji Faki Shaali	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Katiba na Utawala Bora/Mnadhimu wa Upande wa Upinzani/Jimbo la Mkanyageni.
9.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi/ Jimbo la Dimani.

10.Mhe. Ramadhan Abdulla Shaaban	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Katiba na Utawala Bora/Uteuzi wa Rais.
11.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi Vya S.M.Z./Jimbo la Jang'ombe.
12.Mhe. Hamza Hassan Juma	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/ Jimbo la Kwamtipura.
13. Mhe. Machano Othman Said	Waziri wa Nchi, (AR) Mawasiliano na Uchukuzi./Jimbo la Chumbuni.
14. Mhe. Br.Gen. Adam C. Mwakanjuki	MBM/Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Uteuzi wa Rais.
15.Mhe. Samia Suluhu Hassan	MBM/Waziri wa Utalii/Biashara na Uwekezaji/Nafasi za Wanawake.
16.Mhe. Burhan Saadat Haji	MBM/Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/ Jimbo la Kikwajuni.
17.Mhe. Asha Abdalla Juma	MBM/Waziri wa Kazi Maendeleo ya Vijana,Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais.
18.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Makunduchi.
19.Mhe. Sultan Moh'd Mugheiry	MBM/Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/ Uteuzi wa Rais.
20.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Kiembesamaki.
21.Mhe. Zainab Omar Moh'd	MBM/Waziri wa Nchi (AR) Kazi Maalum/ Nafasi za Wanawake.
22.Mhe. Idi Pandu Hassan	Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

23. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo/Jimbo la Mpendae.
24. Mhe. Mzee Ali Ussi	Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chaani.
25. Mhe. Khatib Suleiman Bakari	Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Bububu.
26.Mhe. Khamis Jabir Makame	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mtoni.
27.Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Dole.
28.Mhe. Tafana Kassim Mzee	Naibu Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Uzini.
29.Mhe. Zahra Ali Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi/Nafasi za Wanawake.
30.Mhe. Zakiya Omar Juma	"Waziri Kivuli"-Wizara ya Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Nafasi za Wanawake.
31.Mhe. Said Ali Mbarouk	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) na MBLM Fedha na Uchumi/Jimbo la Gando.
32.Mhe. Abdulla Juma Abdulla	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) – Tawala za Mikoa na Vikosi Vya SMZ/Jimbo la Chonga.
33.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Nchi (AR) Kazi Maalum/Nafasi za Wanawake.

34.Mhe. Hamad Masoud Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Maji,Ujenzi, Nishati na Ardhi/Jimbo la Ole.
35.Mhe. Omar Ali Shehe	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi/Jimbo la Chake-Chake.
36.Mhe. Rashid Seif Suleiman	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii/Jimbo la Ziwani.
37.Mhe. Mohamed Ali Salim	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Mkoani.
38.Mhe. Asaa Othman Hamad	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira/Jimbo la Wete.
39.Mhe. Aziza Nabahan Suleiman	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Nafasi za Wanawake.
40.Mhe. Najma Khalfan Juma	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo/Nafasi za Wanawake.
41.Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin	"Waziri Kivuli"–Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji/Jimbo la Mtambile.
42.Mhe. Abdulla Mwinyi Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.
43. Mhe. Abass Juma Muhunzi	Jimbo la Chambani.
44.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini.
45.Mhe. Ali Denge Makame	Jimbo la Amani.

46.Mhe. Ali Haji Ali	Jimbo la Mkwajuni.
47.Mhe. Ali Moh'd Bakari	Jimbo la Tumbe.
48.Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kwahani.
49.Mhe. Ame Mati Wadi	Jimbo la Matemwe.
50.Mhe. Ame Ussi Juma	Jimbo la Nungwi.
51.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake.
52.Mhe. Anaclet Thobias Makungila	Jimbo la Fuoni.
53. Mhe. Asha Moh'd Hilal	Jimbo la Magogoni.
54.Mhe. Ashura Abeid Faraji	Nafasi za Wanawake.
55.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Nafasi za Wanawake.
56.Mhe. Dadi Faki Dadi	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Pemba.
57.Mhe. Fatma Abdalla Tamim	Nafasi za Wanawake.
58.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	Jimbo la Mji Mkongwe.
59.Mhe. Haji Mkema Haji	Jimbo la Koani.
60.Mhe. Hasnuu Moh'd Haji	Uteuzi wa Rais.
61.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani.
62.Mhe. Major Juma Kassim Tindwa	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Pemba.
63. Mhe. Juma Duni Haji	Uteuzi wa Rais
64.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope.
65.Mhe. Mkongwe Nassor Juma	Nafasi za Wanawake.
66.Mhe. Moh'd Kombo Mkanga	Jimbo la Chwaka.

67.Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim	Mkuu wa Mkoa wa Kusini, Unguja.
68.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake.
69. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	Uteuzi wa Rais
70.Mhe. Omar Ali Jadi	Jimbo la Kojani.
71.Mhe. Pembe Juma Khamis	Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini, Unguja.
72.Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu	Jimbo la Muyuni.
73.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake.
74.Mhe. Said Khelef Ali	Jimbo la Bumbwini.
75.Mhe. Salim Abdulla Hamad	Jimbo la Mtambwe.
76.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni.
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni.
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde.

Ndg. Ibrahim Mzee Ibrahim	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi.**

Kikao cha Kumi na Saba – Tarehe 1 Julai, 2010

(Kika kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Thuwaybah Edington Kissasi) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 78

Utaratibu wa Kamati za Maendeleo Kupatiwa Fedha

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny. Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi) – Aliuliza:-

(a) Ni utaratibu gani unaotakiwa kutumika ili Kamati za Maendeleo za Jamii katika maeneo ziweze kupatiwa fedha hizo.

(b) Je, kuna kiwango maalum kilichowekwa kwa ajili ya maombi ya fedha za miradi ya aina hiyo.

(c) Ni aina gani ya miradi inayokubalika kwa utaratibu huo.

(d) Wizara ya Fedha na Uchumi inatumia utaratibu gani kuziwasilisha fedha hizo kwa wananchi.

Mhe. Waziri Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 78 lenye vifungu (a),(b),(c) na (d) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Fedha na Uchumi ikiwa ni msimamizi mkuu wa Miradi ya Maendeleo ya Wananchi, imefanya mapitio ya maombi ya fedha kwa miradi hiyo. Hivyo, imetoa muongozo na kuainisha vigezo vinavyotakiwa ili mradi uweze upatiwe fedha. Muongozo huo ni kama ifuatavyo:-

- Kwanza, serikali huwa inasaidia sehemu za fedha za mradi, hivyo mradi utakaoombewa fedha uwe

unatoa mwelekeo wa kukamilika na isiwe za kuanzia.

- Fedha zitatolewa kwa kuzingatia majimbo hivyo, mradi ni lazima uwe unatambulika Wilayani na katika Kamati za Maendeleo katika Jimbo husika.

- Barua ya maombi ya fedha iandikwe na Katibu wa Kamati ya Maendeleo kwenda kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Uchumi Zanzibar kupitia kwa Mkuu wa Wilaya husika, ikiwa imeambatanishwa na uchambuzi wa gharama za mradi.

- Kabla ya kupatiwa fedha, mradi utakaguliwa na maofisa wa wizara kuona kama una vigezo vya kuweza kupatiwa fedha hizo na ikithibitika vigezo vimefikiwa ndipo mradi utapatiwa fedha.

(b) Hadi sasa ukomo kwa mradi ni Shilingi Milioni Tano (TShs. 5,000,000/=). Wazo la kuanzishwa kwa Mfuko wa Jimbo (*CDF)* hatimae kutaondosha utaratibu wa serikali kusaidia wananchi katika miradi midogo midogo na *CDF* itatumika kugharamia shughuli hizo.

(c) Aina ya miradi inayokubalika ni ile miradi yenye kusaidia upunguzaji umaskini usiokuwa wa kipato, yaani miradi ya huduma za kijamii kama vile ujenzi wa Skuli, Vituo vya Afya, matengenezo ya barabara ndogo ndogo, Umeme, Maji safi na salama, Masoko na kadhalika.

(d) Utaratibu ambao Wizara ya Fedha na Uchumi wanatumia katika kuziwasilisha fedha hizo kwa Wananchi, ni kutoa cheki kwa Kamati au Jumuiya ya Maendeleo ya Jimbo au Shehia ambayo imefungua akaunti katika benki. Nakla za utoaji cheki hizo hupelekwa kwa:-

- Mhe. Mkuu wa Mkoa husika
- Mhe. Mkuu wa Wilaya husika
- Mhe. Mwakilishi wa Jimbo husika
- Mhe. Mbunge wa Jimbo husika.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, wenzetu Bungeni kipindi hiki tunachoendelea wameanzisha Mfumo wa Maendeleo ya Jimbo. Mfuko huo anayehusika moa kwa moja ni Mbunge, lakini kupitia kamati maalum iliyoteuliwa. Kwa bahati mbaya wawakilishi hawakushirikishwa. Ndio maana serikali ikaamua kwa upande wake wa

Zanzibar na wao kwa kipindi kijacho cha Baraza jipya la Wawakilishi kutakuta na Mfuko huo wa *CDF* kwa ajili ya maendeleo ya jimbo, lakini utashughulikiwa na Kamati ya Maendeleo ya Jimbo. Tukiangalia kiwango chetu kitakuwa kidogo kulinganisha na cha Wabunge.

Je, Mhe. Waziri pana wito gani wa pamoja kuhakikisha kwamba kinachopatikana cha Baraza la Wawakilishi na cha Bungeni kikaongezewa kikawa pamoja ili kuleta ufanisi katika kazi zetu hizo na kuondoa fitina kwa wananchi wetu.

Mhe. Waziri Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, naungana na kauli yake kwamba ni kweli kwamba serikali yetu imeshatia nia na tumeshazungumza kwenye Bajeti yetu ya Serikali kwamba mwaka ujao wa fedha na sisi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tutaanzisha Mfuko wetu wa Maendeleo wa Jimbo (*CDF*), ili kusaidia miradi ya wananchi.

Kwa kuanzia tumeseme hizi fedha ambazo zitatumika kwa miradi hii midogo midogo ya wananchi ambayo ilikuwa mtu aombe, sasa itakuwa kila jimbo linawajibika. Kwa sababu wakati ule ilikuwa kweli kila jimbo wanawajibika kupata, lakini kulikuwa na vigezo mbali mbali lazima uvifuate. Sasa tukaona kuna waheshimiwa wanalalamika kwamba hatupati, labda miradi ipo lakini hivi na hivi. Sasa tumeshasema huo *CDF* itakuwa kwa majimbo yote.

Sasa kuondosha fitina aliyozunguza, nizungumze tu kwamba hapo mwanzo lazima tukiri kwamba inapaswa tuelewane. Mwakilishi na Mbunge waelewane kwa maendeleo ya jimbo lao. Lakini kutokana na sababu mbali mbali ziliopo kuna baadhi ya majimbo kweli Mbunge pesa zile zinaingizwa au miradi ile Mwakilishi hata habari hana. Tunavyoambiwa sheria ile Mwakilishi hakutiwa. Ni kweli, wamezungumzwa madiwani wawili na mwenyewe Mbunge, labda na sheha mmoja kama hivyo. Sisi tunaunda sheria yetu na *Inshaallah* tutajitahidi katika robo ya mwanzo sheria ile tuipitishe ili pesa ziwepo kwa maendeleo ya jimbo letu.

Lakini ninachoomba sana kwa sababu ya maendeleo ya majimbo yetu, tujitahidi kuna Kamati zetu za Maendeleo basi haya matatizo madogo madogo tukae na Mbunge na Mwakilishi na diwani tuyasuluhishe. Lakini kama kuna matatizo basi tupigane haya mambo yaondoke, fitina hizo alizosema Mheshimiwa kweli yana fitina kidogo haya mambo.

Mhe. Salum Abdalla Hamad: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi hii. Kwanza nashukuru kwa utaratibu mzuri Mhe. Waziri aliioueleza kuhusu wizara inavyoshughulikia kusaidia kifedha kuondoa shughuli za kijamii. Kwa

bahati nzuri kwa sababu naamini kusaidia huondoa matatizo haya kwa makusudi kwa kushirikiana kikakmilifu na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, niliamua kwa kushirikiana na wananchi katika Jimbo langu kujenga Kituo cha Afya.

Kituo kile sikukijenga tu kwa maana ya kukijenga, lakini niliwasiliana na Wizara ya Afya wakaniletea mafundi, wakaweka michoro na kadhalika. Tukakijenga kwa kushirikiana na tangu wakati huo tukapeleka maombi yetu Wizara ya Fedha na pamoja na mpango mzima wa mahitaji yanayohitajiwa. Na nilikuwa nikiomba nikipitia kwako na wengine na kila siku nikiambiwa njoo kesho, njoo kesho mpaka hivi sasa jengo lile limeshaezekwa lakini tuko taabani.

Je, Mhe. Waziri mimi nilikosa nini wakati kitu kiko *live* mpaka leo nikawa sijapata chochote.

Mhe. Waziri Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Salum Abdalla Hamadi hakukosa kitu yeye ni Mhe. Mwakilishi ana haki na taratibu zake. Tatizo labda ni ule mradi wake kuwa ulionekana mkubwa kwa mapesa aliyoyataka, alitaka pesa nyingi hauku-*qualify*.

Sasa nikwambie tu kwamba, bado nafasi ipo mwaka huu wa fedha ndio kwanza unaanza, kituo kile wataalamu wangu wapo pale wananisikia, tutakwenda kukitembelea basi tutajaribu kusaidia maandiko. Unajua yale maandiko yana ufundi kabisa, sisemi wewe kwamba hujui kuandika aa, kuna kitaalamu kidogo. Sasa nafikiri uli-*over value* huu mradi na sisi *ceiling* yetu ni shilingi milioni tano. Kwa hivyo, nakuahidi Mhe. Salum kwamba tutashirikiana na wataalamu wetu, tutaandika vizuri na tutakusaidia Kituo chako cha Afya kimalizike.

Mhe. Ame Mati Wadi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ama kweli aliyejuu hamjui aliyechini. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri mwaka uliopita tuliongeza fungu yaani kutoka shilingi milioni mia mbili kwenda milioni mia tatu ili kila mjumbe kwa jimbo lake afaidike. Lakini cha kusikitisha inaonekana majimbo mengi hayakufaidika wakati tumepitisha kile kifungu ili miradi midogo midogo iende.

Basi niombe nikuulize Mhe. Waziri, hivi miradi mingapi ilibahatika kupata hizo fedha na kiasi gani fedha zenyewe walizopata. Kama inawezekana wangeniainishia wapi na wapi wamebahatika kupata fedha za miradi ya wananchi.

Mhe. Waziri Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ame Mati Wadi ni kweli kwamba tumeamua kuwa majimbo yote yana nafasi ya kupata pesa hizi. Lakini kama nilivyosema na nimevitaja vigezo vile, kwamba kila mradi maombi ni mengi, lakini kila mradi u-*qualify* kwa zile sifa nilizozitaja. Sasa maombi mengine huwa hayatimizi sifa hizi, hizo ndizo sababu kubwa kabisa.

Wataalamu wetu wapo wanatembea, wanakwenda, maombi wanayapokea. Hiyo niseme kwa sababu siendi mimi wala wewe Mheshimiwa, wewe unatuongoza hukui ndiko kwenye mradi, lakini sifa hizi hazitimizwi. Sasa ninachosema bado hatukatai nafasi ipo Mheshimiwa, tunakuombea Mungu na *Inshaallah* utarudi, mambo yapo kule tutayaweka sawa.

Pia uliuliza kwa mwaka uliopita wa 2009/2010. Wizara imetumia jumla ya shilingi zipatazo 444.84 milioni. Kwa Unguja shilingi 256.54 milioni na Pemba shilingi 192.3 milioni sawa na asilimia 89.8 ya bajeti hiyo uliyoisema ya shilingi milioni mia tano. Fedha hizo zimetumika kwa kugharamia miradi 112, 59 Unguja na 53 Pemba ikijumuisha maeneo ya usambazaji maji safi na salama, elimu, afya, kilimo, umeme na ukarabati wa barabara. Utaona *figure* hii ni kubwa kuliko ile tuliyoripoti kwenye Bajeti yetu ya Serikali.

Juzi hapa tulitoa *further* nyengine ndio maana hii *figure* imenyanyuka juu. Nakumbuka siku ile tulisema kama asilimia 53, sasa zimeongezeka zimefikia asilimia 89.8. Ahsante Mwenyekiti.

Nam. 69

Huduma za Benki ya Kiislamu *PBZ*

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*) imeamua kuanzisha huduma za kibenki zenye utaratibu wa Kiislamu (*Islamic Banking Division*) katika Tawi la Benki la Mwanakwerekwe katika jumba la *ZSSF*.

(a) Je, serikali inaweza kutueleza mtaji wa benki hiyo unatokana na fedha gani.

(b) Kwa kuwa faida ya benki ni riba. Je, mteja wa huduma hiyo atapata faida ipi kwa kuwa huduma hiyo haina riba.

(c) Nchi kama Malaysia zimewashajiisha wananchi wake kuwekeza katika benki kama hizo fedha maalum kwa ajili ya mfuko wa Hijja na Serikali Kuu huwaongezea kima fulani kwa lengo la kutimiza viwango vya kwenda kufanya Ibada ya Hijja. Je, Zanzibar itatumia utaratibu huo.

Mhe. Waziri Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 78 lenye vifungu (a),(b),(c) na (d) kama ifuatavyo:-

Nakumbuka jana nilimuahidi dada yangu Mhe. Najma Khalfani kwamba nitalijibu swali hili la Benki ya Kiislamu. Kwa hivyo, naomba na yeye kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, tumjumuishe majibu haya.

(a) Mhe. Mwenyekiti, Benki imeshatenga fedha kwa ajili ya mtaji wa kuanzisha kitengo cha huduma za Benki ya Kiislamu. Fedha hizo zimetumika kwa shughuli mbali mbali za matayarisho ya kitengo kama vile kutayarisha jengo, kununua fanicha za jengo, kutayarisha mtandao wa kumputa ambao utatumika katika shughuli hizo. Aidha, kuajiri na kuwafunza wafanyakazi watakaofanya kazi katika kitengo hicho na shughuli nyengine za matayarisho.
Kwa fedha za uendeshaji wa kitengo, benki inatarajia zitokane na amana za wateja wenyewe (*Mudarabah, Qard, Al Wadiah*), malipo ya gharama mbali mbali zitokanazo na huduma hizo kwa wateja pamoja na faida. Faida yenyewe ni ile *service charge* sio *interest*, itakayotokana na biashara ya kitengo chenyewe.

(b) Ni kweli kabisa kwamba kitengo hakitolipa wala kupokea riba katika uendeshaji wake kuendana na misingi ya Uislamu. Chanzo cha mapato kitatokana na shughuli zilizokubalika Kiislamu. Kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa hilo linatendeka, kitengo kitasimamiwa na Kamati Maalum ya Bodi itayokuwa na Wajumbe ambao ni wataalamu wa masuala ya dini na hasa Fiqhi, ambayo ndio msingi katika uendeshaji wa biashara katika Uislamu.

(c) Kwa Benki ya Kiislamu Mhe. Mwenyekiti, mapato yake yatatokana na malipo ya huduma kama nilivyosema hapo awali (*fees and Commissions*) pamoja na faida katika mauzo,

mikataba na Murabah. Kwa mfano, mteja anapokuja benki na kutaka anunue gari, baada ya kuthibitisha ustahiki wake benki haitomkopesha mteja huyo pesa za kununua gari, na badala yake itanunua gari hilo na kumuuzia mteja huyo kwa malipo ambayo yatafanyika baadae na kidogo kidogo.

Kama benki ilinunua gari kwa shilingi Milioni Tano na kumuuzia mteja kwa shilingi Milioni Sita, ile tofauti ya bei ndio faida ya benki. Huduma hii haiingii katika mkopo bali ni mkataba wa mauziano ambapo benki inamuuzia mteja hiyo gari.

(d) Kuhusu Benki kuwa na Mfuko wa Hijja kama zilivyo nchi nyengine kama Malaysia. Nchi nyingi Mhe. Mwenyekiti, zenye Mfumo wa Benki za Kiislamu wana utaratibu wa Mifuko ya Hijja (*Hajj Fund*). Mifuko hiyo hufanya kazi kama vile *Unit Trust* au Mifuko ya Hifadhi – *Pension Funds* (*Hajj Fund*). Mfuko hukusanya amana au michango hio na kuiwezesha katika vitegauchumi tofauti.

Wakati Benki inaangalia uwezekano wa kuanzisha Mifuko kama ya *Hajj Fund*, pia inakusudia kuanzisha akaunti maalum ya akiba kwa ajili ya Hija. Benki inaamini kwamba kuanzishwa kwa huduma za Benki ya Kiislam itakuwa ni chachu ya kuanzishwa huduma nyengine za Kiislamu kama vile huduma za Bima (*Takaful*) na nyenginezo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya kishekhe ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. amesema benki hii itasimamiwa na kamati maalum ambayo itakuwa ina wataalamu wa dini. Ningetaka kujua wataalamu hao ni wangapi na je, tayari wameshachaguliwa.

Pili kwa kuwa benki ina mpango wa kuanzisha Mfuko wa Hijja. Mfuko huu utaanzia lini na je, utaanzia kwa kiwango gani kwa Wazanzibari wote.

Mhe. Waziri Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, hatukutaka kuunda chombo chengine mbali ya Bodi yetu ya Wakurugenzi ya *PBZ.* Sasa Bodi ya Wakurugenzi wa *BPZ* ina wajumbe saba, tukaona wajumbe watatu wawe wako na taaluma hii ya Dini ya Kiislamu kusimamia maalum masuala haya. Wajumbe watatu hao tuko kwenye mchakato wa mwisho kuwamalizia ili tuweze kuwatangaza waingie kwenye bodi na zoezi zima lianze.

Mhe. Mwenyekiti, Mfuko wa Hijja ile nilisema kwamba hiyo ni mipango ya baadae sio sasa hivi kutuuliza kiasi gani, hiyo ni mipango ya baadae. Itapokuwa huko na tumetoa *experience* kwamba nchi nyengine wameanzia hivyo hivyo na baadae ndio wakafikia Mfuko huo. Kwa hivyo, ni mipango yetu ya baadae.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. tulisikia kwamba hii Benki ya Kiislamu mote humo duniani huwa haitozi riba. Lakini Mhe. Waziri kwa mfano aliotupa kwamba mimi nakopeshwa gari ya shilingi milioni tano lakini nilipe shilingi milioni sita. Hii moja si ndio riba yenyewe.

Mhe. Waziri Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ali Abdalla naomba kumhakikishia kwamba benki hii kama zilivyo benki nyengine za Kiislamu haitotoza riba. Riba wenyewe kitaalamu wanazungumza *interest*, hiyo haitotoza kabisa. Lakini huu mfano nilioutoa nimesema kuna *commission* na kuna *service charge*, sasa lile gari kufika hapa kuna gharama nyingi zimetumika mpaka likafika, sasa hizo zitajumlisha gharama hizo nilizozitaja, lakini hatutoongeza riba yetu ambayo kama ni mteja wa kawaida tungeongeza utulipe hiki kama sasa hivi unavyokwenda kukopa. Ukienda kukopa sasa hivi kuna riba maalum umeshawekewa unaijua hasa, asilimia hii inaongezeka unachajiwa. Sasa haitokuwa hivyo, suala la riba kabisa halipo.

Mhe. Zakiya Omar Juma: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti kwa sababu ya uelewa mdogo wa wananchi kuhusiana na namna ya kuzitumia benki hizi. Je, Mhe. Waziri ana mpango gani wa kutuelimisha. Kwa sababu kwa jibu ambalo alikuwa anajibu na swali aliloulizwa inaonekana uelewa wetu bado ni mdogo kuhusu suala hili. Kwa hivyo, ana mpango gani wa makusudi kuielimisha jamii ya Wazanzibari ili waweze kuitumia ipasavyo benki hii.

Mhe. Waziri Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anaeshughulikia Masuala ya Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba haya masuala kidogo yana *element* kubwa ya dini na yanahitaji tupate taaluma. Sasa tutajitahidi benki yetu wana kitengo chao wenyewe kile cha uenezi na taaluma, hivyo tutajitahidi wenyewe kutumia vyombo vyetu vya redio, televisheni hata semina.

Mhe. Mwenyekiti, labda kwa sababu sisi ni wawakilishi wa wananchi inabidi tuzipeleke hizi salamu kwa wananchi wetu. Kwa hivyo, nitoe ahadi kwamba tutalibeba hilo na kuandaa semina maalum *Inshaallah* mapema iwezekanavyo, lakini tumalize kwanza mambo yetu haya.

Nam. 86

Ulipaji wa Fidia Kutokana na Ujenzi wa Barabara

Mhe. Ramadhan Nyonje Pandu – Aliuliza:-

Hadi kufikia mwezi wa Machi, 2010 jumla ya shilingi 300 milioni zimetolewa kugharamia ujenzi wa uzio na ulipaji wa fidia ya mali na mazao ya wananchi kwa ajili ya ujenzi wa barabara sehemu mbali mbali.

(a) Kati ya fedha hizo ni kiasi gani kimelipwa na serikali kuwa ni fidia ya mazao ya wananchi.

(b) Ni jumla ya wananchi wangapi wamelipwa fidia hiyo.

(c) wananchi wote wanaodai fidia ni wangapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na kuhudhuria Kikao cha Baraza ili kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 86 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Kabla ya kumjibu Mheshimiwa swali lake, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Katika kipindi cha mwaka 2009/2010 serikali imepanga kujenga uzio mpya wenye urefu wa kilomita 12 katika Kiwanja cha Kimataifa cha Zanzibar. Ambapo jumla ya shilingi 1.1 bilioni zimetengwa kwa serikali kugharamia ujenzi huo ikiwa ni sehemu ya malipo ya mkandarasi wa ujenzi huo na malipo ya fidia ya mali za wananchi kama vile mazao ya nyumba. Hadi kufikia mwezi Machi, 2010 jumla ya shilingi 327 milioni zimetolewa na serikali kwa malipo ya mkandarasi wa ujenzi huo kati ya shilingi 1.1 bilioni zilizotengwa kwa ajili ya kipindi hicho.

Baada ya maelezo hayo anaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

Kutokana na maelezo niliyoeleza hapo juu, hakuna fedha zilizolipwa kwa ajili ya fidia ya mazao ya wananchi katika eneo linalojengwa uzio huo. Jumla ya wananchi wapatao 141 wamefanyiwa tathmini ya mazao mbali mbali katika awamu ya kwanza ili waweze kulipwa fidia za mazao. Ambapo wastani wa

shilingi 160 milioni zinahitajika. Aidha, zoezi la kufanyiwa tathmini wananchi wengine kwa awamu ya pili ili kujua idadi kamili ya wananchi wote wanastahiki kulipwa fidia zao kiasi cha fedha kinachohitajika kulipwa fidia hizo inaendelea.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, pamekuwa na malalamiko mengi kwa wananchi wetu wa sehemu ambazo zimepita barabara, lakini malalamiko hayo wanasherehekea kuwa barabara nzuri lakini bahati mbaya vipando vyao hadi leo havijalipwa. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katika jibu lake amesema kwamba bado wananchi hao hawajalipwa vipando vyao na mambo mengineyo, lakini katika jibu lake amesema kwamba kuna baadhi ya nyumba zimelipwa.

(a) Je, Mhe. Waziri kwa kuwa barabara hizi zimejengwa vizuri na wananchi wametoa fursa ya kukatwa mimea yao na mashamba yao kwa ajili ya kupita barabara. Haoni ni usumbufu mkubwa kuwacheleweshea pesa zao.

(b) Kwa kuwa baadhi ya nyumba watu wamelipwa fidia, lakini fidia nyingi zinalalamikiwa kuwa ni kidogo sana. Kwa mfano, nyumba imevunjika kiambaza kapewa mtu shilingi laki mbili. Haoni hiyo ni kasoro ambayo watafiti wao hawakufanya ukweli.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka kumjulisha Mhe. Mwakilishi kwamba hapa hili suala ameliingiza si pahala pake kwa sababu anazungumzia suala la malipo ya barabara. Hapa tunachozungumzia ni ujenzi wa uzio wa Uwanja wa Ndege wa Zanzibar. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nafikiri Mhe. Mwakilishi ilikuwa kuna haja nimpe maelezo rasmi katika maeneo mengine lakini hili si pahala pake.

Mhe. Haji Faki Shaali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, mimi namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake yaliyokuwa sio mabaya katika swali hili. Lakini swali langu kwamba wananchi wanakuwa mara nyingi wanalia kwamba fidia za mazao inakuwa ndogo. Je, kilio hichi tayari wamekisikia na watakapolipa mara hii wataboresha hizi fidia ziwe kubwa kidogo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba tunapokea malalamiko hayo, lakini wizara yangu inalipa haya mafao na wanaofanya tathmini ni Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira, kama ni nyumba wanaofanya tathmini ni Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Kwa hiyo, tutashirikiana na wizara mbili hizi ili

kuona kwamba tathmini zinazofanywa basi ziwe zinalingana na yale mazao pamoja na nyumba zinazolipwa.

Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa katika ujenzi wa barabara kuna nyumba hazikuvunjwa lakini zimeathirika kwa kupasuka pasuka ikiwemo Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja. Je, wanafikiria nini wizara katika nyumba zilizopata athari kama hizo.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (AR) Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hili swali limerejewa mara mbili na Waheshimiwa Wawakilishi kama lilivyo hapa, pamoja na kwamba tulikuwa tunajibu maswali yale ya Uwanja wa Ndege. Mhe. Mwenyekiti, nataka niwaambie tu kwamba kama nilivyosema mapema tathmini zinazofanywa zinafanywa na wenzetu hao, kama ni miti basi ni Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira na kama ni nyumba ni Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi ndio inafanya tathmini sisi kazi yetu ni kulipa.

Kwa hivyo, naendelea tena kusema kwamba tutashirikiana na wizara mbili hizi ili kuona kwamba tunakaa pamoja kuona tunapunguza malalamiko ya wananchi ambao wanahitaji kusaidiwa na serikali yao.

Hoja za Serikali

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 – Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe tunatakiwa leo mchana wote huu tuchangie mpaka jioni tunategemea kusikiliza majumuisho kutoka kwa Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo. Sasa tunaanza na Mhe. Abubakar Khamis Bakary halafu baadae tutamsikiliza Mhe. Haji Mkema Haji.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya mwanzo asubuhi hii na mimi nichangie kidogo tu kuhusu wizara hii. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mimi nilikuwa sina la kuchangia isipokuwa baada ya hotuba ya Mhe. Waziri kuna mambo mawili ambayo nilihisi bora nimtanabahishe na baadae anipe majibu.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 20 kifungu cha 14 (xxxv) kinasema kwamba "Imekamilisha taratibu zote za uwekaji wa majani bandia katika Uwanja wa Gombani Pemba".

Mhe. Mwenyekiti, hapa nina wasi wasi sana na habari nilizonazo pengine si sahihi na nitamuomba Mhe. Waziri aje anithibitishie kwamba fedha hizi ambazo zilikuwa zinatolewa na *FIFA* nafikiri kwa kupitia Tanzania Bara kiasi dola 250,000 hivi, fedha hizi zilikuja zikafikia kwa Mwakalebela sijui ndio Katibu Mkuu. Bahati mbaya huyu ndio aliyefanya ubadhirifu na hizi fedha sina uhakika lakini tunaamini kwamba zimeliwa. Kwa maana hiyo, suala hili la kupata majani bandia Uwanja wa Gombani itakuwa ni ndoto.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, hebu Mhe. Waziri atwambie kweli kuna ubadhirifu wa fedha hizi ambazo zilikuwa zinakusudiwa zinunuliwe majani haya bandia kwa Uwanja wa Gombani au ni maneno tu ambayo tunayasikia. Lakini ni hadithi tulizonazo ambazo ni asilimia 80 huko zinasema kwamba pana mbuzi hapa Tanzania Bara ambaye aliyala haya majani bandia. Tunaomba tuhakikishiwe vyenginevyo itabidi tuwe wakali sana katika suala hili. Kwa sababu majani hayatokuja wala hakuna njia nyengine ya kupata majani bandia itakuwa ni hadithi ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, la pili ukurasa huo huo wa 20 kifungu cha 14 (xxxvi) katika suala la Uwanja wa Gombani. Wanasema kwamba naomba kunukuu "Imeshakamilisha kazi ya upelekaji umeme wa fezi kubwa kwenye Uwanja wa Gombani na hivi sasa wanasubiriwa wataalam kutoka nje kuna kuzifungu taa kwenye minara".

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri atwambie wataalam hawa bado wako chuo kikuu mpaka wamalize miaka mitano *engineering*. Kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii ambapo wizara hii imo katika *portfolio* yetu na suala hili tulikuwa tukiliuliza karibu miaka miwili hivi sasa kwamba kazi ya kupeleka umeme wa fezi kubwa tayari umeshapelekwa tunasubiri *engineer*.

Mhe. Mwenyekit, *engineer* huyu yuko wapi, au bado yuko chuo kikuu. Sasa tusubiri miaka mitano au kuna matatizo gani. Kama kuna tatizo la usafiri tuchangie sisi tutawapa nauli ya kumleta huyu mtaalam au vipi. Maana yake kila siku hadithi ni hii hii mtaalam anakuja, mtaalam anakuja huu ni mwaka wa pili. Mhe. Mwenyekiti, naomba masuala haya mawili nipewe maelezo ya uhakika ili na mimi nikubali bajeti hii ya Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine katika hayo matatu niliyosema ambalo limenisikitisha ni hili linalofuata. Mhe. Mwenyekiti, jana kwa bahati nzuri

mimi niliondoka mapema na niliondoka sikutoroka, lakini kulikuwa na mgeni wa Baraza na mimi ni mmoja ambaye nilitakiwa nizungumze nae.

Sasa wakati tunamsubiri huyu mgeni nilikuwa ofisini kwangu nikakaa kidogo nikasikia kutoka kwenye kiredio changu mpaka humu ndani ya mkoba ninacho hufungua kule, nikasikia Sauti ya Tanzania Zanzibar inayorekodi maswali na majibu yamekatwa. Mimi nikasema hao tena sauti ya Unguja wameshaanza matatizo yao ya mitambo kumbe si kweli. Baada ya dakika tano kukatwa nikasikia Moh'd Raza anarejesha fomu kwenye hiyo hiyo sauti ya Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, wamethubutu kukata mazungumzo katika Baraza la Wawakilishi kwa Moh'd Raza anayerejesha fomu. Jamani *are we serious?* Maana yake hapa tuko katika serikali tunaikata kabisa kabisa na kwenda kwa mtu binafsi. Ingelikuwa angalau ni Waziri Kiongozi na Naibu Waziri Kiongozi kwa sababu wao tu ni Wajumbe katika Baraza hili na wao ni wakubwa katika nchi pale kidogo ningelikubali lakini Raza inahusu na nini kukata matangazo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba akija Mhe. Waziri anambie ni sababu gani zilizoifanya idara yake ikakata matangazo haya wakathubutu kudharau Baraza la Wawakilishi kwa mtu mmoja Moh'd Raza ambaye mimi nasema hana maana kwa wakati huu kwa sababu hahusiki.

Mhe. Mwenyekiti, la pili nataka nijue ni kiasi gani alizolipa Moh'd Raza mpaka wakathubutu redio hiyo ikakata kwa sababu ya kutangazwa kwamba anarejesha fomu. Huyu hajawa katika mchakato wa huo ukubwa anaogombea, ndio kwanza yuko katika mchakato huu wa kawaida, ni sawa sawa na mtu wa kawaida. Sasa naomba nijue ni fedha ngapi zilizolipwa na ninapojibiwa nioneshwe risiti sio maneno tu. Vyenginevyo namheshimu sana rafiki yangu Mhe. Ali Juma Shamuhuna lakini haya mambo matatu kidogo nitakuwa mgumu. Labda amwendee Mhe. Burhan Saadat Haji amuombe ile dua aliyonisomea mimi jana.

Maana yake jana Mhe. Mwenyekiti, nilimwambia Mhe. Burhan Saadat Haji kwamba sitokubaliana nae lakini akanipiga dua nikapewa kikaratasi hapa kwamba naitwa. Kwa hivyo, labda afanye utaratibu huo lakini sitokubali kabisa kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, haya ndio mambo matatu ambayo nilisema nataka kuyachangia. Sasa jambo la nne ambalo hili ni la kawaida naomba nichangie ni kwamba Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali wakati alipokuwa akichangia alisema na mimi nakubali kwamba tumeshajiandaa ili kuwa na mitihani yetu wenyewe, ni jambo zuri sana. Lakini sasa hapa namuomba Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo katika mitihani hii

washirikiane sana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali hasa katika suala la Kiswahili.

Mhe. Mwenyekiti, unajua tuna waandishi wengi sana wa Kiswahili Wazanzibari lakini mitihani iliyopo ya siku hizi ya Bara hakuna hata kitabu kimoja cha mwandishi wa Zanzibar ambacho kinathaminiwa. Sasa na mimi ningelipendekeza kwamba vitabu vyao vyote tuvifanye havina Kiswahili, waandishi wetu wawe ni waandishi ambao wamo katika *syllabus* za mitihani ili tuwasaidie. Kwa hivyo, hilo ni ombi langu ambalo nahisi linaweza likawasaidia waandishi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni suala la utamaduni. Hili kama nilivyosema mwaka jana naomba niseme tena kwamba utamaduni wetu kwa kweli tumeutupa. Kwa sababu ukenda katika maeneo chungu nzima kuna zile ngoma za zamani ambazo zote hazipo na huu ndio utamaduni wa Mzanzibari. Mhe. Mwenyekiti, Makunduchi wana ngoma yao ya asili, Mkoani wana ngoma yao ya asili, Mchangamdogo wana ngoma zao za asili na mifano mingine.

Mhe. Mwenyekiti, ngoma hizi zote hazipo kwa nini tunazipoteza. Kwa nini hatuwaweki wenzetu kwa mfano kama Kenya ambapo wana kitu wanaita *Bomas of Kenya* wanakusanya utamaduni wote, ngoma zote za Kenya nzima. Sasa tujaribuni kufanya hivi angalau tuzihuishe zile ngoma za asili na hizo ndio zitatupa hasa ile asili ya Uzanzibari na ngoma zao.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyokwambia sina mengi isipokuwa la mwisho ninalotaka kusema ni kwamba Profesa Ali Denge Makame wakati mwengine ana kitu kimoja ambacho ni kizuri sana, ana muono mkubwa. Wakati mwengine anapozungumza hapa sisi tunafikiria anafanya masihara lakini ni kweli. Nakumbuka juzi alisema kwamba kompyuta nyengine zina matatizo ya kuruka ruka.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubali kwa sababu hata leo hapa kuna eneo ambalo kompyuta imeruka. Kwa sababu nilikuwa nafikiria kwamba katika kitabu hichi na hasa kwa kuwa Mhe. Ali Juma Shamuhuna nae yumo katika mchakato, basi kingelisema kuhusu utaratibu mzima wa maelewano kati ya Mhe. Amani Abeid Karume na Maalim Seif Shariff Hamad pamoja na jitihada zao za kuweka nchi hii katika hali ya usalama.

Mhe. Mwenyekiti, pia kiongozi kama yeye nilikuwa nafikiria na naamini ndivyo msimamo wake ulivyo kwamba angeliwashawishi watu wakubaliane na hali hii ambayo tunakwendanayo ya usalama na kwamba inapofika tarehe 31 Julai, 2010 basi wakubali kwamba sote tukubaliane hii Zanzibar ni yetu na

tuwe wamoja. Sasa kwa maana hiyo, sote tukubaliane kupiga kura ya ndio ili tulete umoja katika nchi hii.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, simlaumu sana kwa sababu kompyuta zina matatizo siku hizi. Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache nakushukuru sana na nitaunga mkono hoja baada ya kupata yale mambo yangu matatu ya Uwanja wa Gombani *engineer*, majani yaliyoliwa na mbuzi na suala la Moh'd Raza. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kunipa nafasi asubuhi hii nichangie bajeti ya Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kwa mwaka 2010/2011.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na viongozi wote wa wizara kwa jitihada kubwa wanayofanya katika kuendeleza wizara yao. Mhe. Mwenyekiti, maendeleo waliyofanya hayahitaji tochi, bali yanaonekana dhahiri tangu majengo ya ofisi yao mpya waliyohamia, matengenezo ya viwanja mbali mbali na maendeleo mengine katika fani zetu za michezo. Nawapongeza kwa jitihada hizo na naomba Mwenyezi Mungu awasaidie yale ambayo wanayoyaomba basi wafanikiwe.

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo nitazungumza masuala mawili tu kwa sababu muda wenyewe ni mdogo. Suala la kwanza liko ukurasa wa 35 kifungu cha 39 Idara ya Michezo. Hapa Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa jitihada mbali mbali zinazofanywa na wizara kupitia serikali kukuza michezo yetu ya fani mbali mbali.

Lakini mimi leo nitazungumzia mchezo wa mpira wa miguu tu kwa sababu niliwahi kupita kwenye mchezo huu na nimeshaiwakilisha nchi yetu katika Timu ya Vijana ya Taifa mwaka 1975/76 nikitokea Mfeneseni katika timu moja inayoitwa *Action Brothers.* Nikiwa na wenzangu kutoka Msuka Karabai na Nassor Humoud tukachanganyika na wenzetu mjini kina Chimba, Thuwein, Abdulwakat na tukawakilisha nchi yetu. Kwa hivyo, mpira kidogo naufahamu ingawa sasa hivi tena umenitoka nachezea Baraza la Wawakilishi kama kujenga mwili tu.

Mhe. Mwenyekiti, mchezo wa mpira wa miguu hivi sasa ni ajira kidunia na hata hapa petu wako wachezaji hawajafika nje lakini ukitoka hapa ukenda Bara hapo ukanunuliwa pia umepiga hatua moja. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mchezo wa mpira una changamoto nyingi sana zinazosababisha tusiende mbele na leo nitatoa mfano wa mambo mengi kwenye huo mpira.

Mhe. Mwenyekiti, mimi bahati nzuri nina timu yangu katika jimbo ya *Mwakaje Rangers* iko kanda huu mwaka wa tatu lakini hatujapata kwenda kwenye daraja la kwanza. Sasa katika kanda hiyo kwanza kuendeleza timu kuna kazi nyingi sana. Kwa mfano, wakati wa ligi ikianza ule usajili kuchukua fomu kwanza ukalipe, ukirudisha fomu ukalipe. Wachezaji wote kama 21 upige picha ulipe kadi. *ZFA* huko. Ukenda kwenye mpira refa pia umlipe wewe unayekwenda na timu, wakati mapato yote yanayokusanywa na *ZFA* hawawezi kusaidia hata kumlipa refa.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano jimbo langu mimi tunachezea Kianga, lakini tukitaka kucheza na mtu wa Wilaya ya Kati tukacheze Hanyegwamchana. Tukitaka kucheza na watu wa Kaskazini 'A' twende tukacheze Kidoti. Tukitaka kucheza na watu wa Kusini tukacheze Bungi Miembemingi. Pahala karibu sana ni Kaskazini 'B' Mahonda. Sasa utakuta ukikusanya gharama zote hizo kama hukupata pahala pakuegemea timu inakufa.

Mhe. Mwenyekiti, ningelishauri kwa kutaka kukuza michezo basi lazima *ZFA* ikiwa Wilaya ya Magharibi ama mjini watupunguzie gharama katika kuandaa timu. Vyenginevyo tutazungumza siku zote lakini timu zitashindwa kwenda mbele hasa hizi za vijijini. Kwa sababu timu yangu ina uwezo mkubwa lakini kutokana na gharama kuwa kubwa tunashindwa kupanda daraja tuko hapo kanda huu sasa mwaka wa tatu tumeganda bahati nzuri hatuteremki. Mhe. Mwenyekiti, naiomba wizara matatizo kama haya wangeyaangalia wakazidi kutusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, isitoshe ukija kwenye vifaa vya michezo jezi za kawaida sasa hivi zinauzwa shilingi 100,000 *stocking* ukanunue kwengine, viatu vya mtumba sasa hivi unanunua shilingi 20,000 mpaka 30,000. Sasa tungeomba kama na hivyo vifaa vya michezo vinalipwa ushuru basi kwa kutaka kuendeleza michezo katika nchi yetu tungejaribu kupunguza ushuru, ili wale vijana wa vijijini na hata mjini wakaweza kununua vifaa vinavyokwenda na wakati kwa sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, tunachezea viatu vya raba lakini si viatu vya kuchezea mpira, raba ni viatu vya kufanyia mazoezi ya riadha basi. Mhe. Mwenyekiti, naomba na hili la vifaa lingetazamwa ili tukaweza kuziendeleza timu zetu kupata hiyo ajira lakini pia zikapata kupanda madaraja mbali mbali.
Mhe. Mwenyekiti, jengine bahati nzuri katika hiyo michezo jana nilisikiliza kipindi cha michezo, si kawaida yangu lakini kulikuwa kuna jambo linataka linipe habari. Katika kipindi kile walikuwa wanahojiana mtu wa michezo na kiongozi mmoja wa *ZFA*. Walizungumza kwamba hivi sasa nchini petu kaja

kocha wa mpira wa miguu na atakuwa na kazi mbili, kufunza timu yetu lakini pia kutoa mafunzo kwa makocha wa timu mbali mbali.

Sasa pakatokea swali lakini huyo aliyeulizwa akashindwa kujibu. Mhe. Mwenyekiti, naomba leo wizara ipo tupate jibu ili wananchi wapate kufahamu. Kwa sababu jana kwenye redio jibu halikutoka sahihi. Aliulizwa je, huyu kocha kaletwa kiserikali? Wakasema kocha huyu kuna baadhi ya wadau wa maendeleo na wafanyabiashara wamemleta. Akaulizwa tena je, mkono wa serikali upo? Akasema mpaka sasa hivi siwezi kujibu lakini wahusika wapo watajibu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kumeanza utata naomba tujue huyu kocha kama kaletwa kiserikali, kaletwa kwa muda gani, kwa mikataba gani na analipwa vipi, ili baadae yasije yakatoka mtu mwengine yakenda lawama serikalini. Tukiyajua mapema kidonda kabla hakijawa kikubwa tunaweza tukakitibu, kuliko kungoja kikawa kikubwa tukakata mguu. Mhe. Mwenyekiti, sasa hili jana limetoka nusu nusu kwenye kipindi cha michezo kwa hivyo leo wizara ipo tulipate kamili.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye suala langu la pili. Mhe. Mwenyekiti, sikuona kwenye bajeti lakini kwa kuwa ni kitu muhimu nimeona nikizungumze viwanja vya kufurahishia watoto kiliopo hapa petu na cha kule Pemba. Mhe. Mwenyekiti, huko nyuma bajeti iliyopita tuliambiwa kwamba wametokea wadau wa maendeleo wataviendeleza vile viwanja ili watoto waweze kufaidika navyo, lakini ukipita Kariakoo ni pembea mbili tatu zinazofanya kazi nyengine mbovu. Je, hawa wafadhili bado hawajaanza kazi. Kama wameanza ni kikwazo gani kinachosababisha pembea zote zisifanye kazi.

Mhe. Mwenyekiti, Pemba siwezi kuzungumza kwa sababu si mkaazi wa kule na sijaenda Tibirinzi. Lakini cha kunishangaza chengine hivi karibuni walikuja wenzetu sijui mabohora wale walikaa Haile Selassie kwa sherehe zao, bahati nzuri wakaja na mapembea mengi wakafunga kwenye bustani yetu ya Jamhuri, walipoondoka wakaondoka navyo. Lakini kuanzia mwezi huu tunakuta pembea zile zimerudi na tayari bustani yetu imeshaathirika sana. Kwa sababu bustani ile hivi sasa wanatumia watoto wote wanaosoma katika vyuo na skuli zilizokuwepo karibu na pale kwa kukaa na kufanya *discussion.*

Mhe. Mwenyekiti, pahala penyewe pana *Pemba grass* nzuri sana hata uvae suti nyeupe ukikaa basi ukiondoka huchafuki, lakini leo tayari pameruka vumbi. Sasa nilitaka niulize baina ya wizara na wizara wakati mnafanya taratibu moja kwenye nchi hamuambizani. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, juzi hapa mwenzangu alizungumzia katika Wizara ya Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ lakini jibu halikupatikana kwamba bustani yetu kwa hapa

Unguja Mjini ni ile pale, pana kivuli kizuri, watu wanakaa wanazungumza, watoto wanasoma, lakini hapo hapo imegeuzwa imetiwa mapembea na sasa hivi bustani inamalizika.

Mhe. Mwenyekiti, kama na mimi ni mzalendo wa nchi hii ningeomba wizara mbili zikae kama wanataka maeneo ya wazi mimi ninayo matatu nitatoa mfano hapa kama yatafaa basi pembea zitolewe zikapelekwe kule bustani ibaki katika hali ya bustani kwa sababu hatuna nyengine. Ukenda bustani ya Forodhani ile imejengwa watu usiku wakale nyama choma wastarehe wapunge upepo. Lakini sio hii hapa, hii mchana wote ukipita watu si chini ya 50 wapo, pana kivuli kizuri, miasumini, miwardi, vilua, sasa tunaivuruga kwa pembea.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nashauri kama pembea hizi wanataka wapewe watoto wacheze basi Michenzani mkabala na Idara ya Majenzi upande wa pili pana eneo kubwa sana, ligaiwe nusu tu ajenge fensi aweke pembea zake. Pale watoto wa Miembeni, Mwembeladu, Michenzani yenyewe watacheza.

Mhe. Mwenyekiti, ukija mjini sasa hivi *Auto Sale* hapa kwendea Bwawani tumefikia shimo nusu liko wazi hapana kazi yoyote na wajenge pale waweke pembea watoto wa Funguni, Malindi, Mchangani, Mbuyuni watacheza pale. Mhe. Mwenyekiti, ukija Amani mitaa ya ng'ambu huku nyuma ya jengo la Judo kuna eneo kubwa sana liko wazi na wajenge pembea watoto wa Magogoni, Amani watakwenda kucheza pale. Lakini bustani tukianza kuzigeuza na wakati tuko katika mambo ya kisheria mji wetu tutauharibu, itakuwa kichwa cha mwendawazimu kila mtu ajaribie. Mhe. Mwenyekiti, wizara mbili zipo na serikali wanasikia jambo hili lirekebishwe ili kuweka mandhari na haiba nzuri ya mji wetu.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 27 kifungu cha 25 Gazeti la Serikali lakini mimi nimekusudia Gazeti la Zanzibar Leo. Mhe. Mwenyekiti, gazeti letu kwa kweli hivi sasa linasomwa sehemu nyingi na linapata wateja wengi sana. Lakini tulisikia katika bajeti iliyopita kwamba tutaligeuza gazeti letu kutoka rangi nyeusi na weupe lije katika rangi za kawaida kama magazeti mengine.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru nadhani Jumamosi ama sijui Jumapili wanatoa gazeti la rangi linapendeza sana. Sasa katika bajeti hii sikuona kugusiwa lolote. Je, utaratibu wa gazeti letu kulitia rangi umeshindikana. Kama umeshindikana tupatiwe jawabu wakati wa majumuisho ni kwa nini. Kwa sababu ruzuku inatoka serikalini kuliendesha gazeti. Mhe. Mwenyekiti, hili nikipata jibu na wenzangu watasikia. Lakini gazeti la rangi kwanza linavutia na halafu linapata wateja wengi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kipindi kilichopita kwenye bajeti lilikuwemo lakini safari hii sikuliona ni kuhusu Kiwanda cha Uchapaji. Hapa mwanzo kiwanda chetu hichi kilichopo kwa Abass Hussein kilikuwa kina matatizo mengi sana ya kuingia maji lakini tunashukuru kimetengenezwa maji hayaingii. Lakini tulitaka kununua kiwanda cha kileo Mwanakwerekwe na kilinunuliwa nikasikia paliingia hitilafu na watu wamepelekana Mahakamani. Mhe. Mwenyekiti, kwenye kitabu sikuona kitu. Je, tumeshindwa juu ya kiwanda kile kukinunua amepata huyu mtu tuliyeshtakiana nae ama kuna tatizo gani. Kwa hivyo, naomba na hapa pia nipate maelezo ili niweze baadae kuzungumza na hawa watu ambao wanahoji suala kama hilo.

Mhe. Mwenyekiti, halafu nikiendelea nije kwenye sehemu ya mapato ya wizara, kuna sehemu ya mapato ya wizara katika kitabu hiki ukurasa wa 47 imeeleza hapa kwamba Idara ya Habari Maelezo fedha zilizopangwa kukusanywa ilikuwa ni milioni 7,008,000 lakini fedha zilokusanywa hadi hivi sasa ni milioni 5,449,000 ni sawa na asilimia 69, hiyo angalau kidogo imevuka lengo, lakini Idara ya Televisheni wao wamekusanya asilimia 12, kwenye milioni 70 wamekusanya milioni 9,065,000.

Mhe. Mwenyekiti, ukija kwenye Idara ya Sauti ya Tanzania Zanzibar imekusanya asilimia 26, walikadiria mapato ya milioni 70, lakini wamekusanya milioni 18.5. Ukija Idara ya Uchapaji halkadhalika, mpaka mwisho gazeti halafu na chuo cha habari. Sasa utakuta makadirio haya mnayapanga wenyewe lakini mnashindwa kukusanya. Kwa hivyo, tulikuwa tunataka kujua tatizo ni nini, kuwa labda katika matangazo hatupati wateja, katika magazeti hakuna wateja au ni kipi kinachokwamisha kwa sababu mapato tunayapanga wenyewe lakini hatuyafikii malengo. Nilitaka nipate sababu kama zipo ili tuweze kutoa michango yetu katika hali hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na kumalizia mchango wangu, nije juu ya suala zima la Baraza la Sanaa, kwenye ukurasa wa 34. Imeelezwa hapa kwamba kifungu cha (iii) ya kirumi. Kutoa mafunzo ya sanaa kwa vijana wenye vipaji maalum ili kuweza kuendeleza vipaji hivi.

Mimi najiuliza Mhe. Mwenyekiti, wenzetu Bagamoyo Tanzania Bara wamejenga chuo maalum cha sanaa, unampeleka mtu pale anapikwa na anatoka kawiva. Lakini kwenye kitabu tunaambiwa tutakusanya vijana wenye kipaji kuendeleza sanaa. Tutawakusanyia pahala gani wakati hatuna jengo, majengo tuliyonayo ya uwanja wa mpira wa Aman na Pemba sioni pengine. Sasa nilikuwa nataka nijuwe kuwa hawa watakusanywa kwenye eneo gani ili waweze kuendelezwa hatimaye tukafikia kwenye hayo malengo. Maelezo mazuri lakini nashindwa kujua sijui utekelezaji utakuwaje.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa nije katika kanda zetu za CD hizi ambazo tunaambiwa kuna baraza maalum linaangalia kanda hizi ili kuona kama zina matatizo katika jamii yetu, basi ni kufutwa kabisa michezo ile. Lakini sasa hivi maduka haya sasa hivi yameenea sana hapa nchini kwetu na sijui ukaguzi huu unafanywaje. Kwa sababu mimi nimeona kanda nyingi tu, bado naona wanaohusika na ukafuzi wa hizi kanda nadhani walipitikiwa na nyengine zinaoneshwa kwenye TV. Mfano kama umekaa na familia yako basi inabidi uondoke kidogo kidogo ujipe sababu, useme kama kuna mgeni nje au unakwenda haja, kutokana na yale mambo ambayo yanaoneshwa pale.

Mhe. Mwenyekiti, nitatoa mfano mdogo sana ambao unasababisha kuleta athari katika jamii yetu. Niliuona mchezo mmoja umerikodiwa na wenzetu wa Dar es Salaam, wenyewe wanamuita *staring* Ray, yeye huyu kijana alikwenda kusoma nje kisha akapata mchumba wa kabila nyengine na yeye ambaye ni Mchina, sasa alipomleta huku kwao kutaka kumuoa akataka lazima apitie katika utamaduni wa huku kwetu, kwenye familia yao. Ilikuwa ni kubwa kwamba ni lazima afanyiwe tohara wakati yeye ni mwanamke na kwao ukishafanya hivyo ndio unapata kumuoa. Yule mwanamke alifanya tabu sana lakini baada alikubali. Siku aliyofanyiwa tohara anarudi katika hicho kitendo basi miguu yote imeroa damu. Sasa mtu yeyote ukikaa na mwanao atafasiri vyengine akiona kitu kama kile.

Kwa hivyo, utakuta michezo ni mzuri na inaelimisha lakini baadae inapotosha. Kwa hivyo, ningeomba bado mabaraza yanayohusika na kukagua hizi kanda zingeangalia zile kanda ambazo ziko katika hali nzuri ndio zioneshwe katika jamii. Hizo kanda zinauzwa na watu wanaangalia. Utakuta mchezo ni mzuri lakini unaharibika pahala padogo tu. Kwa hivyo, nashauri Mhe. Mwenyekiti, mambo kama haya lazima tuyazingatie kwa kulinda utamaduni wetu.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi mwenyewe binafsi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini tunaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja, nakushukuru sana.

Mhe. Ali Denge Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na mimi leo nichangie Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo. Kabla ya hapo kwanza Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Naibu Waziri Kiongozi kwa umakini wake na umahiri wake wa kuamua kuchukua fomu ya Urais.

Mhe. Mwenyekiti, hata michakato bado, sasa hivi tumeshakuwa na muelekeo. Kwa hivyo, tukijaaliwa na Mwenyezi Mungu huwenda Inshaalla atamkubalia maombi yake hayo. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze wizara hii kwa juhudi yake kubwa inayochukua katika taasisi zake zote ilizokuwa nazo ndani ya wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 34 kifungu cha 37 Baraza la Sanaa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, suala hili vijana wetu wanajitahidi kubuni na kusanii mambo mbali mbali. Utakuta hapa kwetu Zanzibar sasa hivi kuna vijana wengi wameibuka na masuala haya ya usanii na kubuni mambo mbali mbali katika kufanikisha shughuli zao hizi za usanii. Lakini tatizo lililokuwepo mara nyingi wana lalamika, baada ya usanii wao wakishatayarisha, wakati wa kupeleka kwenye habari za kurusha huwa wanacheleweshwa hawapati kurusha kwa wakati, wengine wanakuwa hawapokelewi. Sasa utakuta hili likiwa linatokezea basi tunawavunja moyo. Kwa hivyo, ningewaomba wahusika wa urushaji au utangazaji basi wawe karibu na hawa wasanii ili kupata kukuza vipaji vyao.

Kama inavyoeleweka nchi ikiwa na wasanii na wabunifu mbali mbali basi inaleta baraka na vile vile inakuwa ni mvuto kwa wageni mbali mbali wanaotembea katika nchi yetu. Kwa hivyo, ningewaomba wahusika wa kitengo hiki wakajaribu kutoa taarifa mbali mbali kwa wasanii hawa kwa kila wasanii waliokwishakuwa tayari, basi wajisajili au waripoti kwa wahusika ili watambulikane na wapate kufuatiliwa na kupewa miongozi midogo midogo ili kuimarisha usanii wao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sehemu hii ya usanii ningeomba Mhe. Waziri akafanya taratibu hizo ili tupate wasanii wa uhakika na kupata kuleta matumaini katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 35(iii) Idara ya Michezo. Katika kuibua na kuendeleza vipaji vya wana michezo mbali mbali katika nchi yetu, kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, kwa muda mrefu sana wanajitahidi sana wana michezo wetu kuchezesha michezo mbali mbali hasa katika michezo ya mipira. Utakuta sasa hivi katika muda mrefu sana timu zetu hizi hazijatajika kama zinavyotajika timu za wenzetu baadhi ya nchi mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi tukicheza mipira yetu tukifika katika kombe la Afrika tu huwa mara nyingi tunatolewa mapema. Kwa hivyo, utakuta kulinaga na hali ya nchi yetu ilivyo na wanamichezo walivyo, kwa kweli inaleta sikitiko kweli kwa vile tuna mikoa zaidi ya mitano na hatujapata timu iliyoimarika ili tukajua na sisi tuna timu ambayo inaimarisha na kujulikana kwa Zanzibar nzima.

Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi timu zetu hizi kama nilivyosema zikishafika ngazi ya kutoka Afrika tu huwa hazina ushindi. Mara nyingi watu wanasema vijana wa Zanzibar kwa kula vyakula vyao vyenye siha kwa hivyo wanaonesha na ukakamavu wa kufanya michezo yao vizuri. Kwa hivyo, suala hili namuomba Mhe. Waziri aliangalie vizuri sana, kama tunavyosifiwa kuwa

vyakula vyetu vinaleta rutuba na zaidi tukipata michuzi ya pweza, kwa hivyo timu zinakuwa imara sana. Kwa hivyo, Mhe Mwenyekiti, ingeomba Mhe. Waziri alisimamie sana hili ili tupate wanamichezo angalau kwa kila mkoa itoke timu ambayo iko imara. Halafu katika mikoa hiyo zichanganywe timu na tuwe na timu moja ya Zanzibar ambayo tunahakikisha tunajitahidi kuimarisha hiyo timu na kuwaangalia wachezaji wake ili na sisi tuwe na tishio katika Bara la Afrika.

Mhe. Mwenyekiti, kama tutafanya mikakati na kuwa na timu kama hiyo, basi naamini na sisi katika kombe la dunia la miaka ijayo tunaweza tukaingia, kwa kuwa tuna vijana wengi na waliokuwa makini kabisa katika kusimamia haya masuala ya michezo. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri akaliangalia sana hili, baada ya kipindi hiki cha kombe la dunia na sisi katika kipindi kijacho angalau tufikie katika hatua hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 29 kifungu cha 27(iii) kuhusu kuratibu shughuli za utangazaji Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niwapongeze watangazaji wetu wote wa redio na televisheni kwa ukakamavu wao wa utangazaji ambao hauna ubaguzi, wanajitahidi sana kwa hali ya mfumo wetu tulionao wa vyama vingi, kwa hivyo kwa kila chama kinachopeleka taarifa zake huwa wanajitahidi kutangaza kikamilifu. Kama katika michakato hii ya uchaguzi unaokuja wa kura za maoni, hapo nyuma niliwasikia kidhati kabisa chama cha CUF wakimtangaza Maalim Seif Shariff Hamad kuwa anachukua fomu za Urais na siku aliyorejesha wakamtangaza. Kuja michakato ya chama cha CCM nao wagombea wote waliochukua fomu za kugombea Urais kwa ngazi hii kwa kuwa ni wengi na wao pia wamejitahidi kuwatangaza bila ya ubaguzi wowote. Kwa hivyo, kwa hili nawapongeza waandishi wa habari wetu kwa juhudi yao kubwa hiyo wanayochukua bila ya ubaguzi katika michakato hiyo.

Mhe. Mwenyekiti isipokuwa tu kuna baadhi ya vyombo vya habari ambavyo vyengine ni vya kibinafsi, mara nyingi ningewaomba wajitahidi na wawe na juhudi zaidi kutoa matangazo jinsi wanavyoletewa na wateja wao, basi wayapime na wayaangalie vizuri. Hivi sasa umekuja wakati wa kubomoana. Mtu atakuja tu kwa kuwa anajua hiki ni kitengo cha binafsi kwa hivyo bila ya kujitambulisha au kuwa na shahada yoyote basi anarusha habari zake, kwa hivyo matokeo yake inakuwa ni usumbufu kwa wale waliokuwa wamekusudiwa kubomolewa.

Kwa hivyo, ningewaomba wakatumia utaratibu mzuri zaidi, kwa kuwa tuna vitambulisho kwa hivyo vizuri yule anayekuja kutoa taarifa au matangazo yake basi akaulizwa kitambulisho chake na jina lake ili pindi yakitokea yale masuala anayorusha kuwa sio mazuri au kufuatiliwa na kupata uhakika, basi aweze

kutambulika ametokea wapi au ni nani. Kuliko kuchukua ukarusha tu bila kujua, halafu baadae anakutia matatizoni wewe mtangazaji. Kwa hivyo, ningeomba katika vyombo vyetu vya habari hivi vyote kabla ya kurusha matangazo yao kwa yule mlengwa wakawa na ushahidi wa vitambulisho vyake ili kuwa rahisi kuja kumfuatilia.

Vile vile katika taratibu hizi za utangazaji Mhe. Mwenyekiti, nawapongeza sana watangazaji wa kipindi cha mawio. Kwa kweli kile kipindi ni kizuri kinafurahiwa na wananchi wengi na wanakipenda ikifika wakati ule basi kila mtu anawacha yake anakaa pale kwa kusikiliza habari mbali mbali ambazo zimetokea katika nchi yetu. Kwa hivyo, watangazaji wa kipindi kile na watayarishaji nawapongeza sana. Hususan akiwemo mmoja yule jina lake anaitwa bwana Suleiman Juma Kimeya, halafu kuna bwana Hamad Maulid Hamad, nawapongeza kwa juhudi zao kubwa wanazo chukua.

Mhe. Spika, isipokuwa Mhe. Waziri nitaomba hawa watangazaji wetu wanaofuatilia habari hizi, kama hali itaruhusu basi wapatiwe vipando, japo vipando vidogo. Kuna vespa au ciao ili kufuatilia kazi zao zile wakamilishe kwa ukamilifu.

Mfano kuna mtu mmoja nampongeza sana anaitwa Haji Ramadhan Suwed wa TVZ, huyu kama utamuhitaji dakika hiyo hiyo anafika kwa kuwa anao usafiri. Kwa hivyo, na hawa kwa upande wa hii ngazi ya mawio ningemuomba Mhe. Waziri kama hali itaruhusu na wao watafutiwe usafiri ili kupata kukamilisha kazi zao. Kama inavyojulikana matangazo mbali mbali yanayotangazwa katika vyombo vyetu hivi, vinakuwa vinatangaza nchi na wizara hivyo inaleta faida mbali mbali katika nchi yetu. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri na hawa wakafikiriwa kwa kupewa nyenzo hizo ili wakapata kuhudumia kazi zao vizuri kama ilivyotarajiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala la Uwanja wa Amani. Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Mhe. Rais kwa kukabidhiwa uwanja huu. Kwa kweli Uwanja wa Amani umejengeka vizuri, umefanyiwa ukarabati mzuri, unafurahisha na kulingana na hilo jina lake ni Uwanja wa Amani kweli.

Kwa hivyo, ninachokiomba kwa kuwa ule uwanja umetengenezwa kwa gharama kubwa na uko katika hali nzuri. Kwa hivyo, kamati husika ya Uwanja wa Amani iunde kamati maalum ili kupata kuusimamia uwanja ule ili kila linaloharibika wawepo karibu kulirekebisha au kulirejesha. Isiwe limeharibika jambo linaachwa kwa muda wa miaka miwili au mitatu linaambukiza na jengine. Kwa hivyo, ningeomba kwa kuwa uwanja tumetengenezewa mzuri na wa kileo. Hivyo kamati hii ingezidisha kazi zaidi ya usimamizi, angalau ule uwanja ufikie mnamo miaka 10 au 15 uwe katika hali ya kuridhisha. Kwa

hivyo, wawe karibu sana na matokeo mbali mbali yatakayotokezea ambayo yatahitajika kutengenezwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika Tanzania yetu hii na sisi tutajigamba tuna uwanja wa uhakika wa kuchezea wanamichezo wetu. Naomba Mhe. Waziri uwanja tumeshakabidhiwa, hivyo tuwe karibu nao kwa kuushughulikia kwa mambo mbali mbali ambayo yatatokezea ndani ya uwanja ule.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala la utamaduni. Kama baadhi ya wajumbe wenzangu wengi waliokwishakuzungumza na mimi nitaliongelea suala hili la utamaduni. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tuna nyanja nyingi za mambo ya utamaduni, kuanzia mijini mpaka vijijini. Kuna vijana wetu na watu wetu mbali mbali wanaimarisha utamaduni wetu huu katika vijiji na katika miji. Isipokuwa kitu muhimu kinachotakiwa ni kuhifadhiwa hao wahusika na mambo hayo ya utamaduni na kupewa taaluma na elimu mbali mbali ili kuimarisha utamaduni wetu. Kama inavyojulikana nchi ikiwa na utamaduni ndio inaleta mvuto kwa kupata wageni na watu mbali mbali ili kuja kuangalia hali ya utamaduni wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Naibu Waziri wa wizara hii, kwa juhudi yake kubwa anayoichukua, kila ikifika siku za utamaduni basi huwa anahamasisha sekta mbali mbali na mara nyingi huwa anawakusanya washiriki mbali mbali, kwenye maeneo ya Forodhani ili kuangalia hali ya utamaduni wetu. Vile vile ikifika siku za mwaka kogwa ule huwa baadhi ya watu wengi huwa wanaelekea sehemu za Makunduchi kwa ajili ya kuangalia na kutizama shughuli za utamaduni mbali mbali ambazo zimeandaliwa na wananchi. Kwa hivyo, ningemuomba kwa suala hili wangefanya utaratibu zaidi ili kupenya na kuangalia sehemu gani kuna mambo ya utamaduni katika nchi yetu na kuyaimarisha.

Mhe. Mwenyekiti, nina mengi lakini kwa kuwa muda ni mfupi. Kwa hivyo mimi naona kwa hapa nilipofikia panatosha, naunga mkono hoja hii mia kwa mia na kwa kushirikiana na wananchi wenzangu wa Jimbo la Amani, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi asuhuhi hii ya kuweza kuzungumza kidogo. Lakini nitakuomba radhi sitosimama.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niwapongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kazi zao nzuri ambazo wanafanya za siku hadi siku. Mhe. Mwenyekiti, nitazungumzia kidogo tu sitaki nizungumze sana. Nitaanza katika Idara ya Televisheni kwenye ukurasa wa 24.

Mhe. Mwenyekiti, ni vizuri sana idara hii inavyofanya kazi zake na televisheni Mhe. Mwenyekiti, ni muhimu sana hasa kwa wakati wetu huu tulionao na vizazi vyetu. Lakini nina masikitiko sana televisheni hii sisi Pemba hatupati, tuna kilio kikubwa cha kila siku juu ya televisheni hii. Ukitaka kuiona basi uje hapa, tunaona mambo mengine mbali mbali lakini kwa hapa kwetu sisi wenyewe hatujioni. Hasa kwa wakati huu tuliofika. Kwa hivyo, tunaomba televisheni hii iweze kufanyiwa marekebisho na kuboreshwa zaidi ili na sisi Pemba tuweze kuona yale mambo ambayo tunayahitaji.

Kwa mfano. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi inakaribia siku za uchaguzi watu wanajieleza na kuna ambao wanagombea nafasi za Urais wanajieleza, lakini wewe husikii kitu chochote, usikie tu habari kwa watu. Kwa hivyo, haya ni mambo ambayo yanatukwaza sana watu wa kisiwa cha Pemba. Halafu na hawa watendaji nawapongeza sana, naomba watendaji hawa waweze kuboreshwa na kupata msukumo mkubwa wa vitendea kazi ili kuweza kufanya kazi zao za siku hadi siku. Watendaji hawa wanafanyakazi kwenye mazingira magumu, Pemba kama tunavyoijua, hivyo tunaomba watendaji wetu waweze kupewa kipaumbele ili waweze kufanya zile shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nije kwenye Idara ya Habari Maelezo. Mhe. Mwenyekiti, hapa inajieleza kuwa habari maelezo ni kazi nzuri sana ambayo tunajisikia yale yanayofanywa. Maelezo yanayotoka na mambo yanavyoelezwa katika redio na mambo mengine. Watu tuliokuwa nao katika shughuli hizi basi tuweze kuwavuta ili hawa watoto wenye vipaji vya kuweza kutuboreshea mambo haya tuwe nao karibu. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, kila jambo linataka kipaji, huwezi tu kufika pale ukaeleza, lile ambalo hulijui na unalolijua. Lakini hawa ambao kuwa Mwenyezi Mungu amewapa kipaji hiki *Inshaallah* namuomba Mhe. Waziri aweze kuwaona na kuweza kuwavuta, tusiwe ile tunasema kuwa tunawasomesha watu halafu waondoke waende kufanya kazi kwengine. Hivyo wawezeshwe na waboreshwe ili waweze kuvutika na wao kufanyakazi katika nchi yao.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nije katika Bodi ya Sensa. Mhe. Mwenyekiti, hii ni kazi nzito na tuliipitisha hapa na tayari bodi iko iliyochaguliwa. Hivyo namuomba Mhe. Waziri itakapofanyika shughuli ya bodi basi na zile kazi zinazofanywa tukahakiki zile kanda. Mimi ningeomba hizi kanda zisajiliwe. Kwa sababu muna kanda ambazo watu wanazipenda huoneshwi zinafichwa kabisa. Ndio kama Mhe. Mjumbe hapa aliposema kuwa wengine wanafanya mambo yaliyokuwa hayastahiki katika nchi yetu. Lakini zitakaposajiliwa zile kanda basi mtu atajua kanda gani ya kuitumia na atakapoitumia kanda iliyokuwa haijasajiliwa basi itajulikana. Kwa hivyo, wawezeshwe kwa sababu maduka ni mengi sana yanayofanya kazi hizi.

Ukenda kwenye duka moja, basi kwa siku mbili huwezi wewe ukaziakiki kanda na ukaweza kuzijua.

Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Waziri kanda zitakapofanyiwa kazi basi pawe na ruhusa ya kuambiwa watu kuwa kanda zisajiliwe kama vile tulivyosajili simu basi na kanda hizi zisajiliwe madukani.

Vile vile nije kwenye Baraza la Kiswahili. Jamani Kiswahili kweli sisi tuliozaliwa hapa kwetu Zanzibar, mtoto ashindwe na mtihani wa Kiswahili. Lakini tuna hakika kuwa Kiswahili kimechanganyika hapana Kiswahili fasaha na watu hawajuwi lugha yao ya Kiswahili katika nchi yao, jinsi mambo yalivyochanganyika. Watoto katika kusoma basi huyu ana Kiswahili chake na huyu ana Kiswahili chake, watoto wanaigana. Mtoto anaiga Kiswahili ambacho kuwa yeye hakiwezi kumpa maana katika nchi hii. Kwa sababu tuna mifano mingi ya mambo ya Kiswahili watoto wanayoyaiga. Akitoka tu mtoto akisogea mbele kidogo tu basi anaacha maneno ya hapa na kuiga maneno ya nchi nyengine.

Kwa hivyo, tunaomba Kiswahili kiweze kuboreshwa na kitiliwe maanani ili watoto wa Zanzibar waweze kujua maana ya Kiswahili katika nchi yao. Kwa sababu ndio lugha yetu tunayoizungumza na tunakokwenda kwengine basi wenzetu wakiwa wanazungumza basi wao wanawakalimani kuwafahamisha watu. Kwa sababu gani sisi wakija watu hapa tunawacha kuzungumza Kiswahili na tunawaiga wao, basi na sisi tuweke wakalimani ili tuweze kuzungumza Kiswahili na wao wafahamishwe kwa Kiswahili ili wafahamu ndio lugha yetu hii tusiitupe Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo kidogo nitakuja katika utamaduni. Mhe. Mwenyekiti, tunajua kuwa tamaduni zinatupana, kila pahala na utamaduni wake. Sisi tuna utamaduni wa kivazi, malezi na hata ngoma zetu tulizonazo. Mhe. Mwenyekiti, nikikuambia kuwa utamaduni unakufa kwa sababu ya kuigiza mambo mengi ambayo tunayaona, watoto wanaiga yale ambayo wanayaona kwa wenzetu. Kivazi cha kwao watoto wanakiacha na kuigiza kivazi, utaona kwenye TV mule watu wanakuja na vivazi vya maajabu basi watoto wawacha na kuiga hivyo. Hawawezi kufuata kivazi cha kwao ni mtihani jamani msituone hivi, wanawake tuna ulezi mgumu majumbani kuweza kuwadhibiti watoto kwa maigaji. Watoto wanaiga mambo ya maajabu.

Kwa hivyo, tunaomba televisheni yetu iweze kutoa kipindi cha kivazi cha Kizanzibari maalum. Mtu amejikatia kanga, amejitanda na kuweza kutoka ili watoto wajuwe kuwa kile ndio kivazi chetu cha Zanzibar. Sio kuwa tujivalie tu ovyo ovyo na watoto wanaiga.

Mhe. Mwenyekiti, pia ngoma za kwetu nazo zinakufa hivyo hivyo. Hakuna ngoma za asili kama ngoma za misundo, taarabu na nyengine zote hakuna. Sasa hivi utasikia magoma yaliyokuwa hata huyajui yanaanzia wapi na kumalizia wapi. Tuweke vipindi katika televisheni na katika redio ili kuzipiga zile ngoma za kizamani ili mtoto ajuwe kuwe ngoma hii ilikuwa ikipigwa katika nchi hii, msondo na ngome nyengine ili watoto wazijuwe ngoma zao za hapa nchini kwao. Isiwe saa sote tunatizama marusha roho na sijui mambo gani, na hizo roho zinarushika kweli. Kwa sababu wewe mwenyewe ukiona kivazi kinachovaliwa, watu wanajenga uwa kisha wanavua nguo mule ndani wanarusha roho, hizo ni ngoma. Sasa tunaomba utamaduni wa Kizanzibari urudi kwa kutangazwa katika maredio na televisheni ili watoto wajuwe ile stahiki ya nchi yao hasa waijuwe. Kwa sababu sisi tuliolelewa tunajua kivazi cha kwetu na utamaduni wetu, lakini watoto wetu sasa hawajui kitu chochote wanakwenda na wakati.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mengi nilitaka nieleze tu kidogo, na mimi nizungumze wakati afya imeniruhusu. Kwa hivyo, naunga mkono hotuba hii ya waziri kwa asilimia mia kwa mia pamoja na wanawake wenzangu na nawatakia kila la kheri, Mwenyezi Mungu atujaalie kipindi kinachokuja awe yeye ndiye rais wetu. *(Makofi).*

Mhe. Omar Ali Jadi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa hai na kuwa wazima wa afya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ni wizara muhimu sana katika nchi yoyote. Kwa mfano, wizara hii kama inataka kuipotosha jamii basi nchi inaweza kubadilika kwa dakika tatu tu, pia ikiwa inataka kuilekeza jamii, basi inaweza kuwaelekeza na nchi ikaneemeka kwa dakika mbili tu.

Kwa hivyo, ninaamini Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo ni mtu ambaye ni mahiri tena mwenye kuzijua kazi zake kwa ufasaha. Mhe. Mwenyekiti, kwa hili napaswa kumpongeza yeye, Mhe. Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake wote kwa namna walivyojitahidi.

Vile vile naamini hakuna binadamu ambaye hana kasoro na hiyo ndiyo sifa ya binadamu, kama kuna binadamu ambaye anasema amekamilika, basi yeye ndiye mwenye upungufu. Lakini sifa ya binadamu kuwa na upungufu wa mambo yake, hata akijipanga vipi lazima kuna mengine atayakosea. *Inshaallah* namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie Mhe. Waziri ampe yale anayoyataka tena yawe ya kheri kwake pamoja na neema kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa kuzungumzia kuhusu Viwanja vya Kufurahishia Watoto. Kwa kweli watoto ndio furaha yetu wazazi inapofika siku yao ya sherehe katika nchi, wakiondoka majumbani na kwenda kujumuika na wenzao. Lakini tumewasahau watoto katika sherehe zao kuwatengezea yale yanayowahusu na kuwafurahisha roho zao.

Kwa mfano, Kiwanja cha Kufurahishia Watoto cha Tibirinzi, kwa kweli kimepoteza haiba pamoja na mwelekeo. Kiwanja kile wakati nilipokuwa mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii nilikitembelea mara mbili na kila tunapokwenda, basi hali ilikuwa hairidhishi. Lakini mpaka wajumbe wa kamati hii ambao wapo hivi sasa, kila mmoja mwenye kwenda kukiangalia machozi yanamtoka. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, isingekuwa vyema fedha zote za serikali zilizotumika kwa ajili ya kujenga viwanja vile halafu tukaviwacha vikapotea. Kwa hivyo, ni vyema angalau kwa miaka miwili au mitatu kuchukuliwa japo kiwanja kimoja cha watoto na kukarabatiwa, ili wakati unapofika, basi watoto wakapata kufurahi roho zao.

Vile vile tukiangalia Kiwanja cha Kufurahishia Watoto cha Kariakoo, labda ile Siku ya Sherehe yenyewe kwa sababu watoto wanakuwa wamevaa kanzu mpya pamoja na rangi mpya, lakini kiwanja chenyewe nacho kimepoteza haiba.

Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti na kwa sababu anaelekea kwenye mchakato wa urais na watoto dua zao ni kubwa, angalau avitupie macho, ili dua za watoto zimfikie na yeye kesho kutwa awe rais wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye Idara ya Upigaji Chapa. Kwa kweli Mhe. Waziri ameeleza maelezo pamoja na mipango ya mwaka 2010/2011 yakiwemo kuwasomesha wafanyakazi, kuvifanyia matengenezo vifaa vilivyomo, lakini amelisahau kama jengo nalo ni bovu linalowekwa vifaa vile.

Nadhani ingekuwa ni vyema vifaa vinataka kutengenezwa na jengo nalo likatengenezwa, kwa lengo la kulingana na wakati pamoja na vile vifaa ambavyo vitatengenezwa.

Sasa niende katika Sauti ya Tanzania Zanzibar. Mhe. Waziri kwenye malengo amesema kwamba itatoa burudani kwa wananchi pamoja na shughuli za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2010. Mhe. Mwenyekiti, mwanzo nilisema kama habari zitapotoshwa na vyombo vya habari basi kwa dakika tatu nchi

itaharibika na ikiwa zitakuwa za kuelimisha basi pia nchi kwa dakika mbili inaweza kutengenea.

Lakini nimeshtushwa kidogo na sijui kama kuna fungu jengine ambalo limetengwa au litatengwa baadaye, kwenye miradi hiyo nimeona fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Sasa naomba kupata jibu wakati atakapokuja Mhe. Waziri kufanya majumuisho, kama fedha hizi zitatoka huku au tumeziondoa pale na kuziweka sehemu nyengine. Kwa mujibu wa utaratibu fedha za miradi ya maendeleo basi huwa tunaangalia fedha za matumizi ya kawaida, lakini za maendeleo angalia kiambatisho namba fulani. Kwa hivyo, katika Sauti ya Tanzania Zanzibar sikuliona Fungu la Maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri na kwa sababu tayari ameshaandaa pale kwamba atasomesha wafanyakazi pamoja na kununua vifaa vipya. Sasa fedha hizi zitatoka wapi au ziko sehemu gani?

Nikiondoka hapo sasa nije katika Idara ya Michezo. Kwa kweli michezo ni jambo muhimu sana katika nchi yetu, hivi sasa dunia inakua na michezo aina tofauti, isipokuwa mpira wa miguu umezidi wenzake katika vipimo vya michezo.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kwetu Zanzibar katika miaka ya nyuma kidogo, tulikuwa na michezo ya aina tofauti, yaani ukitoka kuangalia mchezo wa mpira wa miguu, unakwenda sehemu nyengine kuangalia mpira wa kikapu, lakini hivi sasa michezo mingi imeachwa.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho anieleze, kwa sababu gani michezo hii tukaiwacha na ile mingine ambayo inayotaka kuendelezwa nayo pia imeachwa, nahitaji sababu za msingi.

Ninavyokumbuka mimi ilikuwa akitolewa ng'ombe Pemba na kuja Unguja kwa ajili ya watu kucheza Mchezo wa Ng'ombe. Kutokana na hili wafugaji walikuwa wanafurahika na kila mmoja alikuwa anashawishika kufuga ng'ombe ambaye awe mkali sana kushinda wenzake, ili naye apate kuja Unguja angalau kwa kutembea.

Vile vile kulikuwa na watu ambao wakishajihika kwenda pale na mkeka wake, kwa ajili ya kumcheza ng'ombe na watu kupata kufurahika. Nakumbuka kulikuwa kuna ng'ombe mmoja akiitwa kipole ambaye alikuwa ni mkali ajabu.

Mhe. Mwenyekiti, samahani nataka kutoa mfano tu, kulikuwa na mtu na mpenzi wake, kwa bahati nzuri akasema mpenzi wangu nataka anichezee ng'ombe yule, ili nifurahike roho yangu na watu waone kama mpenzi wangu kweli ni mchezaji.

Sasa kulikuwa na nyimbo moja Mhe. Mwenyekiti naomba kuinukuu, ng'ombe yupo uwanjani ametanza hana mtu wa kumfika sasa anapigana na masikio yake, basi mwanamke akaitoa nyimbo. Kwa hivyo, alisema "aliyemchezaji kweli leo akamchezee ng'ombe kipole amebakia uwanjani na upembe mmoja wa tembe".

Kutokana na hali hiyo, yule mwanamme alitoka na zile kanzu za zamani bila ya kujielewa. Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoka mwanamme akiwa hajifahamu, lakini kwa sababu ameshaambiwa aliyewangu aende basi alikwenda kupigwa kichwa na mbavu zote zikavunjika na mapenzi yake yakamalizia pale na yeye akawa mgonjwa kitandani *(Kicheko)*.

Sasa ilikuwa ni furaha na watu wakihamasishana, lakini michezo ile hivi sasa imekufa. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri kwa kuwa kila nchi inazo aina za michezo, kwa mfano wenzetu wanacheza michezo mbali mbali na sisi michezo yetu ya ng'ombe. Vile vile kulikuwa na michezo ya kware na yote hivi sasa imekufa.

Suala jengine Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa na mashindano ya kuogelea na hivi sasa duniani yamekua na kwetu Zanzibar yamekufa.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa mjumbe wa kamati hii Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Naibu Waziri, waliwahi kuniambia sasa tunataka kuingia kwenye mashindano hata ya madau, watayarishe watu wako wakati wowote. Lakini mpaka leo hatujakutana na kuulizana imefikia wapi.

Kwa hivyo, ninaomba Mhe. Mwenyekiti kwa sababu michezo ni vipaji, vivutio pia ni rasilimali kwa watu wakati unapokuwa na mawazo, basi unaweza kwenda kwenye michezo na kupunguza mawozo. Mhe. Mwenyekiti, naomba michezo tuikuze pamoja na kuifufua na kuendeleza michezo yetu.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kwenye Baraza la Kiswahili. Kwa kweli Lugha ya Kiswahili ni kubwa sana na kwenye ukurasa wa 38 Mhe. Waziri amesema kwamba Jumuia ya Afrika ya Mashariki itakuwa na ubunifu wa lugha zao katika maeneo.

Sasa ingekuwa ni vyema sio lugha ambazo watachukua wale watu wanaopanga makamusi. Lakini Mhe. Waziri angewaandaa watu maalum kupitia maeneo

mbali mbali katika nchi yetu, kwa lengo la kujua utafiti wa lugha katika maeneo, baadaye kukusanywa na halafu tukapata kitu kimoja cha kutumia.

Mhe. Mwenyekiti, hili nalitolea mfano kila leo. Kwa mfano, leo anaweza kuja Mzungu hapa akaijua lugha inayotumika Zanzibar katika maeneo mengine, lakini mimi kama Mzanzibari ikawa siifahamu. Nadhani alikuja Mzungu mmoja wa Kimarekani mwaka wa 1997 ambaye ni mtafiti wa lugha, wenzangu wakati wa chakula cha mchana kwa bahati nzuri mwenzangu aliniambia anahitaji vushuka, nikaangalia vishuka vitaula vidogo vipo, lakini vishuka sivielewi.

Kwa hivyo, tulikaa na kuhangaishana huku watu wanapika jikoni, matokeo yake aliniambia chakula cha mchana. Kutokana na hali hiyo, basi nilimuuliza lugha hiyo umeikota wapi, aliniambia hii nimeikuta sehemu za Micheweni huko. Mhe. Mwenyekiti, mimi lugha ile siifahamu kama Mzanzibari, lakini mtu mwenye kutoka Amerika anaijua lugha ya mitaani kwetu ndani ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, ndio maana nikasema kwamba Mhe. Waziri aandae timu yake, kwa ajili kwenye maeneo kuchukua maneno ya vijijini yakakusanywa na matokeo yake kupatikana neno moja la kutumia, kama vile kutoka sehemu moja kwenda nyengine na kuweza kuunganisha na baadaye anapokuja mgeni basi neno lile tunalipata kwa urahisi.

Nikiondoka hapa niende kwenye Idara ya Televisheni. Kwa kweli idara hii ni muhimu sana, tena naamini watendaji wanafanyakazi ipasavyo, licha ya kutoa burudani lakini kazi wanaifanya, isipokuwa kidogo nimekuwa na wasi wasi.

Sehemu ya malengo aliyojipangia mwaka 2010 Mhe. Waziri likiwemo lile la utaratibu wa mwenendo mzima kuleta matangazo katika Uchaguzi Mkuu na kuvipa vyama vya siasa haki sawa. Sasa wasi wasi wangu jambo lolote linapoanzia tunaambiwa mwanzo mgumu, lakini kama mwanzo mgumu basi ndipo unapotia wasi wasi.

Mhe. Mwenyekiti, wakati tunaendelea na michakato hii ya chaguzi ninaimani vyombo vya habari vilikuwa vinatoa habari kwa Chama cha Wananchi CUF, wenzetu wakifikia wakati vitatoa maelezo kama vilivyotoa kwetu.

Ushauri wangu katika hili ukifika ule wakati wa uchaguzi wenyewe, basi licha ya kupewa nafasi vyama na wagombea urais, lakini vyema hata Wabunge, Wawakilishi pamoja na Madiwani wawe wanapewa nafasi japo dakika chache kuweza kujieleza. Kwa kweli vile ndivyo vipimo pamoja na vigezo, kuweza kujua mwanasiasa gani amepevuka kisiasa na yupi anapaswa kupewa taaluma zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kinachonipa wasi wasi chengine kwenye idara hii, kuhusu malengo aliyojipangia fedha za maendeleo sikuziona. Mhe. Waziri amesema, ili idara iweze kufanyakazi zake anaziombea fedha kadhaa kwa ajili ya kazi za kawaida, lakini za kimaendeleo hamna na miradi tayari imeshapangwa.

Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwenye ile miradi aliyojipangia, ili aweze kutekeleza majukumu yake vizuri fedha za maendeleo atazitoa wapi au kwa sababu mgombea urais atapata wafadhili mapema, kwa ajili ya kuleta fedha kwenye mfuko wake, basi ninataka nielewe hilo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri kwa sababu anaelekea kwenye mfumo mpya tena ninaimani si mkaidi basi ataweza kunipa ufafanuzi wa kuridhisha na nitaendelea kumuunga mkono.

Kwa hivyo, naomba kumalizia na kuunga mkono hoja *(Makofi).*

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Asha Moh'd Hilal: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kupata nafasi kwa ajili ya kuichangia bajeti hii. Kwanza sina budi kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote. Vile vile namuombea dua Mwenyezi Mungu amjaalie ampe analolitaka ambalo lina kheri na yeye.

Nianzie mchango wangu kwenye ukurasa wa 12 kuhusu mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha mwaka 2005 hadi 2010. Kwa kweli sinabudi kumpongeza kwa kutekeleza haya yafuatayo:-

1. Imejenga jengo jipya,
2. Imetayarisha Sera,
3. Imeweka mitambo mipya ya *Digital MW kilowatts* 50,
4. Imeanzisha mafunzo,
5. Imetengeneza Uwanja wa Amani pamoja na
6. Kuanzisha *Academy*.

Mhe. Mwenyekiti, ule uwanja tumeambiwa hauchezewi gwaride. Sijui Mhe. Waziri sehemu gani ambazo ametupangia kufanya shughuli zetu za kitaifa hususan likiwemo hilo gwaride. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja kufanya majumuisho anifahamishe sehemu gani tutatumia kwa ajili ya shughuli zetu hizo.

Idara ya Habari Maelezo ukurasa wa 23. Pamoja na majukumu yake ya kutoa elimu ya UKIMWI mijini na vijijini, mazingira, ajira kwa watoto. Lakini

napenda kumuomba kitu kimoja Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwenye ajira za watoto hasa katika maeneo ya pwani ambazo wanaingia wageni, kwa sababu kule wanaingia wageni tofauti na watoto wanaacha kwenda skuli na vyuoni kwa ajili ya kushughulikia zile ajira. Kutokana na watoto wanapata dola moja au tano, basi anaona skuli pamoja na chuo vimepitwa na wakati.

Kwa hivyo, hivi *cinema* nadhani tujikite zaidi kwenye sehemu za vijiji ambavyo vinavyoingia wageni sana, kwa sababu huku ndiko kunakotokea matatizo haya, pamoja na suala la wimbi la maradhi ya UKIMWI.

Kutokana na kuwepo kwa wageni na wananchi wa vijijini wengi wanakimbia hii elimu, yaani hawana elimu ya kutosha, kwa hiyo wimbi hili la maradhi ya UKIMWI watoto wengi wanakumbwa na wimbi hili, kwa sababu wao wanaona wageni wameingia. Kwa mfano, akipata dola zake 10 au 15 akirudi tayari ameshachukua maradhi.

Kwa maana hiyo, kuna haja ya kujikita sana kutangaza suala zima la kuvamia hawa wageni, ambao wanatoka sehemu moja na kuja sehemu nyengine, kwa ajili ya masuala ya biashara za hoteli.

Mhe. Mwenyekiti, huu uingiaji wa wageni ndio unaopoteza mila, silka pamoja na desturi zetu, kwa sababu wao wanaingia na lugha zao na lugha yetu inaanza kubadilika. Kwa mfano, baadhi ya maneno yanaingia bila ya kutarajia, kwa vile ni lahaja na unaweza kutumia popote, basi tunaingiza maneno ya ajabu ndio tunaona lugha yetu inavyoharibika.

Kwa hivyo, wageni hawa wanatufaa, lakini wanatuchafulia desturi, silka na hata mila zetu. Vile vile tukiangalia mavazi tunaona kwamba watoto wetu wanaiga kutoka nchi nyengine, kwa vile wale watu hawana elimu na wengi wanatoroka kutokana na kufuata maslahi na ugumu pamoja na ukali wa maisha. Hivyo, wanakuwa wanaiga mambo tofauti, kwa ajili ya kufanikiwa malengo yao pamoja na chakula chao cha kila siku.

Idara ya Upigaji Chapa ukurasa wa 26. Mhe. Mwenyekiti, hapa namshauri Mhe. Waziri kwa makusudi mazima tufanye kama wenzetu magazeti yetu kwanza hali yake si nzuri, yaani sura yake ni mbaya *black and white*. Kwa kweli wenzetu wanaweka rangi haidhuru lizidi bei lile gazeti, lakini liwe katika hali nzuri, kwa sababu ile rangi peke yake inamvuto wa aina yake.

Vile vile Sauti ya Tanzania Zanzibar (STZ) nayo naipongeza kupitia vipindi vyake mbali mbali hasa Kipindi cha Mawio nakipenda sana. Kutokana na vichwa vyake vya habari, yaani *heading* zao zinakuwa nzuri mtu anaposikia ile

heading, basi atasikiliza japo kuwa ile *issue* yenyewe tofauti kidogo, lakini ile *heading* peke yake inakuwa na mvuto.

Kwa hivyo, tukijitahidi nafikiri haya magazeti tukaweka *heading* nzuri ambazo ni za kuvutia, mtu anapoiona ile *heading* tu basi anavutika, sasa anapovutika lazima atanunua gazeti hata kama zile habari zake si nzuri sana, lakini zile *heading* nzuri zenye mvuto.

Mhe. Mwenyekiti, pia tuwahamasishe waandishi haidhuru wamekuja na habari zao, sio kila mwandishi atamudu uwezo, kwa sababu kila mtu Mwenyezi Mungu amempa kipaji chake cha uwezo wa kuandika na kufahamu. Hivyo, tuwafanyie marekebisho *at least* zile *heading* zao ziwe kwenye hali nzuri, ili haya magazeti yawe na mvuto.

Ukurasa wa 32 kuhusu Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa za Maonesho. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri hizi sanaa mbona tunazo nyingi, lakini tukikaa hivi sanaa hizi hazikui na wala hatupati wasanii wazuri na siku zote tutakuwa hivi tulivyo.

Sasa sanaa tutazipata wapi. Kwa kweli maskuli yanazo sanaa za kutosha za kukuza wasanii wetu wa kila fani. Wasanii wengi tunawapata kutoka kwenye maskuli. Kwa hiyo, sisi kila mwaka tunakuwa na Mashindano ya Elimu Bila ya Malipo na mle tunapata wasanii wazuri tena wa kila fani kama ni utamaduni unapata mle, ikiwa ngoma, kwaya, mashairi na mengineyo.

Kwa kuwa mle mnakuwa na mashindano na kunapatikana washindi. Sasa nadhani wale washindi tunawachukua na kuwaonesha kwenye televisheni kupitia vipindi vyetu. Mhe. Mwenyekiti, watoto wanakuwa na tabia na choyo cha kuigana, wakati watakapowaona wenzao wamewekwa vizuri na halafu wanapata zawadi, basi wanavutika.

Kutokana na mashindano hayo tukiwaendeleza basi mle tunaweza kupata wasanii wazuri tu, televisheni yetu itakuwa na mvuto wa kutizamwa na watu wengi pamoja na watoto, watakaa kwa ajili ya kuangalia vipindi vya televisheni yetu na kujionena hali halisi ya mambo wanayofanya wenzao.

Mhe. Mwenyekiti, kusoma kuna njia mbali mbali kama vile kusoma kwa kuiga, yaani kuona mtu anafanya jambo fulani kwa nadharia na vitendo, basi watoto wetu wanaweza kuiga kutokana na kuona hali halisi na kuweza kuingia kwenye mashindano na kupata wasanii wazuri kupitia njia hii.

Ukurasa wa 34 Baraza la Kiswahili. Mhe. Mwenyekiti, naomba kumwambia Mhe. Waziri kwamba lugha yetu ya Kiswahili imeingiliwa na kuchafuliwa.

Katika lugha kuna lahaja na lugha sanifu, lakini hivi sasa imekuwa tafrani hatujui lahaja wala lugha sanifu au ya kigeni.

Mhe. Mwenyekiti, zamani kulikuwa na vipindi vingi vinavyozungumzia lugha sanifu na wakati tunapotaka neno geni kuliingiza kwenye lugha yetu, nafikiri kulikuwa na majadiliano maalum, ili lile neno kulitohoa, yaani ni kutoa neno la kigeni kuingiza kwenye lugha yetu na kukubaliana kwa masharti yetu ambayo yapo tumeyaweka na lile neno linatumiwa bila ya matatizo.

Lakini hivi sasa tumekuwa na mambo ya ajabu sana, kama vile kuna neno kuboresha na mengineyo. Kwa hivyo, ndio ninaposema kwamba lugha imevamiwa tena inaharibiwa.

Nadhani ni vyema tukarejesha ule mfumo wetu wa kuonesha kwenye vyombo vya habari. Kwa mfano, tunapotaka kuingiza neno ambalo ni jipya na hatuna neno la kuingiza lazima tuliingize vile vile, basi tutumie utaratibu ambao upo tokea zamani tulitohowe lile neno na watu wote wajue kwamba neno lile limeingizwa rasmi kwenye lugha yetu. Nafikiri tutafanikiwa kama mwanzo kwenda vizuri kutumia lugha yetu sanifu.

Mhe. Mwenyekiti, naipongeza idara hii kwa kufanya utafiti wa hizi simulizi asili ambazo zilizounganisha lugha za Afrika ya Mashariki na Kati. Kwa kweli hii ni nzuri tena inapendeza na inafaa tuiendeleze, kwa sababu hii tunapata kujua historia ya nchi yako pamoja na ya mwenzio.

Vile vile inatangaza biashara ya utalii, yaani zile mali ambazo tunafanya sisi na wao, kwa vile lugha ni chombo cha mawasiliano, basi tutakuwa tunawasiliana kutoka lugha moja na nyengine.

Pamoja na hilo, inatangaza lugha yetu na kuzidi kuenea na kupanuka, pia inaleta muungano wa hizi nchi za Kiafrika na mwisho tunaweza kujua tamaduni zetu na kuweka rasilimali hizi tamaduni zisipotee. Kwa mfano, sisi tunaweza kujua utamaduni wetu na wenzetu watajua utamaduni wetu.

Kwa hivyo, napenda kumpongeza Mhe. Waziri na hizi ni faida ambazo nimeziona wakati nilipopita hiki kitabu ambazo tunaweza kuzipata.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho natoa wito kwa Waheshimiwa Wajumbe sote tuiendeleza michezo kwenye majimbo yetu, kwa sababu michezo mimi nilikuwa mwalimu na mwalimu anapenda kusema lakini sitochukua muda wako mwingi Mhe. Mwenyekiti.

Michezo kwanza inakuza kiu ya mtoto anakuwa yuko *active* na akili yake inakuwa *bright* na inafanyakazi vizuri kwa vile anacheza michezo, michezo vile vile inafurahisha, michezo inaleta mawasiliano kati ya watoto na watoto na upendo wanakuwa wanafahamiana vizuri wale watoto na wanakuwa wanapendana. Halafu michezo vile vile inatuletea kutembea kutoka sehemu moja kwenda nyengine pia ni kusoma na kusoma sio kukaa tu lakini kutembea pia ni nzuri kwa mtoto anapata kubadilisha mawazo, asiwe na mawazo ya sehemu moja sasa inakuwa ndio ile kukuza akili yake.

Sasa michezo ni kitu kimoja ambacho kina thamani haidhuru kina hasara, halafu michezo inakuweka karibu sana na watoto na jamii yako, kwa sababu hata kukutangaza wale watoto kama kwenye jimbo watakutangaza vizuri ukishughulikia kwenye michezo yao kwa hivyo pale unapata mambo chungu nzima, ukilinganisha na hiki kipindi chetu cha uchaguzi watoto kama unao karibu basi umeshavuka, ni lazima tuwashughulikie watoto. Wanajenga uhusiano mzuri, imani mtoto anakua akili yake na wewe mwenyewe unajua kwamba sasa hivi mtoto wako yuko kwenye michezo kipindi cha michezo basi unakuweko salama na inakuwa huna wasi wasi.

Mhe. Mwenyekiti kwa kumalizia mimi kwa niaba ya wananchi wa jimbo la magogoni naiunga mkono hotuba hii mia juu ya mia. Ahsante sana.

Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa na mimi nafasi ya kuweza kuchangia lakini nakushukuru kwa ushawishi wako na ndio maana nimekuja kukaa hapa nafasi yako, kwa kutaka nichangie usikie sauti yangu.

Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na watendaji wote wa Wizara hii kwa kweli wizara imepata mafanikio makubwa na imebadilika hasa, nataka niwapongeze kwa ujenzi wa kiwanja cha Aman. Kiwanja cha Aman Mhe. Mwenyekiti pale VIP ule mjengo wa zamani ulikuwa ukikaa mpira ukenda huku inabidi na wewe uende huku kwa sababu pana nguzo kati kati, mpira ukienda upande mwengine upishe ile nguzo ili uone vizuri. Lakini *technology* iliyotumika hivi sasa nguzo ziko nyuma huko na kule mbele hakuna nguzo hata moja unakaa raha mustarehe.

Lakini pia na hili eneo la VIP limeengezwa limekuwa kubwa zaidi uwanja umekuwa mzuri unapendeza lakini kama walivyozungumza wenzangu wizara ingeangalia na ile hoteli iliyokuweko nyuma, maana ukija kwenye uwanja unajiona kama uko Afrika ya Kusini kwenye *World Cup* lakini ukienda kule hoteli unajiona tayari uko ng'ambo. Sasa nafikiri namjua Mhe. Waziri uhodari

wake angefanya maarifa basi na ile hoteli ikatengenezwa ili mtu akiingia pale ajione hasa kwamba kweli kaingia pahali panapovutia.

Mhe. Mwenyekiti jengine Mhe. Waziri usione nakusakama lakini ndio ukweli ulivyo sisi tunaoendesha timu tunaumia sana, Mhe. Ali Abdalla alizungumza hapa hasara anazopata kwa timu yake, mchezo ni hasara tunakubali lakini hasara zinakuwa kubwa wenzetu hasa Dar es Salaam sasa hivi kwenye mchezo wa *football* wao wanaanza kupata faida, ndio maana utaona kila siku watu wanagombana wanataka uongozi lakini kwetu huku bado mpira ni ridhaa, lakini tayari tunaingia huko kwa sababu sasa hivi mchezaji ukitaka kumsajili anakwambia mimi sina kazi utanilipa shilingi ngapi, inabidi umpangie mshahara japo shilingi elfu thalathini japo kwa mwezi. Sasa kama unasajili watu thalathini huna njia ya kupata fedha ni matatizo.

Lakini matatizo zaidi yanakuja kwa vifaa viatu, jezi, mchezaji kaumia umhurumie lakini bado wapenzi tu ndio wanaoumia nashukuru *ZFA* kwa kushirikiana na *ZANTEL* walipata udhamini lakini nasikia sasa hivi wanataka kujitoa kwenye udhamini wa ligi kuu, sasa kilio cha wanamichezo cha siku zote ni kile kile wanachokisema kwa nini bado hatutaki udhamini wa Serengeti, Kilimanjaro au TBL. Mhe. Mwenyekiti takwimu zinaonyesha kwamba jiji la Dar es Salaam ndio namba moja kwa kunywa pombe, wakifuatiwa na Arusha na Zanzibar ikiwa ya tatu, sasa hawa wanaouza pombe wanafanya faida kubwa sana kwetu sisi lakini hatufaidiki na faida yao wanaofaidika wenzetu wa Serengeti Boys, Ligi kuu Bara sisi huku bado tunasema hatutaki udhamini wa pombe, matokeo yake ndio tunarudi nyuma.

Mhe. Mwenyekiti nilisema hapa udhamini wa pombe sio kwamba watu wanakunywa pombe uwanjani inakuwa mtu yule anayecheza kavaa fulana tu imeandikwa TBL au imeandikwa Serengeti au Kilimanjaro au kitu chengine chochote lakini sisi bado tunang'ang'ania, juzi Mhe. Mwenyekiti nilipita Mau nimekuta timu ya vijana wamevaa jezi imeandikwa *back beer* wanatoka kucheza, sasa nikawa najiuliza imekuwaje hii *back beer* haijawadhamini lakini wamegaiwa fulana tu kwa umasikini na wao wamezivaa wamekwenda kucheza. Nafikiri Mhe. Waziri aliangalie tena suala hili kama hawa wauza pombe wanapata faida hapa kwetu kwa nini na sisi tusipate pesa hizo tukazitumia.

Mhe. Mwenyekiti katika kitabu hiki ukurasa wa kumi na sita nimeona Baraza la Taifa la Michezo wamewekewa ruzuku ya Shilingi milioni mia moja, nilikuwa naitizama michezo kwa ujumla . *Football, Netball, Volley ball, Basket ball*, JUDO, Karate, Baskeli, Riadha, Karata, Bao, Pools, Darts na michezo mingine chungu nzima iliyokuwepo lakini ruzuku ni shilingi milioni mia moja.

Kuitoa Karume Boys kuipeleka Misri kwa mazoezi ya mwezi mmoja hazitoshi, sasa hao ruzuku yenyewe ni shilingi milioni mia moja kweli hiyo michezo itaendelea ndio hapo utapoona kwenye michezo tunabakia nyuma, hatwendi mbele bado tunawategemea tu akina Mhe. Haji Faki Shaali achangie tunakwenda namna hiyo. Hivi sasa timu zetu za *Cope Coca cola* zipo huko nasikia kwamba timu ya Mkoa wa Mjini na timu ya Mkoa wa Kusini Pemba zinafanya vizuri na zimeingia fainali, sasa tujiandaeni basi wakija hapa angalau tuwachangie changie tuwatie moyo maana kwenda huko kila mmoja kenda kivyake vyake.

Lakini pia tarehe 15 timu zetu za riadha za Mikoa zinataka kwenda Dar es Salaam na mashindano yapo Dar es Salaam na mikoa yote inatakiwa ishiriki, kila mkoa unatakiwa kupeleka wanariadha wasiopungua 30, 35 au 40 kila mmoja na uwezo wake, kama Mikoa hatuna bajeti ya kuwasafirisha inabidi tuhangaike. Nataka nichukue nafasi hii kumshukuru sana Naibu Waziri Mhe. Mahamoud Thabit Kombo kwa timu yangu ya Mkoa wa Kusini kwa sababu ndio kaweza kutusaidia hiyo laki moja, ahsante sana Mheshimiwa lakini pia tunahangaika ili timu tuweze kuisafirisha.

Mhe. Waziri wa Fedha na Uchumi kwa bahati mbaya hayupo kama angekuwepo basi katika bajeti zetu za Mikoa angalau kungelikuwa na pesa kidogo za kuhudumia hizi timu zetu wakati wa kuzisafirisha, bila ya hivyo mashaka yanakuwa makubwa mtaji wetu mkubwa tunategemea Wabunge na Wawakilishi nao sasa hivi wamo katika mchakato humpati mtu, ukimkamata mtu anakwambia aa hebu ngojea kwanza inakuwa mashaka kweli kusafirisha timu.

Sasa ningeliiomba Wizara ya Fedha na Uchumi basi itusaidie kutuwekea angalau vijisenti kidogo katika bajeti za Mikoa, ili zikitokea timu hizi za Kimkoa kusafirishwa tuwe na pesa za kuweza kusafirisha.

Mhe. Mwenyekiti jengine nizungumzie Baraza la Sanaa hapa nisikitike kidogo, Baraza la Sanaa wana utaratibu wa kutoa vibali vya kupiga disko kwa mwaka mmoja, miwili mpaka mitatu wakishatoa madisko yanakuwa mengi, hasara tunayoipata sisi nazungumzia Mkoa wa Kusini kwa upigaji wa disko ni mbili. Moja wanaokwenda kwenye disko ni vijana wadogo na vijana wale ndio tunaotaka wasome wawe wataalam wa kesho, sasa hawa wanaotoa vibali wao wanaangalia pesa tu hawaangalii athari ambazo zinapatikana, athari tunazopata watoto hawaendi skuli wanakimbia wanakwenda kwenye disko matokeo yake ukija kwenye mtihani mwaka juzi 33 *persent* tuliopasisha. Sababu disko.

Lakini sio hasara hiyo tu siku linalopigwa disko linaaza ijumaa, Jumamosi na Jumapili siku hiyo mihogo itaibiwa, nazi zitaibiwa, kuku wanaibiwa, mbuzi

wanaibiwa, Ng'ombe wanaibiwa kwa sababu watu wanatafuta pesa za kwenda kwenye disko, sasa watu wa sanaa hebu waangalie hizi athari tunazopata na hizo faida wanazopata. Tulikaa kikao kimoja tukazungumza wanasema sisi tumeambiwa tuchangie mfuko mkuu wa serikali milioni nne, lakini hasara inayopatikana ni zaidi ya milioni nne kuna maeneo likipigwa disko hao watalii wanaokuja wanahama hawataki kelele. Sasa kwa nini watoe vibali mwaka mzima.

Ninachoomba hapa Mhe. Waziri anisaidie na sio mimi tu mikoa yote huu utoaji wa vibali basi tushauriwe ili tumwambia hapa toa hapa usitoe, hivi sasa hivi kuzungurusha magunia yale kukapigwa disko imekuwa ndio utamaduni mkubwa, sasa hii kwa kweli inatuharibia vijana wetu hawasomi lakini na wizi unakuwa mkubwa. Sasa ningeliomba sana katika kutoa hivyo vibali waangalie vizuri.

Lakini kuna jengine nalo limekuwa kero kubwa na hao ndio wanatakiwa hili walishughulikie hawalishughulikii, hivi sasa huko mashamba uoneshaji wa video kwa kuingiza watu kwa shilingi mia tano mia tano umekuwa mkubwa sana, mtoto anatakiwa asubuhi aende skuli lakini mpaka saa saba au nane yuko kwenye video anaangalia, pengine video zenyewe anazoangalia za matusi matupu lakini hili wamelifumbia macho hawalitizami, sisi tunajaribu kukamata kule lakini sheria wanazo wao. Sasa kama tutapata mashirikiano na wao vizuri badala ya kukaa ofisini wakashuka angalau tukawapa nafasi vijana wetu wakasoma na sio mpaka saa saba au nane wanashughulika wako kwenye video hili kwa kweli linaleta matatizo.

La mwisho nataka nichukue nafasi hii kumpongeza sana Katibu Mkuu Ndugu Omar Dadi Shajak na Naibu wake Said Shabaani Mhe. Mwenyekiti weye ni *board member* wa maktaba yetu, wakati tunataka kufungua maktaba ukuta wa *Eacrotanal* ulikuwa mchafu sana tukasema itatutia dosari katika sherehe yetu lakini nilikwenda nikazungumza nao, wakachukua juhudi kwa siku mbili wakaupiga rangi mpaka leo pale pahali panang'ara nawapongeza sana kwa kazi ile nzuri lakini pia na ukuta wao umekuwa mzuri.

Nimalizie kwa kumwambia Mhe. Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo ni mtu anayejiamini, jasiri kenda kachukua fomu anataka Urais wa Zanzibar, ninachoweza kumuombea mie Mwenyezi Mungu ampe kila lenye kheri na yeye na amuepushe kila lenye shari na yeye.

Mhe. Mwenyekiti naunga mkono hotuba hii mia kwa mia niliyoyazungumza Mhe. Waziri nataka ayafanyie kazi asinijibu. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na naomba nichangie machache tu kuhusu bajeti hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo ambayo imewasilishwa na Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo, Mhe. Sheh Alhaj Ali Juma Shamhuna.

Kwanza nimpongeze kwa kuitikia wito wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu kasema niombeni na kazi ya kutoa ni yake yeye, sasa yeye kuchukua fomu ya kugombea nafasi ya juu kabisa katika uongozi wa nchi kama hii basi ni jumla ya kuitikia wito huo, na mimi naungana na Mkuu wa Mkoa wa Kusini kwa ile dua ambayo amemalizia nami naomba dua ile ile, ampe kila lenye kheri na yeye na sisi mungu atupe. Lakini lolote ambalo lina dalili tu ya shari akuepushe nalo tena umbali wa mbingu na ardhi.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo ambayo tunaijadili lazima nikubali kwamba kuna mabadiliko makubwa ukianzia mwaka 1992 mpaka 2005 basi sisi kule kwenye Chama chetu cha CUF hizi sauti mbili hizi tulikuwa hatuziiti kama mnavyoziita nyie tulikuwa tunasema ni TV kitangi kwa maana TVZ na Redio Kidude hayo ndio majina yetu lakini ni kwa sababu ya waliyokuwa wanayafanya.

Sasa nikiri kabisa kwamba kuna mabadiliko makuwa labda kwa sababu ya hao waliokuwepo na zaidi Katibu Mkuu kwa sababu ni msomi mkubwa ana PhD na amesoma akiwa katika Wizara hiyo hiyo hakwenda Marekani miaka sita kukaa huyu, ndio maana ukakuta kitabu hiki kuna watu wafanyakazi watendaji mbali mbali zaidi ya tisini nimeona humu katika kuendeleza wafanyakazi wa Idara hii au Wizara hii mia moja, Kuna mtu anafanya PhD Uingereza ya uandishi wa habari, kuna shahada ya kwanza, shahada ya pili cheti, stashahada, *O level* sasa na mimi hapa nasema kwa sababu sasa Wizara hii inaonekana wataalam watakuwa wengi zaidi kuliko walivyokuwa. Naomba uchaguzi unaokuja kuanzia hii kura ya maoni basi ionekane kweli haya tunayosema kwamba mmebadilika ukereketwa hamjauwacha *hundred percent* kwasababu hauachiki sawa sawa na umasikini tutaupunguza tu lakini hauondoki.

Lakini msije mkafurtu mipaka hichi ni chombo chetu sote na ni vizuri sote turidhike kwamba kinatupa huduma tunazozihitaji, kwa hivyo nafasi unayogombea hiyo uliyoomba kwa Mwenyezi Mungu basi inahitaji haya tunayozungumza, uwe kiongozi wa watu, kama kuna mtu anasema hukubaliki au huuziki kwamba, *improve wrong* wewe unakubalika sana. Na sio kwamba unauzika lakini tayari umeshanunuliwa.

Naibu Waziri wa Wizara hii mimi nasema nae anahitaji pongezi za peke yake ni kijana *vigilant, vibrant, dynamic* shehe Thabit ni *very young* mimi nafikiri

katika Baraza hili basi *the first five young* yeye yumo ingawa kama hakufanya mazoezi baada ya miaka mitatu anaweza kuonekana kizee kuliko sisi. Kwa hivyo napongeza hizi juhudi za Wizara hii katika kuwaendeleza wafanyakazi wake ziendelee bila ya wasomi, bila ya watu wenye elimu hakuna chochote unachoweza kukiendeleza. Habari ni mdomo wa nchi na hasa zikitoka katika chombo rasmi cha serikali.

Mhe. Mwenyekiti pamoja na kwamba tunaendeleza watu lakini tusisahau kwamba suala sio kulima tu tunatakiwa kuvuna na tufaidi matunda ya kilimo chetu. Inatusikitisha sana kwamba tunapompika mtu ama kwa kumpa fursa mbali mbali ili apee aisaidie lakini hatimae unakuta mtu yule ametutoka sio kufa lakini amekwenda pahali pengine, kweli kuna uhuru, haki za binaadam kuna mwahali mwengine majani ni makavu mwengine kijani. Kwa hivyo mtu atapenda kwenye kijani kuna ndugu yetu Marine Hassan TBC1 sasa hivi kama utasikia kuna kipindi anatangaza yeye basi *channel* nyengine watu wanafunga wanamsubiri wamsikilize yule alikuwepo hapa. Lakini hatuvuni sasa hivi tunampongeza kwa *achievement* yeye angekuweko hapa basi ni TVZ ambayo watu wangekuwa wanaikimbilia kuisikiliza bila ya shaka hakuamka tu asubuhi akaenda kule kuna vivutio vizuri zaidi kuliko vya hapa.

Hapa kuna raha zake na karaha zake sitaki niseme kahama hapa kwa sababu gani lakini mimi nasisitiza tu kwamba kama tunalima basi tuvune na tule mavuno yetu. Juzi tulikuwa tunamsifia bwana mmoja anaitwa Alhaj Juma Mmanga yeye naona sina hakika kama ameajiriwa na Wizara hii au vipi, lakini najua tu ni *correspondent* wa Sauti ya Tanzania Zanzibar lakini aliyeko Dar es Salaam huyu kijana wakati wa Ijitmai mimi niliwahi kumuona hapa Fuoni na Pemba. Kuna wakati mmoja niliwahi kusoma gazeti alipokwenda Makka na mahujaji alitengeneza mkanda wa CD na mkanda huo nilisoma kwenye gazeti alimkabidhi mama Salma Kikwete.

Sasa hivi ni vitu ambavyo sijui ana uwezo gani au elimu gani lakini najua huyu kijana ana uwezo mkubwa, na sasa hivi zile habari mlikuwa mnasikiliza hapa lakini siku hizi Redio Zanzibar wana kipindi cha magazeti na wengi sana tunasikiliza kipindi kile namna ndugu yetu huyu Juma Mmanga anavyojua kusanifu yale mambo, jamani utangazaji ni fani na kuna watangazaji wengine vile wanavyotangaza tu madoi doi basi mtu anaona raha hata kama habari zenyewe pengine sio za muhimu, lakini anaona raha sasa ile raha ndio inamfanya mtu asikilize zile habari. Huyu kijana kama hamjamuajiri tunashauri aajiriwe na kama mmeshamuajiri basi muendelezeni naamini atakuwa na uzalendo wa hali ya juu na kuna siku pengine ni mkereketwa najua, maana yake saa nyengine unaposema unajua lakini ukereketwa sio shani nikisema ukereketwa nakusudia wa CCM, ukereketwa si shani muhimu ni kufanya kazi zake vizuri nafikiri atasaidia sana huyu.

Muendelezeni na niliwahi kusikia na wala sikusikia mbali kwamba BBC wanamdowea Shirika la Utangazaji la Uingereza huyu Juma Mmanga sasa pengine amepata umaarufu kwa haya anayoyafanya. Lakini na nyie mlipompa fursa kwenye redio yetu Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mhe. Katibu Mkuu na watendaji wanasikia huyu kijana sasa hivi ni wakati wa kumkumbatia ili na sisi redio yetu tuone hasa tuna watu wazuri wenye sifa kabla BBC hawajamchukua.

Mhe. Mwenyekiti nakuja kwenye sanaa kuna filamu moja inaitwa *film industry* Wamarekani huoni mji mambo yake ni hayo tu, India mambo haya ya filamu wakati mmoja yalikuwa yanachangia mpaka 50% ya uchumi wa India, sasa hivi Mhe. Mwenyekiti Nigeria *is coming up very first.* Hizi *movie* ukienda Darajani pale zimejaa na Tanzania Bara naona nyoka keshafika, sasa hivi kuna watu kama Kanumba mtu anakwambia kabisa nataka mchezo alioigiza Kanumba. Sasa hivi bara wanasafirisha hizi CD kupeleka Kenya na nchi nyengine za Afrika na hata Ulaya.

Sisi hapa tunaangalia filamu za Kifaransa kwani sisi wafaransa na wao sasa hivi wameendelea zaidi kwa sababu zile filamu mna maandishi ya kiingereza kwa hivyo wanaojua kiingereza pamoja na kwamba ni filamu ya Kiswahili anafahamu kinafanyika nini.

Mhe. Mwenyekiti, tusisahau hawa Wabara wameiga kutoka kwetu. Kuna filamu moja hapa kama mtakumbuka ya Marehemu Dokta Ayubu sijui kama bado ipo ile. Kila mtu alikuwa mchezo wa marehemu Dokta Ayubu anauangalia na nina hakika mimi kuna watunzi wakubwa sana hapa wa michezo, kwa nini watu wajifundishe kwetu halafu sisi tuwe wa mwisho. Hii ni *industry* nyengine ambayo inaweza ikatoa uajiri. Kuna mama bongo fleva nao ni usanii.

Mimi nina vijana wangu basi wameshachoka kuchimba mawe kikundi cha watu watatu wakanambia bwana sisi tunaona mambo yanavyokwenda hivi tumeanzisha bongo fleva. Lakini ile pesa ya kwenda studio kurikodi laki saba, nikamwambia miye sina, fanyeni changeni angalau 60% zilizobakia nitakusaidieni miye.

Mimi nashauri kama kuna vijana hawa na tatizo ni kurikodi maana yake huwezi ukaimba uko porini ikawa unajulikana, unatakiwa urikodiwe kwenye studio uanze kuuza 1, 2, 3, 4 mpaka muwe maarufu. Ni wakati wa Wizara ya Habari kuwakaribisha vikundi kama hivi tena kwa gharama nafuu mno. Kwa sababu wakisha kukuwa hawa wazuri kwa kuwaendesha nyie wenyewe watafungua

studio zao. Bara kuna studio nyingi tu na wamezifungua kwa sababu wamekuwa na uwezo hawa wasanii wa kufanya hayo mambo.

Nashauri kwanza *film industry* inawezekana, kanda ile ya marehemu Dokta Ayubu itolewe kwenye CD iuzwe wanaweza kuuza hata Idara ya Habari, wakapata fani lakini vile vile inakumbusha kwamba kumbe na sisi tunaweza na hasa ukiwawezesha zaidi ndio wanaweza zaidi. Hili nilikuwa nashauri sana.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ali Abdalla hapa alikuwa anaeleza mchezo wa mpira ulivyokuwa ghali mno kiasi ambacho unafanya kukua kwa mpira. Yale yale aliyoyasema yeye yameripotiwa na kuungwa mkono na Gavana wa Kusini . Jamani mpira sasa hivi ni ajira, lakini mbali ya ajira kwa kweli ni starehe. Wakisikia timu yao wanakwenda mahala fulani wanatoa mpaka nauli vijana wao waende, timu ikifungwa kijiji chote kinahuzunika.

Nashauri kwamba ZFA gharama zetu zimekuwa nyingi, zimekuwa kubwa kumsajili mchezaji laki moja. Timu zenyewe za shamba huo uwanja wao wameshindwa kuutengeneza, mawe matupu, lakini haya tu twende, wengine wanacheza miguu chini. Lakini ndio hao hao wanaokuwa ma-*star* wakaja mjini wakanunuliwa. Tunashauri sana *policy* hii ya gharama ambazo zina *discourage* mchezo wa mpira mzipunguze na ushuru wa vifaa vya michezo. Amesema hapa Mhe. Ali Abdalla mtumba wa kiatu cha kuchezea mpira shilingi 30,000/.

Mimi naamini kabisa kama ushuru utapungua sana kwa vifaa vya michezo, jezi, viatu basi watu hawatanunua ghali hivyo. Na hata kama watanunua hakuna atakayenunua mtumba ghali wakati kiatu kipya kipo dukani tena bei rahisi.

Enzi za Gavana wa Mjini Magharibi alipokuwa mkuu wa duka la vifaa vya Michezo Zanzibar ilikuwa katika raha kubwa. Utake nini usikipate. Mimi sisemi mfungue vifaa vya michezo kwa sababu ni biasha ra huru, hamtoweza serikali, hamtaweza kushindana na hao. Lakini mimi nashauri kabisa msi-*control* bei lakini naamini kwamba ushuru ukipungua *competition* itakuwa kubwa kwa hivyo kila mtu atanunua mahali ambapo anaweza kununua. Hakuna mfanyabiashara atakayeweka bei ambayo vitu vyake havitonunuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, sasaa hiyo hiyo ya michezo wakati mmoja kuna mtu alinihadithia kuna hawa (*comedians*) wachekeshaji na hawa nao ni vivutio, ni starehe katika TV. Ni kipindi ambacho kama mtakitengeneza vizuri mtatafuta wale *comedians* wapo *natural* hawa hawakuenda shule popote. Kuna mmoja alinambia kwamba kuna mchekeshaji mmoja namjua kwa jina lakini simtaji aliomba kazi magereza lakini katika mambo hayo hayo ya utamaduni. Wakati wa kufanyiwa usaili maana walikuwa wengi yeye kidogo ana mapengo na

kakaa hivi kuchekesha chekesha tu maana yake hujui kama anacheka au analia ndio alivyo maumbile yake. Sasa akaulizwa wewe bwana unataka kuomba kazi hii mbona unaonekana una mapengo, meno yamekaa upande, basi pale pale hakufikiri akasema kwani huko tunakwenda kutafunana?

Sasa hivi vitu wewe ukivisikia tu huku nyie mnacheka hapa, kuna wachekeshaji wengine *natural*. Profesa Gogo yuko kule kwetu Kangagani, vitimbi vyake yule ukivirikodi hasa ukavitoa kimoja kimoja hivi mnaweza mkacheka mpaka mbavu zikakuuma. Sasa vitu kama hivi ni ajira vyote vinahitajika katika Wizara hii, watafuteni hawa waheshimiwa. Hawa ni vivutio katika TV zetu na radio zetu hawa watachangamsha watu wasikilize angalau hivi vichekesho na kwenye vichekesho hapo hapo mnatia na matangazo ya biashara Zantel,Voda na ndivyo vyombo hivi vya habari vinapotengeneza fedha. Fedha zinatengenezwa kwa matangazo ya biashara zaidi. Ili mtu asikilize tangazo hili unalitia pale mahali ambapo yeye amevutiwa kuangalia. Watafuteni hawa wapo wengi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna watu kama wataiga sauti ya Mwalimu Nyerere marehemu huko nyuma kama humjui unasema kwamba Nyerere kafufuka. Kuna watu walikilia mlio wa nguruwe wa paka lakini hao huoneshwa puu yamekwisha. Mshamba wa Mungu kaletwa hapa keshapewa Sh. 20,000/- keshalia milio mpaka roho inamtoka anakwenda zake Nungwi au Fukuchani sijui anakaa, ndio keshasahauliwa huyo. Ndiyo, yeye unafikiri alichukua muda gani kufanya *rehearsal* ya mambo yale. Hawa ni watu wa kuendelezwa, mna wa- *promote*.

Mhe. Mwenyekiti, Wazungu vitu kama hivi hawana wanachukuliwa hapa kama anavyochukuliwa bi kidude mara Ujerumani, Spain na hawa mkiwachukua chukua hivyo hivyo jamani leo kuna mtu hapa analia kama mbwa, analia kama paka, ana sauti ya Mwalimu Nyeree, ana sauti ya Marehemu Karume, basi na hata hapa inafanyika.

Mhe. Mwenyekiti la mwisho juzi katika bajeti ya Vikosi suala la *garden* iliyopo hapa mbele yetu liliulizwa, Waziri hakuwa muwazi, akatugeuza tu kama chapati, hatukuondoka na jibu. Haya mambo ya mapembea yaliyokuwepo hapa mwenyewe nani. Ipo chini ya Manispaa. Hii haipo chini ya Manispaa, Manispaa hata siku moja hajawahi kuweka mabofu pale, hawana hasa vifaa vile. Serikali nzima hawana wachilia mbali Manispaa, tuambie ukweli kuhusu hili hapa.

Garden hii kama walivyosema wenzangu, hii *garden Is another school* ukenda pale sasa hivi vikundi vya watoto wanaofanya *revision* huko maskulini hakuna nafasi eti darasa moja lina wanafunzi 100. Kwa hivyo hapa ni mahali kwa skuli

karibu zote za mjini *catchments* hii ni kubwa. Mimi nasema hata kama mmekodisha kwa kiasi gani manufaa tunayopata, watoto wetu kwa kwenda kufanya *revision* pale ni makubwa zaidi kuliko hicho mnachokipata. Michenzani imependekezwa upande huu ambapo kuwa yamewekwa yale ma-*calvat* sasa hivi hayapo pako safi kabisa pasafishwe yule bwana kama anataka ku- *invest* aka *invest* pale, pale ni kati kati zaidi kuliko hapa. Uwanja utengenezwe vizuri watoto wetu wapewe nafasi ya kufanya shughuli zao za kusoma pale.

Mwisho kabisa naunga mkono hotuba ya Shekh Rais mtarajiwa, rafikiyangu mkubwa Waziri Ali Juma Shamhuna.

Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi: Mhe. Mwenyekiti awali ya yote mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya na kuhudhuria kikao hichi cha Baraza ili kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nianze kama walivyoanza wenzangu, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa jimbo langu la Chaani kwanza tunaunga mkono hotuba hii ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2010/2011 ya Mhe. Naibu Waziri na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote kwa ujumla kwa jinsi ambavyo wanajituma katika kufanya kazi hizi katika Wizara hii na idara zake mbali mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, mmi nianze na Idara ya Michezo, mimi sijawahi kufanya kazi katika Wizara hii lakini ni mmoja katika wabia wa wizara hii kwa sababu ni mwana michezo na ni mtu ambaye nimefanya kazi katika sehemu za michezo kwa muda mrefu kwa hivyo nina uzoefu na mambo haya ya michezo. Nataka niwapongeze sana wenzetu kwa kazi nzuri wanayoifanya lakini bado nataka nitoe maombi yangu kwao kupitia kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, tunapozungumzia mambo ya michezo basi tuelewe kwamba jambo la kwanza katika hata hizo sheria za michezo tunazungumzia neno kiwanja hiyo ndiyo sheria namba moja hata kama kwenye *foot ball* basi ni uwanja wenyewe wa mpira. Kuna tatizo ambalo tunalipata katika maeneo yetu mbali mbali Unguja na Pemba. Kwanza kama tunavyojua ardhi yetu ni chache lakini pia viwanja hivi vya michezo vimekuwa vikiingiliwa aidha kwa kujengwa au pengine kwa kufanya mambo ambayo pengine hayastahiki, aidha kufunga ng'ombe katika viwanja.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyoelewa kwamba ng'ombe yale mavi yake akinyia pale kwenye kiwanja basi wale wadudu wanaozaliwa wachezaji kama wanacheza pale akianguka akichubuka basi tayari tetnasi anapata.Ukipata tetnasi katika umri mkubwa kwa mujibu wa maelezo ya daktari anasema ukizidi miaka 15 mbele kuna 2% mtu akapona. Sasa kwa kweli ni jambo la kutizamwa na kuona kwamba halifanyiki hivyo, vyenginevyo kuwa na adhabu kali kwa wale ambao watakuwa wanafanya hivyo kwa sababu kufanya hivyo ni kuidhalilisha michezo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ningependa kulizungumza mbali na kudhibiti viwanja lakini pia kuweza kuwa na viwanja ambavyo vinamilikiwa na ngazi hizi za wilaya kwa mfano kama mpira wa miguu basi angalau kila Wilaya wawe na kiwanja chao chenyewe kinamilikiwa na ZFA ngazi ya Wilaya.

Mhe. Mwenyekiti nasema hivyo kwa sababu tunapokuwa na viwanja hivi basi itakuwa ni nafuu tunatizama wakati mwengine tunakwenda kuchukua viwanja vya vilabu kunakuwa kuna matatizo yanajitokeza. Mimi nilipokuwa Katibu wa ZFA kule Kaskazini tuliwahi kufanya *project right up* kwa ajili ya kupata kiwanja, lakini nasikitika sana kwamba tulishindwa kupata hizo fedha na zilikuwa si nyingi wakati huo lakini kutokana na uwezo wetu mdogo tulishidwa kuzipata na tayari tumeshapewa eneo na tukakaguzwa kwamba hapa mnaweza mkafanya shughuli hizo, lakini tukashidwa kulipa.

Kwa hivyo naomba sana kwa kipindi hichi ambacho tunaendelea nacho zifanywe juhudi za makusudi kwa kushirikiana na uongozi wa michezo katika ngazi ya Wilaya. Hasa kwa sababu tukizingatia kwamba maafisa wa michezo ya Wilaya nao ni watu wasimamizi wakuu wa karibu na mambo haya basi wawe ni kiungo kati ya Wilaya na Taifa kuona kwamba vinapatikana viwanja hivi katika mawilaya yetu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nalitaka kulichangia katika Wizara hii wenzangu wamezungumzia hapa suala la ugumu au pengine gharama kubwa zinazotozwa na ZFA katika usajili na mambo mengine. Mimi nafikiri eneo moja tunaweza tukalitizama hili lililozungumza usajili wa wachezaji hizi ZFA wanaweza wakapunguza zile gharama. Pengine kwenye *lessens card* hapa wanaweza wakapunguza kwa sababu zile wanatoa wenyewe. Lakini suala la uhamisho mfano kwa wachezaji mimi naomba viwango vilivyokuwepoa hapa vibakie. Na kwa nini nasema vibakie.

Mhe. Mwenyekiti, tunachotaka kuona katika kuendeleza michezo kulinda wachezaji katika vilabu vyao. Kama hatutokuwa na kiwango kikubwa kitakachomzuia mchezaji kubakia katika klabu yake, lakini pia kulinda muda

wa mchezaji kubakia katika klabu ambayo amejiunga kwa kipindi ambacho kimewekwa basi pia tunaweza tukapata tatizo. Kwa sababu pengine itakuwa klabu inamuendeleza mchezaji lakini baada ya kwisha kumuendeleza tayari anafaa sasa hivi kutumika, inakuja klabu kumchukua katika mambo ambayo yatarudisha nyuma ile klabu husika. Iwapo kutakuwa na kiwango kikubwa cha uhamisho wa wachezaji maana yake ni kusema kwamba tutadhibiti ule uondokaji ovyo wa kiholela.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nilitaka nilizungumze ili kuvisaidia vilabu katika huu usajili kuna hili eneo la mchezaji ambaye anatoka katika klabu ile ile na wanapotaka kusajiliwa kwenda katika klabu ile ya *division,* wale wanalazimika kuhamishwa na huyu anaitwa ni mchezaji huru ambaye hamilikiwi na klabu. Lakini mchezaji yule tayari amecheza pale tokea haelewi kupiga mpira mpaka ameelewa yupo katika klabu ile pale kuna haja ya kuangalia vizuri kuona kwamba tunaweza kuvisaidia vilabu vipi ili kuondosha zile gharama ambazo hazina ulazima sana katika kumuhamisha yule kupitia mchezaji huru kutoka ZFA na klabu husika ambayo inamsajili.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ningetaka kulingumza nataka na mimi nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote pamoja na Naibu Waziri kwa kusimamia vizuri suala la ujenzi wa uwanja wa Amani. Uwanja wa Amani kwa kweli ulikuwa umeshapoteza haiba yake ilikuwa kama unakwenda mpira pale kulikuwa kuna matatizo vyoo mashaka na pahala ambapo panapokusanyika watu wengi lazima wengine watapata tatizo la haja kwa kweli ilikuwa halipendezi. Lakini leo hii sote tumekuwa mashahidi kuona kiwanja kile sasa kimekuwa ni kiwanja cha kisasa zaidi. Kwa hivyo tunahitaji tuone kwamba kiwanja kile kinalindwa kwa nguvu zote.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nilikuwa nataka kuliomba, niiombe serikali kwa ujumla kupitia wizara hii kwamba kuna haja hivi sasa ya makusudi kuwa na kiwanja mbadala ambacho kitatumika zaidi kwa mambo ya sherehe za serikali badala ya kiwanja cha Amani kama wanavyofanya wenzetu Tanzania Bara. Tanzania Bara pale Temeke wana viwanja viwili, kile kimoja cha zamani ndio wanafanya sherehe lakini kile ambacho kimejengwa kwa gharama kubwa zaidi hawatumii kwa mambo ya sherehe kwa misingi hiyo kwamba kile kitakuwa kiwanja bora zaidi kwa masuala mengine. Naomba hilo litiliwe maanani ili kuona kiwanja chetu hichi kinadumu kwa muda mrefu.

Mhe. Mwenyekiti, magwaride yale katika ule mwendo wa kwata sote tunaelewa yanaharibu sana tatan na mambo mengine. Lakini hata pale kiwanjani unaweza ukakikuta kiwanja kinakuwa kipara kwa sababu wakati mwengine wanakuwa muda mrefu wanakuwepo pale kwenye gwaride. Mimi ningeomba sana kwamba tukajitahidi kuwa na kiwanja chengine mbadala

ambacho kitatumika zaidi na mambo haya ili mambo yote yafanyike, sherehe zile tuzifanye kwa sababu tuna haki ya kuzifanya lakini pia na shuhuli zetu hizi za michezo ziende vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nilitaka kulizungumza kwa upande wa riadha. Nataka nikipongeze sana chama cha riadha kinafanya juhudi. Vile vile ningeomba kwamba tutizame kila uwezekano kuona kwamba timu yetu ya riadha hasa ya Zanzibar inaangaliwa kwa jicho la huruma kuona kwamba wanapata walimu wa riadha lakini pia waweze kusaidiwa mambo mbali mbali ya vifaa na mambo mengine kwa sababu ili uweze kukimbia unahitaji kuwa na viatu vya kukimbilia na mambo mengine. Niombe basi wenzetu ambao wana uwezo wasaidie hili ili kuona kwamba suala la michezo linapata kipaumbele kwa nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ningependa nilipongeze vile vile niwapongeze wenzetu wa TBC kwa upande wa Zanzibar TVZ kwa kutuwezesha kuangalia kombe la dunia katika muono mzuri. Tunafurahi sana kuona kwamba tunaliona kombe la dunia kama vile ambavyo Wizara zetu ambavyo vimejitahidi yaani Wizara yetu ya Habari ya Zanzibar na kwa upande wa Tanzania Bara.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye mchezo wa *netball*, hapa nataka nipongeze Chama cha Mpira wa *Netball* Zanzibar kinafanya vizuri na ushahidi wake kwamba timu zetu zinaposhiriki katika mashindano haya huwa zinafanya vizuri hii ni dalili nzuri.

Pia nije kwenye mpira wa miguu yenyewe niupongeze uongozi wetu wa michezo pamoja na Wizara kwa ujumla. Kwanza kwa kuelewa hasa timu yetu ya taifa imekuwa pamoja muda mrefu na bado haivunjwi mara kwa mara. Hichi ni kitu kinaifanya timu yetu ya taifa iwe bora zaidi tofauti na timu ya Taifa ya Tanzania kwamba kila siku au kila Jumamosi kocha anabadilisha wachezaji pamoja na kwamba wanachukia baadhi ya viongozi lakini hawana budi waridhie.

,Mhe. Mwenyekiti, ili timu iwe nzuri basi ni lazima inahitaji kuwa pamoja kwa muda mrefu. Hili tunaliona kwa wenzetu wa Misri timu yao ile ya Taifa iko pale kwa muda mrefu inafanya vizuri na pia ina kocha mzalendo lakini bado inaendelea kufanya vizuri. Pamoja ya kwamba kwa bahati mbaya imetolewa na Algeria kuingia katika zile timu ambazo zimekwenda katika *Would Cup* kule South Africa lakini bado timu yao ni nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, suala la gharama kwa vifaa vya michezo, na mimi nataka nilizungumzie hili kwamba kuna haja ya makusudi kwa Wizara kuiomba

Wizara husika Wizara ya Fedha na Uchumi kuangalia uwezekano wa kupunguza gharama hizi za kuondosha au kupunguza ushuru ili wenzetu hawa wanapopunguziwa ushuru basi na sisi tutapata nafuu ya kununua hivo vifaa.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana hawa wafanyabiashara unajua wafanyabiashara ni watu wajanja wanaweza wakalamikia jambo kwamba ushuru mkubwa lakini hapa pale serikali inapunguza ushuru ama kuondoa kabisa lakini bado wao hawafanyi vile ambavyo wamesema. Sasa ningeomba kidogo wawe waungwana pale ambapo tutapata nafasi ya kupunguza ushuru basi na wao vile vile waweze kupunguza bei ili wenzetu hawa wanamichezo waweze kupata unafuu katika kuzinunua vifaa mbali mbali vya michezo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kulizungumza ni katika suala la utamaduni. Kama walivyosema waimbaji kwamba utamaduni ni mambo ya asili ningeomba sana michezo mbali mbali ya ngoma na mambo mengine ya asili ya Zanzibar basi yaendelezwe ili kuendeleza utamaduni wetu. Pia ningeomba kwa eneo hili Wizara kwa makusudi aidha iangalie kama itatoa kwenye mfuko wake wa serikali lakini au kama itatafuta njia nyengine kuweza kuwasaidia maafisa wa michezo na maafisa ya utamaduni katika ngazi za Wilaya na Mikoa. Hapa nataka niwaseme kwamba wasaidiwe kupata usafiri kwa sababu hawa wanafanya kazi katika ngazi ya wilaya wanatakiwa waende kila sehemu kila kijiji kila shehia kuona kwamba michezo inaimarika katika maeneo hayo. Ama mambo ya mila na utamaduni yanaimarika katika maeneo hayo.

Pia wenzetu hawa inapotokea sherehe mbali mbali hizi za kitaifa kwa mfano mwenge wa uhuru unatembea nchi nzima kwa mfano Mkoa wa Kaskazini, Mkoa wa Mjini, Mkoa wa Kusini na Mikoa mengine ya Pemba washiriki mle. Lakini ushiriki wao unakuwa mgumu kidogo kutokana kuwa hawana vyombo vya usafiri. Mimi ningeomba sana na hili nimekuwa nikizungumza kila bajeti ya wizara hii wapatiwe basi mkopo wa vyombo alau vespa kuona kwamba na wao wanapewa usafiri wa kuweza kwenda sehemu mbali mbali kuona vile shughuli wanazozifanya wanazifanya kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka kulizungumza katika Wizara hii ya Habari, Utamaduni na Michezo niwapongeze waandishi wetu wa habari wale ambao wapo kwenye taasisi za serikali lakini na wale wanaojitegemea. Vyombo vile vile vya Radio na Televisheni wanajitahidi kutupatia habari na vipindi vyao vimekuwa vizuri na vya kuvutia pamoja na kasoro ambazo zipo ndogo ndogo kama walivyosema wenzangu. Pale penye kasoro ningeomba tu parekebishwe lakini wanatupatia habari vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa katika kuchangia katika Wizara hii niseme basi wale watangazaji wa mawio nafikiri wanakuwa si watu ambao wameajiriwa moja kwa moja na Wizara ya Mhe. Waziri wa Habari. Hasa nikizingatia kule Kaskazini tunae mtangazaji anaitwa Bakari Sauti Mirando, huyu ni mtu ambaye anapenda sana fani hii ya habari, na anafanya kazi nzuri ya michezo na kazi nyengine ambazo sio za michezo lakini zile za kutoa habari. Amekuwa akifatilia kwa karibu sana na hata ukimualika basi ni mtu ambaye anayekuja na kuweza kufanikisha zile habari ambazo zinapatikana pale na ni mwepesi wa kutoa habari.

Sasa mimi basi niseme Mhe. Waziri tuangalie uwezekano pale ambapo kutakuwa na nafasi basi aajiriwe huyu kupitia Wizara yake. Kwa sababu mbali ya kuwa yeye mwenyewe atakuwa na ajira lakini vile vile ataisaidia sana Wizara kupitia michezo kwa sababu na yeye mwenyewe ni mwana michezo kwa hivyo tukimuajiri huyu tutakuwa tumeweza kuongeza nguvu katika suala zima la uandishi wa habari ambao wana taaluma ya mambo ya michezo hata kama pengine hajasomea sana lakini pengine tukimchukua na kwa sababu wizara yako ina utaratibu mzuri wa kuwasomesha wafanyakazi wake basi nafikiri tukimpeleka chuoni muda si mrefu tunaweza kuwa na mwana habari mzuri kama vile wale kina Kipevu lakini sasa hivi naona tayari wameshaajiriwa. Kwa hivyo, naomba sana na huyu ambaye anafanya kazi muda mrefu aonekane kama ni mtu ambaye amejituma na kujitolea na kama nilivyosema kwamba wale ambao wanajitolea katika ngazi mbali mbali basi baadae nao wachukuliwe katika ajira za kudumu ili waweze kuendesha maisha na pia watasaidia taifa kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia nasema kwamba mimi naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri hasa na mimi nikiwa mdau katika mambo haya ya wizara hii kwa asilimia mia moja kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chaani. Ahsante sana.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi kutia baraka katika hotuba ya Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo katika hotuba yake ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2010-2011.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kunipa uzima mimi mwenyewe pia kumpa uwezo Mhe. Waziri kuwasilisha hotuba yake ya kazi za mwaka uliopita. Pia niongeze kumpongeza kwa hatua yake ya ujasiri na ya kizalendo ya kuchukua fomu ya kuwania kiti cha Urais wa Zanzibar. Nampongeza sana kwa hilo Mwenyezi Mungu atamsaidia. Amin.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri anao uwezo huo na anazo sifa za kuwa Rais wa Zanzibar, kwanza ameshatimia umri unaotakiwa, pia ana uwezo wa kusoma na kuandika, elimu yake imeshapindukia kiwango kinachotakiwa, ni Mzanzibari wa kuzaliwa, yeye ni mtu mchapakazi, muumini wa amani na utulivu pamoja na mshikamano kwa umoja wa kitaifa. Kwa hivyo, kwa nini watu wa CCM wasituletee kiongozi wetu huyu akawa Rais wetu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mwenyezi Mungu kiongozi wetu wa Chama cha Mapinduzi awepe ilhamu ya kumuona mwenzetu huyu kuwa anafaa na tuletewe ili tumpigie kura za ndiyo siku itakayofika. Pia nikuombe wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu unayo kura hiyo umuone mwenzetu huyu katika mchakato wetu tumpigie kura za ndio.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hapa sio pahala pake mambo hayo.

Mhe. Haji Mkema Haji: Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo sasa nije katika hotuba hii. Mimi nawapongeza waliomsaidia Mhe. Waziri wa kwanza Naibu wake, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi pamoja na wafanyakazi wote. Wizara hii imetusaidia sana na kweli imefika malengo na mapungufu mengi ambayo tuliyatoa mwaka uliopita hivi sasa yamerekebishika. Kwa hivyo, hakuna sababu kwa nini nisiipongeze wizara hii. Pongezi zangu za mwanzo nizitowe wazi wazi kwa kuwataja hasa waandishi wetu wa habari kwani wamefanya kazi nzuri, wale wa serikali pamoja na vile vyombo vya watu binafsi.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba taarifa zao zimeimarika hazina chumvi nyingi wala hazina majungu, kwa muda wote utapenda kununua gazeti kuweza kusoma taarifa ambazo zilizokuwa ni sahihi. Mhe. Mwenyekiti, hili mwaka uliopita tulilipigia kelele kwa hiyo Mhe. Waziri juu ya hili amefanikiwa sana kuwarekebisha waandishi wetu wa habari kutupatia taarifa hizi sahihi za ndani pamoja na za nje ambazo tunapata kwenye magazeti na vyombo vyetu vya habari.

Mhe. Mwenyekiti, pia niwapongeze watangazaji wetu wa Sauti ya Tanzania Zanzibar, Televisheni Zanzibar kwa kweli na wao wameimarika wamerekishwa hivi sasa wanasoma taarifa zao vizuri sana. Kwa hivyo, na eneo hilo Mhe. Mwenyekiti, nimpe pongezi sana Mhe. Waziri amefikia lengo la wawakilishi ambalo mwaka jana tulililalamikia sana.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi nije kwenye mambo yetu ya utamaduni. Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Utamaduni imepangwa kuwemo katika shughuli za kiserikali ili kuhifadhi utamaduni wetu usipotee, ukuzwe na udumishe ndani ya jamii yetu. Lakini bado ni kwamba kuna mapungufu, mapungufu yaliyomo

Maafisa wa Utamaduni ambao tumepangiwa vijijini hawana utaalamu wa kutosha ili kumudu shughuli zao. Nafasi zile zimekuwa kama ajira tu anapewa Afisa Utamaduni basi kazi kubwa kule angojee kuna harusi wapi atoe cheti cha rusha roho, taradhia, maumbwa ni hilo tu lakini namna ya kwenda akafika vijijini kuelimisha namna gani kila shehia tuweze kutunza utamaduni uwezo huo hawana.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nafikiri iko haja sasa hivi Maafisa wetu wa Utamaduni ambao tumewaweka katika Wilaya wawe na taaluma maalum ili lengo lililokusudiwa liweze kufikiwa. Mhe. Mwenyekiti, pia katika shughuli za kila siku tamaduni zetu maadili yanaporomoka ukiachia jando na unyago kila siku hapa ni mambo ya harusi, harusi zetu za Mzanzibari nazo zimegeuka sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nafahamu siku za harusi, harusi nyingi zilikuwa zinafanywa wakati wa mchana, asubuhi lakini hivi sasa harusi nyingi zinafanywa asubuhi mapema au usiku sana. Kwa hivyo, hata ule utamaduni wa vyakula vinavyoandaliwa kwa harusi nao umebadilika, maana ilikuwa mchana watu wanapiga ubwabwa, lakini sasa hivi unakwenda asubuhi au jioni unapata futari. Mhe. Mwenyekiti, hapa utamaduni umebadilika hata vile vyakula ambavyo vinataka kuandaliwa katika shughuli vimebadilika kiutamaduni.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kulikuwa na uji wa kungu, uji wa mlezi, uji wa mzazi. Uji sio kama uji ule wa kunywa lakini ilikuwa ni matayarisho ya vyakula unaweza kuwemo uji wenyewe, chai, shurba, juisi pamoja na maandazi, mikate na vyakula vyenginevyo. Sasa hivi utamaduni huo umeondoka sasa hivi kuna chai tu, leo chai ya mzazi, chai ya mashoga tena mambo hayo yanaweza kuendelea hata miezi mitatu huo uharusi umeshakwisha lakini utasikia kuna chai tu. Mhe. Mwenyekiti, maadili yanaporomoka sana.

Mhe. Mwenyekiti, pia kwenye harusi zetu ilikuwa hawa Maafisa wetu wa Utamaduni waanze kuliweka hili yale mambo ya uji yawepo. Uji wa mzazi unakuwa anatoa yeye bure, uji ule wa kungwi ulikuwa unalipiwa ada kidogo kuna na nyimbo zake huwa zinaimbwa. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi hata zile nyimbo za harusi haziwezi kuimbwa kwa sababu ile shughuli yenyewe haipo.

Mhe. Mwenyekiti, hata biharusi mapambo yake ya Mzanzibari yako maalum, sasa hivi anavishwa veli anakwenda kuoneshwa kwenye *hole*, utamaduni huo haupo. Bi harusi siku hizi akishaolewa tu anatiwa mgongoni anachukuliwa lakini zamani ilikuwa anawekwa wiki nzima anapigwa supu wiki moja, anapikiwa vyakula vizuri vizuri na katika wiki hiyo mlikuwa na mambo ambayo yanahitajiwa. Mhe. Mwenyekiti, jambo la kwanza ni kufahamiana na familia, bwana harusi anabakia kwa mke ili aweze kumjua Shangazi yake, watani wake, ndugu zake kwa wiki nzima inakuwa ameshawaelewa. Hivi sasa

biharusi siku hiyo hiyo anachukuliwa siku utakayokwenda kwa ndugu yake au akija ndugu yake mwanamme unaanza ugomvi, huyu nani tena.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba yamekosekana yale maadili kwa sababu siku zile saba ingelikuwa zimewekwa ingekuwa ameshamjua huyu ni mtoto wa mjomba wangu, huyu ni mtani wangu au huyu mjomba wangu. Lakini hayo yote mheshimiwa yote yameporomoka Mhe. Waziri mambo haya nawaomba Maafisa wetu wa utamaduni wayajue na wayaelimishe ili yasipotee hapa kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, hata ngoma zetu za kwenye harusi zetu pia zimebadilika, ni kwamba ngoma zetu za asili tunazo tuna Msihaba sehemu za Kidoti, tuna Maumbwa Ukongoroni, tuna Taradhia Ubango, kuna Jungu Bovu Kizimkazi na mwengineyo. Mhe. Mwenyekiti, hizo zote kabisa zimepotea hata wale wenyewe wana vijiji sasa hivi hawajui.

Mhe. Mwenyekiti, tunajua sasa hivi tuna kitengo maalum cha kuhifadhi utamaduni lakini ngoma zile huwa wanachezewa wageni tu ziko huku huku mjini katika kitengo maalum bado hakijateremka vijijini akajua asili yake Ndanda inachezwa Donge basi angalau baadhi ya siku wende kule Donge wakaweza kucheza ili wakawaambia kwamba hii ndio ngoma yetu wakatafutwa vijana wakafundishwa, hii Taradhia nyinyi watu wa Ubago ndio ngoma yenu, hili Bomu watu wa Michezani hii ndio ngoma yenu. Lakini sasa hivi Mheshimiwa ngoma hizo zipo lakini ziko kwenye kitengo maalum mpaka aje mgeni anakuja kupigiwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba eneo hili tulirekebishe itakuwa ni sehemu ya kuweza kudumisha utamaduni wetu na tutaweza kuboresha. Nimeona nizungumzie haya kidogo tu Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nije kwenye michezo Mhe. Waziri amefanya kazi kubwa sana katika eneo hili, tumeona timu zetu za *netball* kama zilivyozungumzwa hapa na Mhe. Mzee Ali Ussi zinafanya vizuri, riadha, mpira wa miguu kazi ni nzuri sana. Lakini pili jitihada za kutafuta wadau kutusaidia Kiwanja cha Amani najua kumepatikana kazi kubwa sana, hii inatokana na umahiri wa Mhe. Waziri na wasaidizi wake. Kwa hivyo, tunamshukuru sana kwa jitihada hizi sasa hivi tuna kiwanja cha kisasa kwa mchezo wetu wa mpira timu yoyote ya kimataifa inaweza kuja kucheza pale bila ya matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, zaidi ya hapo nimpongeze Mhe Waziri leo asubuhi nimesikia kwenye taarifa ya habari tumepata Kocha mzungu wa miaka mitano. Mhe. Mwenyekiti, nampa hongera Mhe. Waziri maana yake huwezi kufanikiwa bila ya kuwa na mwalimu, atasaidiana na walimu wazalendo ili kuimarisha

mchezo wetu wa mpira, na tunaona desturi ya kuwa na mwalimu hasa wa kigeni. Mhe. Mwenyekiti, tunao walimu wazalendo lakini hufika mahala wenyewe wachezaji kwa wachezaji wakaweza kushirikiana na mgeni kuweza kufanya jambo kwa kustahiwa kwake na tukaweza kufaulu.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, jambo hili nalipongeza sana, lakini jitihada za Mhe. Waziri kuhamasisha vijana *under* 20 hili mbona limenikuna sana kwa sababu wachezaji wazuri hasa wanapatikana kwenye umri huu na Mhe .Waziri siku zote katika hotuba zake na anapokwenda kuzungumza na vijana eneo hili ndilo analolitilia mkazo. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru uendelee kwa sababu hata hao kina Pele hawakuchukuliwa katika daraja kuu walionekana tu katika umri mdogo wanacheza mpira ndio baadae wakawa watu mashuhuri katika ulimwengu huu wa soka. Mhe. Waziri naomba uzi kwenye mchezo wa mpira uwe ndio huo huo.

Mhe. Mwenyekiti, maendeleo yaliyopatikana kwenye vyombo vyetu vya habari juu ya mitambo ile ya AM nayo lazima ipewe pongezi. Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana tulikuwa na maneno mengi hapa lakini pia jitihada hizo za kuletwa mitambo hii ni moja katika kurekebisha vyombo vyetu hivi ili wananchi waweze kupata huduma hii ya habari kwa ufanisi zaidi. Mhe. Mwenyekiti, mimi namshukuru sana pamoja na watendaji wake na wataalamu wake.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba tu mitambo tumeshapata, vifaa tumeshapata hiyo ni sehemu moja, lakini wale wataalamu wa kuvitumia vyombo hivi nao tuwatizame. Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa kwenye Kamati ya Ustawi wa Jamii miaka miwili iliyopita hali ya wataalamu wetu mafundi wa mitambo hali yao ilikuwa mbaya sana. Kwa hivyo, Mheshimiwa juu ya eneo hili nalo mitambo na vifaa ni sehemu ya kwanza lakini na wale watalamu wenyewe nao kama hatukuwaangalia ndio mmoja mmoja hivi kama alivyozungumza ndugu yetu Marin Hassan na wengineo wataanza kututoka wende kwenye vyombo vyengine na sasa hivi imeshakuwa hii ni biashara kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuanzia leo soko huria nchi zote za Afrika ya Mashariki kwa hivyo biashara hii inakubalika moto humu kwa sababu ukishatangaza kwa Kiswahili inafahamika na watangazaji wa Zanzibar Kiswahili chao ni kizuri. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, tutahadhari ili tuwaenzi watangazaji wetu pamoja na waandishi wa habari wa Zanzibar wenye lugha laini, maneno fasaha wasije wakachukuliwa na vyombo vya habari kuanzia leo maana yake kipenga kimeshaingia biashara huria.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Koani mimi naiunga mkono hotuba ya Mhe. Waziri na fedha ambazo ameziomba kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2010-2011 ningewaomba wajumbe

waheshimiwa wenzangu tusipige buti tuziunge mkono na tuziidhinishe ili aweze kufanya shughuli zake. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuunga mkono mia juu ya mia.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa fursa na mimi kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo. Mhe. Mwenyekiti, kama wenzangu waliotangulia na mimi nampongeza swahiba wangu kwa kutekeleza wajibu wake wa demokrasia na ni haki yake na yeye kuchukua fomu ya Urais wa Zanzibar, namuomba Mwenyezi Mungu *inshaallah* amjaalie ampe lile ambalo kuwa amekusudia.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa shukurani na kumtakia kheri swahiba wetu sasa naomba nimpongeze kwa kufanikisha jengo la Uwanja wa Amaan na huo *alhamdulilah* sasa hivi tuna uwanja wa kujivunia, *inshaallah* Mwenyezi Mungu amuwezesha na ule wa Gombani aushughulikie uwe kama ule wa Amaan.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitazungumza na kutoa shukurani kwa redio jamii iliyokuwepo Micheweni.

Mhe. Mwenyekiti, Redio Jamii iliyoko Micheweni imefanya kazi kama ilivyokusudiwa au zaidi ya ilivyokusudiwa, lakini hapa nina masikitiko kidogo naomba nitoe masikitiko yangu.

Mhe. Mwenyekiti, wakati lilipomaliza jengo lile la Redio Jamii wakati linataka kufunguliwa mimi kama mwakilishi wa Jimbo la Micheweni nilishirikishwa kikamilifu na nashukuru nilishiriki swahiba wangu ni shahidi, nilishiriki kikamilifu ufunguzi wa jengo lile. Lakini kabla ya kufungua niliwekwa pamoja na wenzangu tukafanya kikao cha pamoja kwa ajili ya ufunguzi, wakati huo nikaambiwa kama hii Redio Jamii ya Micheweni itakuwa na bodi yake, wajumbe wa bodi miongoni mwao wanaotakiwa ni saba. Mhe. Mwenyekiti, mmoja kati ya wajumbe wa bodi itakuwa ni wewe Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni.

Mhe. Mwenyekiti, Mwenyekiti wa Bodi akiwa ni Mkuu wa Wilaya na Katibu ni Mkurugenzi wa kituo kile cha Redio Jamii na wajumbe wengine ni Mkuu wa Usalama na Mkuu wa Polisi na Sheha na baadhi ya wajumbe wengine. Bahati nzuri nilishirikishwa kikao kile kikamilifu na nikaambiwa wajumbe hawa wa bodi kutakuwa na kamati nyengine mbili. Mhe. Mwenyekiti, katika kamati ambayo kuwa itakuwa inapanga matumizi ya redio jamii kupanga matumizi yake, vipindi itakuwa ni hii bodi ikishirikiana na huyu Mkurugenzi au Mkuu wa hiki kituo ndio itakuwa mnapanga pamoja haya mambo.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la kusikitisha ni kwamba mimi kama mwakilishi wa Jimbo la Micheweni wakati nimeshateuliwa kama ni mjumbe wa bodi, cha kusikitisha baada ya kushirikishwa vikao vile vya ufunguzi mpaka hivi sasa ninavyozungumza sijashirikishwa tena kitu chochote wala sijui lolote linaloendelea. Mhe. Mwenyekiti, hapa tukiwa humu mna tabia ya kusema kama wenzetu wa upande wa pili tukiwashirikisha hamtaki kushiriki, lakini mimi masikitiko yangu ni kwamba pale tunapotaka kushiriki hamtushirikishi. Kwa nini tangu siku hiyo mpaka leo sijaitwa wala sijaulizwa kitu chochote, basi iwe tangu siku tuliyokaa kikao cha ufunguzi mpaka leo hakujakaa kikao chengine.

Mhe. Mwenyekiti, hapa naleta masikitiko yangu kwamba jamani mnapotushirikisha kitu basi tushirikisheni kwa ukweli, msitujaribu au mlikuwa mnanijaribu. Kwa hivyo, mimi naomba msitujaribu twambieni kitu kile ambacho kuwa mnaweza, kitu ambacho kuwa hamuwezi msitwambie.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo sasa naendelea na mchango wangu. Mhe. Mwenyekiti, sasa niingie kwenye michezo, kwa kweli michezo pamoja na utamaduni wetu ukishirikiana na michezo kwa kweli sisi wenyewe mimi nataka kusema Mhe. Waziri kwamba bado hujafanya kazi yakutaka kujua kama michezo au mila ya utamaduni wetu uliomo visiwani ukaujua kikamilifu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu mnakaa mkisema michezo lakini kama mtafuatilia kwa uhakika basi mfuatilie Wilaya kwa Wilaya, jimbo kwa jimbo, shehia, kijiji ili mujue tamaduni zetu na michezo yetu tuliyokuwa tukiendelea nayo ifufuliwe iendelee kwa sababu michezo iliyokuwa ikichezwa katika vijiji vyetu sasa hivi ndio vinakufa. Mhe. Mwenyekiti, zile mila zetu au michezo yetu inapotea moja kwa moja, na hii michezo ndio inayofanana na mila zetu.

Kwa mfano, kama kwetu Micheweni kulikuwa na mchezo wa taro naamini wajumbe mlio wengi hamuujui mchezo huu. Huu ni mchezo mzuri kweli kweli na ulikuwa ukipendwa sana ni mfano wa mchezo wa mpira wa *basket ball* unapigwa kwa mkono. Lakini sasa kwetu ni mfano tu ni vigongo vinakwata vidogo vidogo huu mchezo ulikuwa na nguvu na ulikuwa unapendwa kweli kweli watu walikuwa wanakwenda mechi baina ya vijiji na vijiji, wanatoka wanakwenda mechi.

Mhe. Mwenyekiti, vinakatwa vigongo vidogo halafu unachukua kigongo kikubwa huu unakuwa una sheria zake, unaweka chini huwa kinaruka kile kigongo, kikiruka ndio unaupiga na huko mbele kunakuwa na watu wanasubiri. Mhe. Mwenyekiti, una masharti yake akitimiza mara saba kupiga ikiwa hakijagongwa itakuwa mmefungwa. Huu mchezo ulikuwa na ubilisi mkubwa na ulikuwa una nguvu kweli kweli, sasa hivi mchezo huu umekufa wala haulizwi.

Mhe. Mwenyekiti, mchezo mwengine uliokuwa na nguvu ni ngware kama anavyozungumza Mhe. Omar. Ngware ilikuwa inachezwa Ramadhani mpaka Ramadhani watu wameshashiba uji wao unatoka mji wako unakwenda mji mwengine kwenda kucheza ngware. Pia mchezo huu nao ulikuwa na masharti yake hata mtu kama ameangushwa kwenye ngware ikiwa amekufa basi hakuna kesi wala hakuna chochote, kama utakatwa mkono basi hakuna chochote wewe ndio umekufa kwenye ngware. Hii ni michezo ilikuwa ina nguvu, lakini sasa hivi ndio imekufa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nakuomba hebu jaribu uje Micheweni uwashajihishe watu uwaambie wakuoneshe mchezo wa ngware au uone mchezo wa taro hii ni michezo ambayo mnaweza mkaifanya na ikawa na nguvu katika nchi yetu. Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri kama ni michezo iko mingi iliyokuwepo kwenye nchi sio mpira tu, mchezo wa mpira sasa ndio una nguvu lakini kuna na michezo mengine ilikuwa inataka ifufuliwe kwa sababu ni jumla ya mila zetu za silka zetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine kwenye michezo ni kama wanavyozungumza wenzangu kwa kweli watoto wetu walikuwa wana viwanja ambavyo walikuwa wakijifurahisha siku za sikukuu, lakini viwanja vile vimekufa ni aibu, ni fedheha kukiona kiwanja kama cha Kariakoo watoto ikifika siku za sikukuu hawana kiwanja cha kuchezea. Mhe. Mwenyekiti, bahati nzuri ilikuwa si kujifurahisha tu hata hii wizara ilikuwa inaingiza fedha kwa watoto kwenda katika viwanja hivyo, lakini viwanja hivyo vimekufa.

Kwa hivyo, nakuomba Mhe. Waziri unieleze kuna mpango gani wa kuvifufua vile viwanja na lini vitafufuliwa vile viwanja nakuomba Mhe. Waziri ukija unieleze ili kwa faida ya watu wa Baraza zima waliomo humu na wasikilizaji wetu wapate faida kama kuna mpango wa kuvifufua tena au ndio basi. Mhe. Mwenyekiti, na je, kuna mpango wa kuongeza viwanja vyengine au hakuna kwa sababu hili suala kila siku tunaliuza.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ni kwamba kipindi kilichopita cha bajeti ulitwambia kwamba kuna mpango wa kukuza vipaji vya wachezaji wa mipira na ukatwambia utakwenda vijiji kwa vijiji, jimbo kwa jimbo na maskuli kukuza vipaji vya wachezaji wa mipira ili kupata wachezaji bora.

Je, hatua ile uliyotueleza ilifikia wapi? Tumepata wachezaji wa kukuza hivyo vipaji au tupo pale pale. Naomba na hili ukija Mhe. Waziri unijibu kwa faida ya watu wote.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, niende katika Televisheni Zanzibar. Mhe. Waziri sisi tuna tabia moja,bajeti iliyopita nilisema na leo ninasema tena tuna tabia moja, tabia yetu sisi tunaanza tukisha hatumalizi, na kuanza ukisha usimalize ni sawasawa na kuwa hukufanya. Tujaribuni tukianza tumalize. Sisi

tulianza mwanzo hapa televisheni ya rangi kuliko wenzetu, lakini sasa hivi cha kusikitisha ni kwamba tumepitwa tuko nyuma kabisa.

Ukienda Tanzania Bara *TBC* wameanza juzi kuliko sisi, lakini sasa hivi tunaona choyo *TBC* karibu watu wote wanaipenda Tanzania nzima inapatikana hakuna hata sehemu moja isiyopatikana. Lakini sisi leo Televisheni Zanzibar hapo Pemba haipatikani kwa nini? Wenzetu wanakwenda mbele sisi tunarudi nyuma, kuna kitu gani kinachotudhuru? Naiomba serikali pamoja na wizara iangalie kuna kitu ambacho kinatudhuru. Moja la kulifanyia utafiti ni hilo, tufanyeni utafiti tujue ni kitu gani kinatudhuru, ya kuwa sisi tunaanza lakini hatusogei mbele tunarudi nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu wanaoanza mwisho wanakwenda mbele wanatupita sawa sawa na wale waendaje wa mbio ikawa mtu kapigwa ngwara kaangushwa hapo chini mwenzake akapita. Kwa hivyo, sisi watu wanatupita tunarudi nyuma kwa nini? Nakuomba Mhe. Waziri tufanye utafiti na hili tulione. Leo itakuwaje tumeanza sasa hivi televisheni yetu hapo Pemba hupati. Kuna vipindi vingapi ambavyo vinawaelimisha watu.

Kwa mfano, hivi sasa tunaingia katika Uchaguzi Mkuu karibu, kesho kutwa tuna kura ya maoni na tunaomba Mwenyezi Mungu aipitishe nchi yetu iwe salama, ipite kura ya maoni na Uchaguzi Mkuu kwa salama na amani, kwa maelewano na masikilizano. Lakini katika vipindi vya televisheni kulikuwa kuna kuwaelimisha watu aidha kwa kura ya maoni au uchaguzi mkuu, lakini sasa je wakuelimika wa huku Unguja pekee wa kule Pemba hawaelimiki ndio tumefaidi? Nchi yetu Zanzibar ni visiwa viwili Unguja na Pemba, lakini leo

Mhe. Mwenyekiti: Malizia tena Mheshimiwa.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Sawa Mhe. Mwenyekiti, lakini unajua tena mambo matamu unataka usimalize lakini *Inshaallah* nitajali heshima yako.

Leo Pemba televisheni haionekani nina mengi sijamaliza lakini naheshimu muda wako. Haionekani. Kwa hivyo, Mhe. Waziri hebu fanya jitihada na kule Pemba tuone tupate tuione televisheni yetu tufaidi matunda yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuheshimu kiti chako naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru sana kupata nafasi hii fupi ya kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanza kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa wizara hii kwa shukurani alizozitoa kwa viongozi mbali mbali na watendajio wake na mpaka wizara hii ikajivuta ikafikia hali hii iliyo. Lakini hii ni Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa maana ya habari ni lazima iende na wakati. Chombo cha habari kinaangalia mazingira yanavyokwenda na huwa kinatoa taaluma kwa wananchi.

Katika vitabu vingi vya Waheshimiwa waliopita walikuwa wakitoa taarifa nzuri sna tu, kuhusu historia Zanzibari itakayoweka tarehe 31 Julai, 2010 ya kupiga kura ya maoni. Kwa vile sisi tunakitegemea chombo cha habari kiwajibike kikamilifu katika suala hili kwa kuielekeza jamii kule ambako kuna manufaa na sisi. Kwa masikitiko makubwa nilifikiria humu itaeleza vizuri hata kulivyo katika vitabu vyengine suala hili halikuelezwa wakati ni la kitaifa.

Pili Mhe. Mwenyekiti, wakati hii ni wizara kubwa sana kweli kweli, ni lazima tujue kuwa kufanya kazi kwake ndio namna jamii itakavyokua. Mfano mdogo tu, jana tulikuwa katika usajili wa simu kwa sababu ilikuwa ni tarehe ya mwisho. Lakini vyombo vya habari kusema tu kumeongezwa wiki mbili watu wote wametulia, hii ndio maana ya vyombo vya habari. Kwa hivyo, kwa lile la heri na la shari iwe inatokea kama hivyo. Sasa ushauri wangu kwa Mhe. Waziri ni kuona kuwa chombo hiki kinakwenda kwa wakati katika hali ya haki sawa kwa wote.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, tunapoingia katika Uchaguzi Mkuu unahusu wananchi wote na vyama vyao na kila mgombea kwa maana hiyo kwa sababu kura tunaowahitaji si ya chama ni ya wananchi anayo haki sawasawa na mwenzake. Nimefarajika sana kweli kweli, kuona wananchi wenzangu kutoka CCM namna walivyopokewa nakupewa muda mrefu wa kujieleza kwa kila mgombea, lakini na mimi namsubiri mgombea yeyote atakayetoka huko kachukua fomu katika mtindo huo huo na huko huko, lakini hatukuona shamra shamra yoyote.

Kwa hivyo, wito wangu ni kwamba na sisi lazima tubadilike kwa namna ya wakati unavyokwenda. Mhe. Rais wa Zanzibar kafanya kazi kubwa ya maridhiano na Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi *CUF* tuko pamoja, tunaona Baraza letu linavyokwenda basi na vyombo vyetu vibadilike kuipeleka jamii huko katika umoja.

Jengine nianze na Idara ya Michezo. Kwanza nakubaliana na malengo yote waliyoyaweka kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, isipokuwa kuna kifungu nambari 17(ii) cha ukurasa wa 24 hiki kidogo ningetaka maelezo. Kwa ruhusa yako Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu.

Kifungu Nam.17(ii) kinasema kwamba:

> "Kuelimisha jamii juu ya uhuru wa vyombo vya habari kwa kutumia sheria iliyopo".

Mimi suala langu ni kuwa sheria hii iliyopo ni kama hivi tunavyokwenda kuwa wengine wanapata haki zaidi kuliko wengine, au sheria hii iliyopo ni nzuri lakini hatuitumii vilivyo. Kwa hivyo hii sheria iliyo kwa bahati mbaya siielewi hivyo nataka nipate maelezo.

Kifungu Nam. 17(iv) kinasema:

> "Kusimamia utendaji wa vyombo vya habari katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2010 kwa kutengeneza vipindi na makala maalumu, kuandaa mikutano ya wanasiasa na vyama vya siasa pamoja na kutoa taarifa maalum kwa wananchi na vyombo vyengine vya habari vya ndani na nje ya nchi".

Hii taarifa maalum kwa vyombo vyengine vya habari, kwa sababu najua kila chombo cha habari kina uhuru wake wa kufanya mambo, mazingira wanakuwa wanayakabili pamoja, lakini hii kutoa taarifa maalum ningeliomba mfano wa taarifa hiyo ni upi. Ni ya kutisha au ni ya kujenga?

Halafu ukitizama katika kazi zao wanajikita sana katika kutoa taarifa na kuelimisha jamii katika Uchaguzi Mkuu wa 2010. Kwa nini huu wa Kura ya Maoni haukuingizwa wakati muhimu zaidi utakaoamua serikali itakayopatikana baada ya uchaguzi huo itakuwa vipi, wakati wananchi wana haja ya kujua kinachoendelea.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niingie kwenye Michezo. Mhe. Mwenyekiti, michezo ni kitu muhimu sana, kinamjenga mwanadamu kiakili, kimwili, kisiasa na halafu kinaitangaza taifa katika mataifa mengine. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake kwa kuona kabisa kuwa iko haja ya wanamichezo wetu kukuzwa vipaji vyao na kuweza kushiriki kikamilifu katika siku za mbele. Hata ikabidi kuajiriwa huyu Mwingereza ambaye jina lake silijui vizuri kuanzia mwisho wa mwezi huu kufanya kazi kubwa sana ya kuendeleza michezo hapa Zanzibar.

Lakini pia ninavyojua huyu nasikia ni mwajiri wa *ZFA* na serikali inaye huyu mtaalamu kutoka Misri, basi sijui kazi zao zitakuwa zinakwenda vipi. Kwanza hili nataka nipate maelezo.

Halafu la pili kwenye michezo mipango iliyomo ni mizuri, lakini kuna mambo ya utekelezaji ndio muhimu mpaka kufikia haya malengo yaliyokusudiwa. Michezo takriban yote inahitaji viwanja katika *design* ya mchezo

unaokusudiwa. Niliposoma kitabu hiki nimeona kazi kubwa itakayofanywa ni kushughulika na kuimarishwa kwa michezo ya ndani ya Uwanja wa Amani basi. Lakini viwanja vyengine vyote viliopo Unguja na Pemba vimeachwa. Wakati wanamichezo ni wengi na viwanja vinahitajika na hivyo vilioko vinatumiwa katika hali mbaya sana.

Mhe. Mwenyekiti, nilizungumza sana kuhusu kiwanja chetu cha Mao-tse-tung, ni kiwanja kizuri, kina nafasi kubwa, kikubwa, kingehitaji kuimarishwa. Na kama ni wanamichezo kweli tuliona aibu iliyotufika wakati kiwanja cha Amani kilipokuwa katika matengenezo, pale si mahala pa kucheza timu za kitaifa lakini tulifanya kwa sababu hatuna pahala pengine.

Mimi ushauri wangu kwa wizara ni kwamba hivi sasa umefika wakati kama tunataka kuendeleza michezo kwa hivyo hakuna sababu lazima tuviimarishe viwanja vyetu. Nataka nijue hasa hiki kiwanja cha Mao-tse-tung zaidi ya vile kuwa kinatafutiwa mfadhili sijui nani kukiendeleza, kuna mpango gani wa makusudi kuonesha kuwa hiki kiwanja nacho kimeshughulikiwa ipasavyo wakati nina uhakika kama kinafanya kazi vizuri usiku na mchana itatumika na itakuwa ni njia moja ya kukuza hiyo michezo yetu.

Pili kwa Pemba tuna kiwanja kikubwa tu cha Gombani, *Alhamdulillah* tunashukuru umeme tayari tunasubiri wataalamu ambao hatujui siku watakaofika kuja kufunga hizo taa, lakini ule uwanja ulipojengwa ulikuwa na *plan* yake kubwa. Kwa maelezo ya mdomo ambayo si ya kuamini ilikuwa kabla hatujakabidhiwa rasmi tuliufanyia sherehe moja tena wale waliohusika ikabidi waondoke na wakauacha bila ya kukamilika. Ikiwa hivyo ni kweli, tuliambiwa kulikuwa kuna viwanja vya michezo pale tofauti vitajengwa, hoteli kubwa sana itajengwa na kadhalika, lakini yote yameondoka.

Ule uwanja kwa hadhi utakayokuwanayo kama hizo nyasi bandia zitakuja kweli, Mhe. Waziri ameweka utaratibu gani wa kuona kuwa na kile kiwanja kinaimarika kutokana na hali yake itakayokuwa hapo baadae hasa kwa mpani hiyo ya mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti: Malizia Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, la kumalizia kwa ufupi tu naomba dakika mbili japokuwa ni nyingi, namna ya kukuza vipaji vyetu. Mhe. Mwenyekiti, twende kwenye *football* watoto wetu wanacheza mpira kuanzia daraja la chini kuja juu na huko kuna waamuzi. Lakini tunavyoona hizi *ZFA* za Wilaya zinapopanga waamuzi wao hawapangi waamuzi kwa sababu ya kuendeleza zile timu, wanapanga waamuzi kwa kutafuta riziki tu, ukitoa shilingi elfu tano tu basi japokuwa hujui kitu utashinda.

Kwa maana hiyo, wao wanaturejesha nyuma sana. sasa namuomba Mhe. Waziri kama kweli tuna lengo itolewe taaluma kwa waamuzi na adhabu husika kwa kila tutakapoona kuwa hawa katika kufanya kazi zao ni kuturejesha nyuma na kuwavunjia watu haki zao ambapo sio lengo la wizara. Nashukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Nilikuwa nataka kumwita Mhe. Rashid Seif pale lakini naona simuoni sijui kaenda wapi na Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Waziri Kiongozi amepata dharura kidogo ana kazi. Basi tunaendelea na majadiliano.

TAARIFA

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwa vile hakuna mwengine naomba niendelee. *(Kicheko)*

Mhe. Mwenyekiti: Dakika tano tukiwa tunamsubiri Mhe. Rashid Seif.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, dakika mbili nitatumia kwa Kituo cha Redio Jamii na halafu kidogo nitakuja kwenye utamaduni. Kituo cha Redio Jamii kilioko Micheweni.

Mhe. Mwenyekiti, nimekitembelea hiki kituo na kweli kinafanya kazi vizuri na kazi inayofanyika kule hata na sisi tungelikuwa tunafaidika kama ingelikuwa tunapata kusikia na kufurahika. Sasa wataalamu walitwambia kama ikiongezwa *aerial* juu kidogo tu basi inaweza ikasikika mpaka Mombasa au ziadi ya hapo. Swali, kwa nini wizara haioni umuhimu wa kile kituo kikaongezwa hiyo *aerial* kama maelezo tuliyopewa ni kweli na sisi tukafaidika na shughuli za Kimicheweni. Hiloni moja.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti ni utamaduni. Mhe. Mwenyekiti, utamaduni wetu tunaujua kuwa umeporomoka kabisa kabisa na umeporomoka kwa kuingiliwa na utamaduni ambao sio wetu katika nyanja zote, mila desturi na kadhalika hata silka. Vizazi vya watoto wetu tunavyowaona, nyendo zao tunaziona na tukifungua hivi vyombo vya habari yaliyoko ukiacha hiyo Televisheni Zanzibar tunayaona na Mhe. Waziri kasema kuwa kazi yake kubwa ni kudumisha huu utamaduni wetu.

Mimi nataka nijue tu, atafanya njia gani kutokana na hali ya hapa tulipofikia kwa kutumia huo utaalamu wake kuona kuwa kweli tunaiweza jamii hii ya Wazanzibari ambao wengi wameshapotoka na utamaduni ambao si wetu na kuweza kuwaingiza katika utamaduni tulionao.

Mhe Mwenyekiti, nashukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Anayeshughulikia Fedha na Uchumi: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nichukue fursa hii kuchangia machache hapa na pale katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo ambaye pia ni Naibu Waziri Kiongozi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza awali ya yote na mimi kwa niaba ya Jimbo la Dimani naomba kuchangia hotuba hii kwa asilimia mia moja. Naiunga mkono hotuba hii kwa nia moja tu, kama mwanamichezo na sisi jimbo letu tunapenda michezo na tunapenda hasa kuendeleza vipaji. Juzi tu nilialikwa Kisauni pale kwenda kufungua mashindano ya *Juvenile*, fainali nimeshamdokeza Mhe. Waziri naomba atafute nafasi kidogo nitamuomba aje atufungie mashindano rasmi.

Mhe. Mwenyekiti, nimepitia hotuba hii na nyanja zote zilizozungumzwa. Kwa kweli lazima tukiri katika safari, safari ni ndefu, kuna mafanikio na matatizo njiani. Hususan katika mambo ambayo mfano nasema wewe kama wizara unaandaa sera, unasimamia lakini kuna jumuiya zake. Nitatoa mfano kwenye *football* kuna *ZFA*, chama cha riadha, kuna chama cha *netball*. Sasa hawa wana sera zao, kanuni, wana mambo yao mengi tu na wengine wanasema hawataki kuingiliwa na serikali, lakini serikali ndio baba na ndio msimamizi. Kwa hivyo, nakubali kwamba tuna matatizo, lakini pia tuna mafanikio makubwa sana.

Leo timu zetu mfano *Coca Cola* nasikia tayari zimeshaingia kwenye *Semi Final* Kusini Pemba, Mjini Magharibi, sijafuatilia vizuri, lakini lengo hasa tizama vipaji vinavyokua. Tukitoka nyuma huko mimi nakumbuka zamani nacheza *Combine, Young African* na timu yetu ya Kisima Majongoo ile ya Mzee Abeid Amani Karume, *African Sports* tunapigwa boli saba, *Zanzibar Combine* na *Dar es Salaam Combine* goli tatu au nne, lakini leo tume-*improve.* Timu yetu ya Taifa ya Zanzibar mwaka jana nakumbuka tumechukua mshindi wa tatu, tumeshashinda Kombe la *Challenge*, zamani tulikuwa hatuko kabisa huko.

Sasa kwa kweli mimi nasema wizara kama msimamizi tumepiga mafanikio makuwa na iko haja ya kuipongeza wizara jamani. Lakini kama ninavyosema tofauti katika *association* zipo kwa sababu wana miko yao, taratibu zao, lakini usimamizi ndio jambo gumu sana na hasa wanaosimamia watu.

Nitatoa mafano kuna matatizo mengi sana. nilizungumza na rafiki yangu hapa Mhe. Salum Abdalla Hamad habari za *association* hizi za wilaya kwenye *league* za wilaya. Kweli *league* za wilaya zina maatizo kweli kweli, kila siku wanawapiga bakora ma-*referee,* wanapigwa faini nakumbuka, ziliwahi timu kufungiwa, lakini siku ya pili pale pake.

Kama ninavyosema ma-*referee* wengine wazito wanaweka maslahi yao mbele kuliko hata maslahi ya taifa. Sasa haya nayo ningeomba kama waheshimiwa na sote tunapenda mipira hapa, kwenye wilaya zetu kule tujitahidi sana tusimamie na twende. Unajua katika nyanja moja ya kampeni nzuri sana ni kwenye michezo katika majimbo kule. Lakini pia tunapo-*promote* michezo tuwapunguzie mzigo hivi vyama, tuipunguzie mzigo serikali, leo *referee* unakwenda unamtandika, unamtia kabali, unamuangusha chini haipendezi. Sasa unafanya madhambi hayo yote halafu unakuja kumuomba msamaha. Bwana tusamehe, timu yetu ndio hivyo ya mtaani hii au ya jimbo, lakini sasa umesahau umemtia kabali umemuangusha chini.

Mimi siku moja watu wangu Jimbo la Dimani walikuja kule, hivyo hivyo, wamemtia kabali *referee* wamemuangusha chini, wakampiga na bakora, wakataka kuwekwa ndani Mazizini pale wakanijia Mheshimiwa tumekuja tunaomba ukatuombee. Nikawaambia mmefanya nini? Tumempiga *referee*. Nikawaambia ah, mmepiga *referee*? Sheria hizo mmziona wapi? Haya utafanya nini tena ndio mtoto akinyea kiganja, nikagomba kidogo pale nikenda nikawachukulia dhamana tukayamaliza.

Sasa haya nataka kusisitiza Waheshimiwa ni matatizo mengi sana ya michezo tunayo. Lakini tukiyasimamia vizuri vipaji tunavyo bwana, vipaji Zanzibar tunavyo Unguja na Pemba tena huko vijijini ndio zaidi.

Zamani tulifikiri labda *footbal*l linachezwa hapa Mjini Magharibi, yaani vipaji vizuri viko hapa, si kweli, vipaji viko mashamba. Kwa mfano, timu yetu ya Baraza la Wawakilishi tulikwenda Pwanimchangani kule tukacheza uwanja wa michanga kule tena sisi tuna viatu wao wamecheza miguu chini, kina Mhe. Ali Abdalla Ali wanapigwa chenga unataka kumhurumia. Sasa hii yote inaonesha kwamba vipaji vipo. Kwa hivyo, ningeomba sana wizara wanaendelea na juhudi zao hizi za makocha kuwatoa wale wanakwenda nje kutafuta vipaji tuziendeleze sana.

Hii naishukuru sana Idara ya Michezo Mhe. Mwenyekiti. Idara hii wanajitahidi suala hili, lakini ndio kama ninavyosema matatizo madogo madogo ya kazi yapo ya hapa na pale.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nigusie sana Sauti ya Tanzania Zanzibar. Kwa kweli mimi nawapongeza sana Sauti ya Tanzania Zanzibar, juu ya matatizo na uchakavu wa vitu vyao lakini wanajitahidi. Wewe peleleza watu wengi sana taarifa ya habari, matangazo ya vifo, matangazo maalum na baadhi ya vipindi kama siku hizi Baraza wote wanafungua Sauti ya Tanzania Zanzibar. Hii inaonesha umuhimu wa Sauti ya Tanzania Zanzibar kama chombo chetu kikuu

na serikali kwa kweli tumejitahidi sana mbali ya mikataba na marafiki zetu wa kichina ya kuongeza nguvu redio hii.

Leo nimesikia na ninawapongeza sana kwamba wamezidisha muda wao wa matangazo, baada ya masaa 12 yamekuwa 15. zamani walikuwa saa tatu wanafunga hapa, wakimaliza matangazo pale wanafunga, leo hawafungi mpaka saa sita usiku. Kwa kweli haya ni mafanikio makubwa sana Mhe. Mwenyekiti na wanastahili kupongezwa. Najuwa wana matatizo ya hapa na pale na hiyo ndio kazi, usipotenda huyaoni matatizo, lakini unapotenda ndio unayaona.

Nakubaliana na waheshimiwa wamesema kweli. Mhe. Waziri Kivuli alizungumza matatizo ya magari, lakini tunajitahidi hapa na pale kuyapunguza. Tumenunua mtambo mpya wa FM ya Unguja na Pemba umechangia serikali yetu. Zamani *FM* yetu ile *Spice* nimeambiwa ni *MW 50*, huisikii popote ukishatoka hapa tu ukiwa unakwenda zako Makunduchi huisikii, leo wana up grade unakwenda *MW100* kama hizi redio za *private.* Redio za *private* zina MW 100 zina nguvu kweli kweli, ukifungu tu wewe ushakamata, sasa na sisi tumewapa nguvu hivyo hivyo, tumewawezesha sisi. Lazima tuipongeze serikali na wizara kwa sera nzuri.

Ninachoomba kwamba kidogo katika watangazaji nao tuwape mafunzo. Tunae Ndugu Suleiman Juma Kimea pale na wengine wanajitahidi, lakini tuwasaidie kidogo. Zamani kulikuwa na *exchange program* wanakwenda zao *BBC*, wanakwenda Redio Ujerumani, wanakaa miezi miwili au mitatu wanakuja zao, *exposure* ile, wakiona nje wenzetu wanafanya vipi basi wakirudi wamegeuka wale ni *incentive* kabisa. Hili ningemuomba sana Mhe. Waziri tuwasaidie. Unajua wenzetu walisoma zamani na teknolojia inabadilika.

Wenyewe nao wizarani huko kwenye televisheni wamebadili kutoka kwenye *analog* sasa wanaingia *digital*, hata zana zimebadilika. Kwa hivyo ningewaombea sana mafunzo madogo madogo sio ya muda mrefu, leo ukamchukue Ndugu Kimea ukamwambie aende kozi ya mwaka mmoja unamuumiza, lakini madogo madogo haya ya miezi mitatu, sita, mwezi mmoja, *exchange program* hizi Mhe. Mwenyekiti, zipo na zinatusaidia sana.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda huku na huku lakini nirudi kwenye riadha. Riadha katika nyanja ambayo wizara nayo na wenyewe wamefanya vizuri sana wa kupigiwa mfano ni nyanja ya riadha. Kwa kweli wametuletea sifa sana na kuna vipaji vingi sana vya wakimbiaji nchini mwetu. Tunae fundi mitambo huwa tunamtania sana tunamwita Bwana Nyambui (Suleiman), yeye tumeanza tangu watoto wadogo, lakini kwa ule wembamba wake ndio akaitwa Nyambui na kweli humkamati anakimbia kweli kweli.

Sasa mimi nilikuwa nataka kumuomba sana Mhe. Waziri najua yapo mashindano ya maskuli yale lakini imekuwa zaidi wanafanya wenyewe tu, lakini tuyafanye kama ya kitaifa. Zamani tulikuw ana siku maalum ya *cross country*, mwenyewe Mhe. Waziri anakumbuka alikuwa mkimbiaji. *Cross Country* zinaanza Ben-bella zinakata Maisara pale zinaangukia kwetu Kiungani kule, zinapandisha Kiinua Miguu inakuwa mji mzima wamekaa wanatizama, wanangoja *cross country.* Yalikuwa mashindano mazuri na vipaji vizuri kabisa. Mimi ningeomba sana Chama cha Riadha na wizara tungerudisha mambo yale ni mazuri yanahamasisha jamii kweli kweli.

Halafu resi za maskuli. Zamani tulikuwa na *primary* mbali na *secondary* mbali. Sekondari zilikuwa zikishandana Lumumba, Jamal Abdel Nassir, Tumekuja na nyenginezo, yaani mashindano kila mmoja ana hamu ya skuli, na siku hizi yapo lakini hayana nguvu kama zamani. Basi ningeomba wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tujitahidi tuyarudishe.

Halafu na *primary* nao hivyo hivyo, Kidongochekundu walikuwa wakishindana na Kiembesamaki, Darajani, una hamu hasa unasisimka na kila mmooja anataka skuli yake ishinde na ilikuwa vipaji vile vinakua. Sasa ningeomba sana wizara mambo kama haya mazuri na wala hayana gharama kubwa, ni mipango tu kuisimamia na kuirejesha itatoa hamasa kubwa sana.

Lakini Mhe. Menyekiti, naomba nimalizie kwa kuwapongeza sana ndugu zetu wa TVZ. Juu ya matatizo waliyonayo ule mtambo jamani umeshachoka na tayari sisi kama serikali kupitia pesa za *MDRE* tumeshawatengea pesa maalum mtambo wa Pemba na wa Unguja kubadilisha kitu kizima kile. Kwa hivyo, mapesa yale ya *MDRE* tumeshawatengea na hivi sasa wamo njiani kutumia hayo mapesa kujaribu kuleta mtambo mpya. Naamini kabisa kweli inauma sana ndugu zetu wa Pemba.

Tulikuwa tunanunua *transmitter* lakini bado kuna mambo mengine. Matatizo ya umeme yale tulikuwa tunaambiwa tuwe na *standby generator*, matatizo juu ya matatizo, lakini sasa umeme ushafika Pemba kwa hivyo, *transmitter* itakuweko kama ya hakiba tu. Lakini tayari tumeshatenga pesa hizo tunaamini *Inshaallah* kabla pengine hatujaingia, aa ni karibu mno. Kwa sababu unajua mambo ya ununuzi ni marefu kidogo. Lakini nia ipo na pesa zipo, kitu kikubwa ndio hicho. Kwa hivyo tutajitahidi mambo tutayaweka sawa.

Mhe. Mwenyekiti, naunga tena mkono hoja ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe tumepokea taarifa kwamba Mhe. Muhyddin Moh'd Muhyddin amefiliwa na mwanawe hivi punde tu katika

Hospitali ya Mnazi Mmoja kutokana na matatizo ya uzazi. Mazishi yatafanyika Bububu njia inayoelekea Kwanyanya baada ya Sala ya Alasiri.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nikushukuru kuweza kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa moyo wake thabiti wa kukipenda Chama chetu cha Mapinduzi na akathubutu kuwa miongoni mwa watarajiwa katika nafasi ya urais wa Zanzibar. Namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri katika mbio zake hizi na *inshaallah* atampa kile alichoomba. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea natoa pongezi zangu za dhati tena kwa Mhe. Waziri kwa kuweza kuiongoza wizara hii kwa ufanisi mkubwa na kwa kweli tunashukuru kwamba alipokabidhiwa wizara hii na sasa hivi tofauti ipo na kila mmoja anaiona.

Mhe. Mwenyekiti, pongezi zangu vile vile ziende kwa Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kwa umahiri wake katika kuwajibu Waheshimiwa Wajumbe wanapouliza maswali mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri ni mtaalam kabisa kwa mambo ya *IT* na hapa alipowekwa kwa kweli ndio pahala pake.

Mhe. Mwenyekiti, pongezi zangu nyengine ziende kwa Katibu Mkuu wa Wizara hii ambaye nae ni mzoefu sana katika shughuli hizi za habari kwa muda mrefu, ni kijana kada wa Chama cha Mapinduzi, kwa kweli tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pongezi zilizobakia naomba nizitoe kwa jumla kwa Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na watendaji wote kwa kazi kubwa wanayoifanya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikianza sasa kisekta nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri kwanza kwa kuweza kuanza kuiboresha TVZ. Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa kwa muda mwingi tukisikitika tukilalamika tunatumia yale makamera ya kizamani, lakini sasa hivi tayari tuna kamera za kisasa na vile vile wakati wowote

wanapokusudia kutoa vipindi vyetu *live* basi wana uwezo huo. Kwa kweli nampongeza sana Mhe. Waziri lakini kama tunavyojua kwamba safari ndefu basi inaanzia na hatua moja.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka niipongeze Sauti ya Tanzania Zanzibar na zaidi nataka nimpongeze Mkurugenzi wa Sauti ya Tanzania Zanzibar, Ndugu Yussuf Omar Chunda.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimpongeze kwanza kuanzia tarehe mosi nadhani ndio leo, unajua siku hizi tarehe tunazisahau, unajua majimboni huko tena michakato unakuwa mara moja unasahau. Kuanzia leo tarehe 01 Julai, 2010 Sauti ya Tanzania Zanzibar inasikika kwa masaa 15 mfululizo. Kwa kweli hizi ni pongezi kubwa za dhati na suala hili tulikuwa tukililia kwa muda mrefu tunashukuru. Kama nilivyosema safari yoyote lazima inaanzia na hatua moja. Sasa naomba sana kwa marekebisho haya basi ule muda ulioongezeka tuutumie vizuri kwa kuweka vipindi ambavyo vitawaelimisha zaidi wananchi wetu.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nimpongeze Mkurugenzi wa Sauti ya Tanzania Zanzibar kwa ubunifu wake. Mhe. Mwenyekiti, kuna kitu kimejitokeza ndani ya wiki mbili zilizopita lakini kuna baadhi ya sisi waheshimiwa tumekuwa tukikilalamikia, suala la kutoa *breaking news.*

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kuna uchukuaji wa fomu wa watu wanaogombea nafasi za urais wa Zanzibar kupitia vyama mbali mbali. Wamekuwa wakilaumiwa hapa ooo maana yake sijui katolewa Moh'd Raza, Raza kama nani. Mimi nadhani kama kweli tunakubali demokrasia na demokrasia hii tusibague kwamba labda kwa kuwa mkubwa fulani yeye ndio kachukua fomu atangaziwe, yule ambaye hana cheo kachukua fomu asitangaziwe. Mimi nadhani hapa huu utawala bora na haki za binadamu na demokrasia hapa kwa kweli tutakuwa tunaidumaza. Mimi wale waliokuwa wanamponda Raza ooo maana yake Raza kama nani, mimi namheshimu sana Raza.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza Ndugu Moh'd Raza ni mwanachama wa Chama cha Mapinduzi ameamua kukichangia chama kwa sababu mambo haya ya michakato anaweza akafanikiwa au asifanikiwe. Hata kipindi kilichopita alijaza fomu. Kwa hiyo, akishafika *stage* hii sisi kwa upande wetu kama Chama cha Mapinduzi tunatakiwa waliochukua fomu wote kwanza tuwape ulinzi kwa sababu wakati wowote atakuwa rais wa nchi hii. Sasa leo tukianza kumdharau mtu kwa kuwa Raza, kwa kuwa nani, mimi nadhani hatutendi haki.

Mhe. Mwenyekiti, unapoamua kuingia katika mchakato kwa sisi Chama cha Mapinduzi, hata mfano mimi ndio niwe Makamo wa Rais nimechukua fomu, basi ninapochukua fomu akitokea balozi wa nyumba kumi hana cheo chochote

baada ya ule ubalozi wake wa nyumba kumi lakini katimiza masharti, basi haki mnakuwa sawa sawa hakuna huyu mkubwa huyu mdogo. Unapochukua fomu umeshajikubalisha wewe ni mwanachama. Chama cha Mapinduzi unalipia kadi ada ndogo tu shilingi mia, sio kama labda Mwenyekiti wa Chama Taifa analipia shilingi mia tano, aaa ada ndio ile ile. Kwa hiyo, mimi nafurahi sana na nampongeza sana Mkurugenzi wa Sauti ya Tanzania Zanzibar.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, sio hawa tu wa Chama cha Mapinduzi hata wengine wanakwenda kuchukua fomu kimya kimya. Sasa unapokwenda kuomba kwamba nataka vyombo vya habari hukupewa pale lalamika. Mhe. Mwenyekiti, mimi namshukuru sana Katibu Mwenezi kawaita waandishi wa habari kawaeleza program yetu uchukuaji wa fomu unaanza lini mpaka lini. Sasa wananchi wanapata kufurahi, wanapata kuona.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Ndugu Yussuf Omar Chunda hata rafiki yangu Joe chama chake nafikiri sijui *NLD*, basi akitaka kuchukua fomu ya urais nendeni kamchukueni *live*, nendeni kwenye chama chao kwa utaratibu wao ndio demokrasia. Kwa sababu hii serikali sio ya CUF na CCM, hii serikali ukishaingia ndani ya madaraka wananchi wote unatakiwa uwaongoze.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu hao ni wachanga ndio wanatafuta misuli ya kuingia hapa, sasa ikiwa sisi tu tuliokuwa na makoti, tuliokuwa na mavyeo tunapokwenda kuchukua fomu tena tutangaziwe kina Joe wasitangaziwe hiyo itakuwa sio demokrasia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba kwamba hii demokrasia maana yake Wazungu wanaita *this is more than democracy*, yaani zaidi kuliko ile demokrasi, demokrasi imepanuka zaidi. Kwa hiyo, Sauti ya Tanzania Zanzibar tunakupongezeni sana na tunakuombeni muendelee na moyo huo huo. Pia akija mwengine yeyote kwa mfano yule wa Jahazi, CCJ akenda kuchukua fomu ya kugombea urais mtoeni *live* na yeye ajisikie hii nchi yetu sote.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani waheshimiwa wasiwe na hofu sana, wengine wanasema walete risiti. Mhe. Mwenyekiti, Maalim Seif Shariff Hamad siku aliyotangaziwa kafa Sauti ya Tanzania Zanzibar ndio wa mwanzo kutangaza. Sio kama wao ndio waliotangaza kafa aaa, baada ya kutoka *rumours* Maalim Seif kafa redio Zanzibar wao ndio waliokwenda kumfuata wakamuuliza *live* dakika 25 nzima. Mzee vipi umeshakufa? bado, uko ngangari? ngagari, kinoma? kinoma. Sasa hakupewa risiti wala hakuambiwa alipe kodi.
Kwa hiyo, mimi nadhani hivi ni vitu vya kawaida, kwani watu wangapi wanatangazwa wamekufa hapa wamefuatwa na redio Zanzibar au TVZ kuhojiwa. Mhe. Mwenyekiti, nafikiri kuna mambo mengine hebu tuiachieni demokrasia ifanye kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema nawapongeza na kwa kweli waendelee na moyo huo huo. Mhe. Mwenyekiti, hili nilitaka niliweke sawa kwa sababu Mhe. Waziri sijui atalijibu vipi, mambo ya kuleta risiti, nani kaomba. Demokrasi Joe, tena nasema Joe leo ukiniona kwenye TV usiku basi siku unayokwenda kuchukua fomu ya urais wa Zanzibar nenda kajitangaze. Pengine unaweza ukaja ukawa rais, msishangae Joe kuwa rais, marais wa nchi hii wanaibuka tu hujui watatokea wapi. Kwa hiyo, hii ni demokrasi. Mhe. Mwenyekiti, rafiki yangu Mhe. Hamad Masoud Hamad amefurahi lakini ndio ukweli wenyewe ulivyo. *(Kicheko)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka niendelee na kutoa pongezi kwa Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri Kiongozi mimi ni mwalimu wangu wa siasa kila siku huwa nasema, nimejifunza mambo mengi kutoka kwake. Mimi nimeingia hapa sijui a, be, che, hata semina sikuwahi kupata, lakini tulikuwa tunakaa tunamuangalia mheshimiwa anavyosema na sisi tunasema, anavyofanya na sisi tunafanya. Kafanya miradi ya maendeleo jimboni nimemuiga, njooni Kwamtipura muangalie nafikiri nimeshampita kwa sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, hata serikalini hapa mwanzo tulikuwa sisi wizara zetu zote ziko Mji Mkongwe, siku zote nasema Waziri yuko ukumbini, Katibu Mkuu yuko chooni, Mkurugenzi yuko wapi sijui, ndio majumba ya Mji Mkongwe yalivyo kwa sababu yalikuwa yanakaliwa na watu. Sasa Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri akasema hapana kwa nini iwe hivyo, kaamua kujenga jengo la wizara.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya yeye kuanza unajua wa mwanzo ni wa mwanzo tu, wengine watakuwa wanaiga tu. Kwa hiyo, yeye kaanza, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kafuata, Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto na yeye kafuata. Pia sisi na Waziri Kiongozi tumefuata lakini tumesema aaa kama nilivyosema huyu mwalimu wetu kwa kuwa yeye kaanza Unguja sisi tumeanza Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi ukenda kule Pemba kuna jengo zuri la Afisi ya Waziri Kiongozi. Sasa haya mambo mazuri yote aliyaanzisha yeye kwa hiyo ni haki yake kuweza kumpa hizo pongezi. Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo kwa kuanzisha utaratibu huu kwa ajili ya ujenzi wa maofisi ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka nizungumze kidogo kuhusu suala la michezo. Mhe. Mwenyekiti, watu wengi wanasema michezo hali hivi. Mimi nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri katika vikao vyetu vya kero za Muungano katika sekta ambayo ilikuwa ina matatizo kwenye kero ni Wizara za Habari. Lakini

tunashukuru mawaziri katika rekodi zangu wanaokaa katika vikao kwa sababu tusisubiri tu kuondoa kero katika vikao aaa, wanakaa ni Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na ile Wizara ya Habari ya Tanzania Bara. Mimi nadhani sasa hivi tukiangalia kuna mambo mengi ambayo tayari yameshaanza kupatiwa ufumbuzi kwa jitihada za Mhe. Waziri.

Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, naona unaangalia saa na dakika zangu 15 zinakaribia kumalizika. Sasa mimi nilikuwa nataka niseme Mhe. Abubakar Khamis Bakary alisema sana maana yake Mhe. Waziri kwenye bajeti yake hakutia maridhiano na nini. Maridhiano tayari yapo mbona wananchi wote wanajua, mpaka mabalozi wa nyumba kumi, watu wa maskani na wengine wanajua. Lakini mimi nataka niseme kitu kimoja maridhiano ni kwenye moyo isiwe kwenye maneno.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitatoa mfano rafiki yangu Mhe. Hamad Masoud Hamad leo yupo. Mhe. Mwenyekiti, hotuba ya Mhe. Hamad ya Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi niliichukua. Mimi nasikitika hotuba ile haikulenga maridhiano bali imewasifu Wanorway, imesema tunawashukuru Ubalozi wa Norway na wananchi wa Norway hakuitaja Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Sasa ule msaada kama si Rais wa Zanzibar, tena hata rais hukumtaja, maana yake huyo bingwa wa maridhiano ni Rais Amani Abeid Karume.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, unajua ile hotuba mimi ndio maana husema hotuba za Waziri Vivuli na Wenyeviti nipewe kwa sababu hotuba zile ndio zinachukua mawazo ya ile jopo zima. Sasa ina maana katika mchango wa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi kwa kweli hamkututendea haki, hamkuitaja Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa jitihada za Mhe. Rais kuleta ule mradi wa umeme Pemba. Mradi ule ulikuwa haumo kwenye bajeti lakini Mhe. Rais kwa jitihada zake akazungumza na wale Wanorway wamekubali.

Lakini pia wenzetu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wametusaidia karibu dola za Kimarekani bilioni 5, sisi tumechangia karibu dola milioni 10. Sasa mheshimiwa angalau ilikuwa utupongeze. Mhe. Mwenyekiti, namwambia Mhe. Abubakar Khamis Bakary kupitia kwa sahibu wangu Mhe. Hamad Masoud Hamad kwamba haya maridhiano yawe ndani ya nafsi yasiwe kwenye maneno. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikasirika mradi ule wa umeme Pemba asitajwe Rais Amani Abeid Karume kaenda kutajwa Balozi wa Norway, aaa mambo mengine taire.
Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache mimi naomba Mhe. Hamad Masoud Hamad urafiki wetu uendelee pale pale haya yalikuwa namfahamisha tu. Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura tunaunga mkono hotuba ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri kweli kabisa unafaa kuwa Afisi ya Waziri Kiongozi. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kutoa mchango wangu pamoja na baadhi ya mambo ya ufafanuzi katika yale yote tuliyopokea kwa mwaka huu.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijafanya hivyo kwanza naomba kuchukua fursa hii kukushukuru wewe, kumshukuru Mhe. Spika, Naibu Spika, Mwenyekiti mwenzako kwa kuliendesha hili Baraza kwa ufanisi mkubwa sana ambapo tunatarajia mwaka huu nchi hii itaweka historia ya aina yake haijapata kutokezea huko tunakoelekea. Kwani mifumo imeshawekwa tayari na tumeona mifumo hiyo, ninaamini huko tunakoelekea kama yalivyokuwa mengine hayajaweza kuepukika basi na hilo nalo litakuja na tutakuwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Amani Abeid Karume kwa kutuongoza hadi kufikia leo hapa tukawa na rekodi za aina yake. Kidogo nimeshangazwa wajumbe hawajagusia rekodi za michezo ambazo naweza kusema zimevunja rekodi za miaka yote.

Kwa sababu mwaka huu katika ukurasa wa kuanzia 61 mpaka kumaliza huku mwisho kwenye 64, basi ni mafanikio mbali mbali yaliyopatikana Zanzibar katika michezo pamoja na medali mbali mbali, ushindi vikombe mbali mbali. Mhe. Mwenyekiti, yote hayo ni chini ya uongozi wa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Amani Abeid Karume pamoja na Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, Mhe. Ali Juma Shamuhuna ambaye amekuwa akituongoza kwa busara, hekima na fikra zake. Kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na uzoefu wake wa kisiasa hadi kufikia hapa leo ambapo tena tunamalizia ngwe hii ili tuanze ngwe nyengine, basi yeye amekuwa akituongoza ambapo tumeweza kupata mafanikio haya yote.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Ali Juma Shamuhuna kwa hekima na busara zake, mbali ya kutuongoza sisi lakini ameona kuwa anafaa, ameshawiva, ameshakuwa tayari sasa kuongoza nchi yetu ya Zanzibar na ameshatumia nafasi hiyo ya kidemokrasia ya kuchukua fomu. Bahati nzuri Mhe. Mwenyekiti, sisi wizara yetu ni ya aina yake tumetoa wawili, yuko mwengine pia Mhe. Hamad Bakari Mshindo nae ametokea Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Kwa hiyo, haya yote ni jumla ya mafanikio ya kufanya kazi chini ya Mhe. Shamuhuna ambaye amekuwa

akituongoza. Mimi pia nawatakia kila la kheri na fanaka katika mchakato huu ulioanza. *Inshaalah* Mwenyezi Mungu ajaalie wafanikiwe.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na pongezi hizo naomba nitoe pongezi kwa watendaji wote wa wizara yetu, nikianzia kwa Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi, Wenyeviti wa Mabaraza, Makatibu Watendaji na wafanyakazi wote wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwa hapa Unguja na Pemba, pamoja na Afisa Mdhamini wa Pemba ambapo tumekuwa tukipata mashirikiano yao makubwa. Kwa sababu mafanikio haya hayaji tu kwa viongozi bali ni kwa mashirikiano ya watendaji ambapo leo tumefikia kuwasilisha hotuba hii ya Mhe. Waziri mbele yako na mbele ya Baraza tukufu ili tuweze kuelekea mbele zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, pia nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi nikianzia na Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii pamoja na wajumbe wake ambao wamekuwa wakitupa mwongozo pamoja na taaluma mbali mbali pale inapobidi, ili na sisi tuwe na mwelekeo ambao utatuletea mafanikio sote kwa pamoja. Mhe. Mwenyekiti, pia niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi ambao wamekuwa wakituuliza maswali mbali mbali pamoja na michango waliyotoa, mawazo, fikra nzuri nzuri kama zile za Mhe. Nassor Ahmed Mazrui juu ya uwanja wetu mpya wa Amaan. Mhe. Mwenyekiti, yale yote naomba nithibitishe kwamba yamepokelewa na watendaji wapo wameyasikia, sisi tupo yatafanyiwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, nikenda kwenye michango mbali mbali iliyotolewa na wajumbe pamoja na mimi mchango wangu, naomba kwanza kabisa nichukue fursa hii kutoa pole kwa familia ya ndugu yetu aliyekuwa msanii, muibuaji vipaji maarufu kwa hapa Zanzibar lakini wengi kwa bahati mbaya hawakumfahamu na leo kidogo nitaomba nitoe wasifu wake ili afahamike. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilibahatika kufanya nae kazi kwa karibu sana ndugu yetu DJ Yussuf Chuchu. Natoa pole kwa familia hiyo na tumeondokewa. Mhe. Mwenyekiti, nitaeleza kidogo sifa zake nani alikuwa huyu DJ Yussuf Chuchu.

Mhe. Mwenyekiti, DJ Yussuf Chuchu ni *promoter* mmoja mkubwa sana wa muziki wa Kizanzibari na miongoni mwa wazalendo wa kwanza waliofungua studio za kurekodia muziki wa Zanzibar, yaani wanaita *Zenj Flava* pamoja na miziki ya taarab asilia. Yeye ndie pia alifanikiwa kum-*promote* Bi Kidude katika nyimbo mbali mbali. Watu wengi wamekuwa wakimuona Ndugu Yussuf Chuchu kama wasanii wengi wanavyoonekana wakati mwengine labda muhuni, anakwenda nje ya maadili na kadhalika. Lakini naweza kusema mtu huyu tulishirikiana nae kwa karibu sana, pia baada ya kufungua kituo chake cha Chuchu FM tulishirikiana sana katika kuokoa baadhi ya maisha duni

waliyokuwanayo mayatima mbali mbali katika nyumba za yatima hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, DJ Yussuf Chuchu mimi nimebahatika kushirikiana nae karibu sana katika nyumba ya yatima Forodhani pale na kila mwezi wa Ramadhan alikuwa akifuturisha pale kupitia kituo chake cha Chuchu FM pamoja na kushirikiana na Kampuni ya Simu ya Zein. Pia mara kadhaa alifanya mipango hiyo hiyo ya kuwapelekea vyakula na kuwatazama wazee mbali mbali waliokuwepo Welezo pamoja na nyumba za wazee pale Sebleni.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kuondoka kwa DJ Chuchu Mwenyezi Mungu amuweke pahala pema peponi, wasani wengi watakuwa wameumia, vijana wengi wa Zanzibar watakuwa wameumia ambapo alikuwa anawafadhili. Kwa sababu hapa katika michango mbali mbali imeelezwa kwamba vijana hawana ufadhili. Mhe. Hamad Masoud Hamad aliombwa shilingi laki saba nakumbuka na ikawa ni ngumu kwake kutoa. Ni kweli kutoa muziki au ku-*produce* muziki ni zaidi ya pesa hizo, lakini DJ Chuchu alikuwa amefungua studio zake ambazo ziko pale Mlandege na vijana wengi wenye vipaji aliwasaidia na kuweza kuibua vipaji vyao. Wapo vijana wengi kama hao ambao leo wamefaidika na wanamkumbuka.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kijana mmoja ambaye nilibahatika mimi kumjua kupitia kwake yeye DJ Yussuf Chuchu anayeigiza sauti za komba na wanyama mbali mbali. Kama wapo wapenzi wanaosikiliza redio hiyo ya Chuchu FM watakuwa wanazisikia sauti hizo huwa zinatolewa. Yule kijana ni mnyonge anatoka kwenye familia ya kimaskini lakini aliweza kufika pale kwa hizo hizo shilingi 20,000 za kupewa, kusaidiwa na kadhalika na leo sauti yake imekuwa kubwa na sasa hivi wenzetu Tanzania Bara wanataka sauti hiyo kuitumia katika vipindi vyao mbali mbali. Kwa hiyo, natoa pole kwa familia ya Marehemu Yussuf Chuchu na daima tutamkumbuka katika mchango wake.

Mhe. Mwenyekiti, pia tumepokea michango mbali mbali, namshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii juu ya pongezi za huyu Alhajj Juma Mmanga na wengine wengi miongoni mwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamemtaja. Mhe. Mwenyekiti, naomba nimtambulishe rasmi leo kwenu. Yule kijana Alhajj Juma Mmanga ni mwanawe Mhe. Raya Suleiman Hamad, mjumbe wetu wa Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, sifa zote kama alizomwagiwa yule kijana, leo sifa zile zinamwendea pia na mama yake Bi Raya kwa kumzaa kijana huyo, kumlea na kumfikisha hapo alipo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nithibitishe kwamba huyo ni *correspondent* wa kuajiriwa wa Sauti ya Tanzania Zanzibar, ni mfanyakazi wetu na pia anafanya

kazi nyengine mbali mbali za *part time* kwenye redio za dini kule Tanzania Bara pamoja na Skuli ya Al-Haramain. Kwa hiyo, huyo ndio Alhajj Juma Mmanga na yeye ndio miongoni mwa mtu wa mwanzo kufika hospitali baada ya kupokea zile *message*. Wengi tulipokea, hata mimi nilipokea *message* ya kushtua ya kifo cha Maalim Seif Shariff Hamad. *Inshaallah* Mwenyezi Mungu ampe umri mrefu tuweze kufikia malengo waliyowekeana yeye na Dk. Amani Abeid Karume ya kuleta Umoja wa Kitaifa katika nchi yetu hii ya Zanzibar ambapo hivi sasa tunaelekea.

Kwa hiyo, Alhajj Juma Mmanga ni mfanyakazi wa Sauti ya Tanzania Zanzibar yeye ndio alifika wa mwanzo pale kumhoji na yeye ndio wa mwanzo kutoa taarifa hizo. Mimi nilibahatika kumpigia sahibu yangu wa karibu sana ambaye tuliwahi kuishi pamoja kipindi fulani Mkunazini pale Salum Bimani na yeye akanithibitishia kwamba taarifa hizo si za kweli akanipa na mkasa wote ulivyotokezea kuanzia *Airport* hali yake ilipobadilika mpaka pale Hospitali ya Hindu Mandal.

Sasa waandishi kama hao kwa kweli tunatakiwa kuwa nao na sisi kwa upande wetu tunajitahidi kuwaenzi, kuwalipa vizuri na vipindi hivyo naamini sifa zote hizi zilizotolewa leo ndani ya Baraza la Wawakilishi atakuwa na yeye amepata na sisi tutazifikisha kwake. Kwa bahati nzuri mama yake yumo humu ndani Mhe. Raya Suleiman Hamad, naomba utusaidie pia kufikisha sifa hizo kwa mwanao.

Mhe. Mwenyekiti, tulipata taarifa kuwa kitabu chetu cha bajeti kilichelewa na Mhe. Waziri Kivuli alilizungumzia hilo suala na alilizungumzia kidogo kwa hisia za ndani kabisa kwa sababu aliguswa na hilo suala. Mimi naomba niseme kwamba katika ratiba iliyotolewa ya awali ya Baraza la Wawakilishi, wizara yetu sisi ilikuwa imepangwa tarehe 4 na tarehe 5 mwezi Julai kama sijakosea, baada ya hapo ratiba ikabadilishwa sisi tukapangwa tarehe 30 Juni na tarehe 1 Julai, 2010. Kwa muda tuliofikisha kitabu ndani ya Baraza kwa ile ratiba ya mwanzo basi naweza kusema sisi tuko mbele kuliko wizara nyengine zote.

Sasa namuomba Mhe. Najma Khalfan Juma Waziri wangu Kivuli kuwa mimi napata mengi pia kutoka kwake kwa sababu imezungumzwa ile sauti ya ladha. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Zakiya Omar Juma alizungumzia kwamba siku hizi ile ladha ya sauti, ladha ya maneno, ladha ya mtu anapozungumza imepungua. Mimi huvutiwa sana na Mhe. Najma anapokuwa anazungumza hotuba yake kwa sababu nakumbukia enzi zake alipokuwa kama mtangazaji na ule mtiririko anavyouzungumza.

Sasa hili najua limemgusa lakini naomba nimuombe sana kwamba sisi kitabu chetu kimefika mapema kabla ya wakati, lakini kutokana na ratiba ya Baraza la

Wawakilishi kubadilika ndio maana yeye kaona kwamba amepata katika muda mfupi. Lakini sisi tulikuwa tumejitayarisha kwa ajili ya tarehe 4 na tarehe 5 mwezi huu. Kutokana na ratiba hiyo yeye mwenyewe hayupo hapa lakini naamini wajumbe wenzake watalifikisha hilo kwake Mhe. Najma Khalfan Juma.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba nieleze kidogo mambo yaliyogusiwa katika hotuba ya Waziri Kivuli juu ya mafanikio yaliyopatikana ndani ya sekta ya redio hapa Zanzibar. Mbali ya pongezi tulizopokea kwamba sasa redio Zanzibar itakuwa inatoa kwa jumla ya saa 15 kwa siku, lakini hivi sasa Redio Zanzibar imerudi upya kama zamani, inasikika kuanzia mwambao wa Msumbiji mpaka Lamu Mombasa. Kwa hiyo, mwambao mzima huu wa Afrika Mashariki kuanzia chini Kusini mwa Tanzania mpaka Kaskazini Lamu kutokana na huu mtambo mpya uliofungwa katika *media wave* wa KW50, basi huo tayari sasa hivi unafanya kazi unasikika na kuanzia leo ndio hizo saa 15.

Mhe. Mwenyekiti, pili kuanzia leo kutakuwa pale ambapo hapana Baraza la Wawakilishi au hakuna program yoyote nyengine asubuhi, kuanzia saa tatu mpaka saa tano ni vipindi kutoka Pemba. Kwa hiyo, waandishi wa habari wa Pemba watakuwa wanaripoti vipindi vyote kutoka Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa Wawakilishi kadhaa walizungumza juu ya wao pia kupata nafasi ya kuzungumza. Kuna vipindi kadhaa vimeanzishwa katika Sauti ya Tanzania Zanzibar na Ndugu Suleiman Juma Kimea ni mmoja wapo wa viongozi wa vipindi hivyo na huwa anawatembelea viongozi mbali mbali kutoka majimboni. Sasa naomba wawakilishi mkifuatwa kwa ajili ya kipindi hicho basi msikatae mwende mpate kuzungumza na nyinyi muweze kutoa michango mbali mbali ambayo imekuwa ikitolewa hapa ili kuweza kufanikisha kipindi hicho hususan wawakilishi kutoka Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba niseme kwamba Sauti ya Tanzania Zanzibar ina mitambo ya KW2 ya *FM radio* ambayo hii ni ya uhakika pamoja na majenereta yake hata umeme ukikatika hayakatiki na pia hutoa matangazo ya uhakika. Siku ile ya viongozi mbali mbali wanaoingia kwenye mchakato basi hawa walisikika katika mtambo huu wa *FM radio* na ule mtambo mwengine ulikuwa unaendelea na matangazo yake kama kawaida.

Lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, ambalo bado linabakia changamoto kwetu sisi Mhe. Mwenyekiti, tunaomba pia Baraza lako tukufu la wawakilishi , kwa sababu wenzetu Bungeni wanafanya hilo, na leo pia nilikuwa najaribu tena kuliulizia na linafanyika, huwa kunakuwa na kasma maalum ambayo inatolewa na Bunge kwa vyombo vyote vya kutoa habari au kupata ile *airtime*.

Kwa mfano Startv ambayo ndio tunatizama mara nyingi kwenye nyakati za usiku tunaweza kuona Bunge. Sasa wale huwa wanapata ruzuku maalum kutoka Bungeni, ile ni *private TV* na hii ni *public TV*. Kwa kuwa sisi muda wetu ni mchache kutokana hii bajeti pia tuliyoipata, tunaomba Mhe. Mwenyekiti, Baraza lako la Wawakilishi lifikirie na kuidhinisha bajeti maalum ambapo muda wa coverage wa Baraza lako tukufu utaongezeka, isibaki pale tu kwenye maswali na majibu bali iweze kuongezeka na Mhe Subeit aweze kusikika na wale samaki wake wanaocheka mpaka kule kwake Micheweni Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na michango mbali mbali, kuna suala la Shirika la Magazeti ambalo Mhe. Haji Faki Shaali aliliuliza, sasa hivi kwa bahati mbaya hayupo lakini naamini atalipata jibu hili katika ukurasa wa 484, ambapo alisema kwa nini shirika hili lina bajeti yake maalum kwenye hiki kitabu, matumizi yake na kadhalika. Lakini kwenye kitabu cha bajeti shirika hili limo kwenye idara nyengine hii ni kutokana na kwamba ni shirika jipya bado hatujapatiwa *votes* kutoka Wizara ya Fedha, au haijapatiwa ile shirika *votes* yake kama *SLS* ili iweze kutoa katika bajeti yake. Kwa hivyo, bado bajeti yake inaingia katika mifumo hiyo mingine ambayo ipo.

Pia Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kuwa shirika hili limeanzishwa kwa kupewa ruzuku ya kawaida ya afisi ya gazeti la Zanzibar Leo, ndio walikoanzia huko kwa mwaka wa fedha huu wa 2009/10 ambayo jumla yake ilikuwa ni Shs. 246,000,000 ambazo zimetumika pamoja na fedha nyengine iliyokusanya hilo shirika lenyewe katika kuendesha shughuli zake za kawaida.

Kutokana na kuanzishwa shirika hilo Mhe. Mwenyekiti, bila ya mtaji kama ilivyotarajiwa katika kuanzishwa Mashirika ya Umma, Shirika la Magazeti ya Zanzibar linaendelea kutekeleza mpango wake mkakati, kuna mpango maalum mkakati ambao umeshafanywa tayari huu bado hatujautoa ndio huu hapa. Mpango makakti wa Shirika la Magazeti.

Mhe. Haji Faki Shaali aliuliza sana juu ya kuwa mtoto huyu atakuwa lini? Mtoto wa Kiingereza wa miaka 16 anaruhusiwa kwenda zake kuishi anavyotaka, lakini mtoto huyu atakuwa lini? Kwa mpango wa mkakati huu basi mtoto huyu atachukua miaka 5 kukua ili ajitegemee mwenyewe na abuni biashara zake mpya, abuni magazeti mengine mbali mbali na pengine atabuni pia na mtambo wake mwenyewe wa kuchapisha ili aweze kuchapisha mambo mbali mbali. Kwa hivyo, muda wake wa kuweza kujitegemea na kusimama kwa miguu yake miwili ni miaka 5.

Ndio maana Mhe. Mwenyekiti, tumeona kwa kuanzia hivi sasa na shirika hili linavyokwenda, limeanza kutoa gazeti la kila Ijumaa la rangi. Kadiri mpango

huo utakavyoendelea na hali ya fedha itakavyoruhusu katika hiyo ruzuku wanayopata, basi litachapisha pia magazeti ya rangi kwa siku mbali mbali za wiki na kuongezeka siku hadi siku mpaka kufikia mwisho kabisa kupatikana kwa gazeti la rangi.

Aidha, Mhe. Mwenyekiti, naomba tuelewe kwamba shirika ni lazima liendelee kulelewa kwa muda huo tulioutaja. Wao wenyewe wametuambia, ingawa mpango mkakati unazungumza miaka 5, lakini wamesema wanaweza wakafika kabla ya muda wao yaani miaka 4 wakawa tayari. Kwa hivyo, nawapongeza pia kwa kujiwekea malengo hayo.

Pamoja na maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, naomba tuelewe kuwa Shirika la Magazeti ufanyaji wake wa biashara ni lazima uzingatie pia huduma, sio biashara tu badala ya kulenga katika biashara peke yake. Kwa sababu hili ni gazeti la jamii na ni gazeti la serikali na ni gazeti la Wazanzibari. Jambo ambalo linaweza kuwakosesha haki ya kupata habari wananchi kama ambavyo inaweza kufanywa na vyombo vya habari binafsi.

Mhe. Mwenyekiti pia Waheshimiwa Wajumbe mbali mbali walieleza kuhusu kivutio. Vyombo vya habari vinakuwa na sera yake na vyombo vya habari daima sera yake inakuwa ni tofauti kidogo na vyombo binafsi. Nilikuwa nasoma gazeti moja leo, gazeti la majira la Jumatano, katika *heading* imeandikwa, Dk. Mwakiembe kufukuzwa CCM. Hajafukuzwa Dk. Mwakiembe CCM, lakini kwa sababu hili ni gazeti binafsi basi huwa linaweka vionjo kama hivyo vya kuvutia habari. Lakini gazeti la serikali haliwezi kutokana na sera yake kuweka vionjo kama hivyo kuvutia habari.

Mhe. Mwenyekiti, kidogo nitaelekea upande wa michezo katika mchango wa Mhe. Haji Faki Shaali, alieleza mashindano ya majimbo ni muhimu na yameibua vipaji vingi. Pia alizungumzia michezo ndani ya mashirika na wizara za serikali. Lakini tuzungumzie zaidi katika mashindano haya ya majimbo. Viongozi pekee ambao wanaweza kushajihisha mashindano haya ni Wawakilishi pamoja na Wabunge katika majimbo. Kwa hivyo, kwa upande wetu sisi tutaendelea kushajihisha mashindano hayo, lakini pia naomba mashirikiano kwa Waheshimiwa Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile ilizungumziwa Kituo cha Redio cha Micheweni, baadhi ya wajumbe wamegusia suala hili na Mhe. Subeit Khamis Faki mwenyewe ameligusia jambo hili. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Subeit Khamis asikae kimpya kusubiri kuitwa kwenye bodi, akiona imechelewa bodi kumuita, basi amfuate Mwenyekiti wake wa bodi amwambie vipi Mwenyekiti, mbona tunasinzia hapa lini tunakutana tena. Nadhani alisema yeye mwenyewe

ni mkuu wa wilaya kama sijakosea. Kwa hivyo, anapokiona kimpya kirefu basi aulizie kwa sababu ile redio inamuhusu na yeye katika jamii yake.

Mhe. Mwenyekiti, kuna wajumbe kadhaa wamezungumzia kuhusu kuongezwa mnara ili redio ile ifike mbali na kadhalika. Ile ni redio ya jamii imefadhiliwa na UNESCO pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa kuwa ni Redio ya Jamii ya Micheweni, hivi sasa kutokana na mkataba tuliokuwa nao na UNESCO, basi inatakiwa itowe matangazo yake kwa jamii ya Micheweni tu. Sasa tukitaka ifike huko kwengine basi tujaribuni kubuni njia nyengine za kuja na redio nyengine.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, redio hii pia ina kasoro ndogo ndogo za kupata maudhui yanayowahusu watu wa pale. Sasa Mhe. Subeit Khamis mwaka huu mimi amenikosha sana, kwa sababu katika Baraza lako tukufu ametupa semina moja kubwa sana ya kilimo cha maweni pamoja na uvuvi, mimi imenivutia sana ile. Kwa sababu kuna mambo matatu mapya ambayo nimejifunza humu. Kwanza samaki anacheka, nilikuwa sijui kama samaki anacheka.

Pili, kwamba bahari yetu utajiri iliyokuwa nayo ambao haujaguswa kabisa. Suala hili Mhe. Mwenyekiti, nililitizama mpaka kwenye *internet* nikaona kwamba ni bahari pekee wanasema samaki anazaliwa mpaka anakufa kwa siku yake ya kufa bila kuvuliwa au kuguswa kwa bahari yetu sisi. Lakini bahari nyengine zote huko Japan na China samaki wanazolewa mpaka mayai yao, lakini sisi bahari yetu imepata bahati kubwa sana ya kuwa na utajiri huo.

Kwa hivyo, namuomba Mhe Subeit Khamsi kwa kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, akipata nafasi basi aitembelee redio hiyo na kutoa vipindi kama vile. Kwa sababu vipindi kama vile au mimi naita semina ile aliyoitoa hapa kwenye Wizara ya Kilimo, Mifugo na Mazingira basi itaweza kuwasaidia pia sana wananchi wa Micheweni. Kama kilimo cha maweni, chooko, mbaazi na mazao mengineyo pamoja na uvuvi basi hayo yanaweza kusaidia sana na ile redio Mhe. Subeit Khamis ipo kwa ajili yao jamii ya pale, naomba na wewe, hutokuwa mtangazaji hapana, basi utakuwa ni muasilishaji mada katika redio ile.

Mhe. Mwenyekiti, suala la EACROTANAL pia liliguswa sana na Mhe. Haji Faki Shaali alieleza juu ya TAKILUKI na mengineyo. Lakini kwa kuwa tumepata nafasi hii ya kujiunga na wenzetu *East Africa Community* na sisi kupata Kamishni ya Kiswahili, tunaona kwamba tuendelee kutumia nafasi hii kama kadiri itakavyowezekana na sasa hivi tumo kwenye mchakato mpaka hapo tutakapofanikiwa kuweza kufanisha suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Uwanja wa Amani. Kwanza mimi nayapongeza sana mawazo mbali mbali yaliyotolewa na Mhe Nassor Ahmed Mazrui na Waheshimiwa Wajumbe mbali mbali juu ya uwanja wa amani. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti hii ni *leagues* aliyowacha Mhe Ali Juma Shamuhuna na itakumbukwa, kwa sababu haya yamefanyika wakati wake.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mkuu wa Mkoa alizungumzia juu ya ile *sealing* iliyokuwepo pale. Zamani anasema kulikuwepo na maguzo kwa hivyo watu wakitaka kutizama mpira kwa hivyo yale maguzo yalikuwa yanawazinga. Ile ni *suspended sealing* na huwa inafanyika kwa mahesabu makubwa sana, ili kupata vile vyuma vya nyuma kuweza kuzuwia dari la mbele na ukitaka vile vyuma vimeanzia mbali sana kule nyuma na vinazuia dari zaidi ya mita 20. Kwa hivyo, ule ni utaalamu wa aina yake ambao sisi Zanzibar tumefaidika pamoja na teknolojia ya raba iliyotumika ile ya kukimbilia ambayo imewekwa pale.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile naomba niligusie suala la Mhe. Saidi Ali Mbarouk, ambaye aliwapongeza CHANEZA kwa msimamo wao thabiti. Mimi pia naendelea kuwapongeza, kwa kweli wamekuwa katika mstari wa mbele katika kutetea haki ya Zanzibar. Naweza kusema kwamba hayo yamefika sehemu nzuri hivi sasa na michakato yao inaendelea vizuri na wataendelea kushirikiana na kukutana na Baraza la Michezo la hapa Zanzibar pamoja na la Taifa.

Pia kuhusiana na kufanya Shirika la Habari la Zanzibar, hili lina faida na hasara zake. Lakini tayari naomba nilijulishe Baraza lako tukufu Mhe. Mwenyekiti, kwamba mchakato ulianza chini ya Uenyekiti wa Mhe. Shamuhuna kama Mwenyekiti, wa Kamati ya Uongozi wa wizara, mchakato huo umeshaanza na bado mijadala inaendelea ili kuangalia hali halisi ya Zanzibar na mashirika kama haya yatatusaidia vipi. Kwa sababu sisi ni tofauti na wenzetu, hali ya kimazingira ya hapa ni tofauti na wenzetu Tanzania Bara na pia ni tofauti na nchi nyengine duniani. Kwa hivyo, inabidi litazamwe kwa mtazamo wa kina kabisa ili kuangalia vipi shirika hili la kujumuisha wote yaani STZ, TV, gazeti na wengineo.

Mhe. Mwenyekiti, nasikitika sana rafiki yangu hayupo Mhe Said Ali Mbarouk, lakini nilikuwa nimemtayarishia majibu ya kihandisi. Lakini nitajaribu kuyatoa katika lugha ya kawaida, kuhusiana na kukosekana TV Pemba. Nadhani hili ni muhimu sana lijulikane.

Mhe. Mwenyekiti, kama utakuwa umeona sasa hivi katika mchakato huu unaoendelea ulimwenguni wa kuhama kutoka *analogy* kwenda *digital*. Wenzetu Bara la Ulaya pamoja na Bala la Asia baadhi ya nchi katika Bala la Asia sasa hivi wameshaondokana na kutumia teknoloji ya *analogy*. Ndio maana hapa kwetu sasa hivi tunapata TV nyingi sasa siku hizi, hizi za *secondhand*

zinakuja kwa wingi sana. Siku hizi Mhe. Mwenyekiti, unaweza kununua TV ya rangi nzuri tu mpaka Shs.50,000/- hapa Zanzibar na hii ni kwa sababu teknolojia ile imeshahama kwao ndio inakuja kwetu. Kutokana na hali yetu sisi tulivyo hatuwezi kupiga vita au kukataza lile jambo moja kwa moja, inabidi tulipokee. Lakini ninachojaribu kusema ni kwamba tunatakiwa sote tuhame kwa nchi zote duniani na ITU, tuhame na tuelekee katika mfumo mpya wa *digital*.

Mhe. Mwenyekiti, kule kisiwani Pemba tukianza kubadilisha sasa hivi wakati tunaelekea kwenye mchakato mpya. Mhe. Waziri wa Fedha kazungumza suala moja muhimu sana, kwamba masuala ya fedha yameshakamilika tayari, lakini haielekei leo tunahama Baraza hili Mhe. Mwenyekiti, tunakwenda kule Mbweni tena tuhame na vikorokoro hivi vyote tuondoke navyo, naamini kule kutakuwa na teknolojia mpya ambayo ni kubwa zaidi. Pengine kutakuwa na *wireless.* Mhe Mwenyekiti, unavaa hapa kwenye kifua kidude kidogo tu kama tunavyowaona wenzetu vyombo vya habari vya nje unazungumza, pengine naamini hivyo, teknolojia hii itakuwa haipo wala haielekei tuhame nayo.

Kwa hivyo, hofu iliyokuwepo ni kamba Pemba tukibadilisha mitambo sasa hivi tukanunua vifaa vyengine ambavyo ni ghali pia na teknolojia ya *digital* inabadilika keshokutwa, basi itakuwa tumeiingiza serikali katika hasara. Kwa hivyo, mchakato unaoendelea sasa hivi ni kuangalia mifumo mipya ya *digital*, hii ni mifumo mipya duniani hata mimi mwenyewe bado sina utaalamu wa kutosha na mifumo hii, kwa sababu ni mipya na nchi nyingi waliohamia kwenye mfumo hii, huwa wanaomba ushauri kutoka katika zile nchi ambazo zinazalisha au makampuni yanayozalisha vifaa vile vya *digital*. Ni vipya na vya aina yake huku kwetu havijawahi kutokezea hata Tanzania Bara bado hawana.

Sasa katika mchakato huu Mhe. Mwenyekiti, sisi tumeona kwamba fedha hizi zitumike kwa Pemba kwa kuanzia. Kwa hivyo, huwenda Pemba wakawa na *advance* teknoloji zaidi kuliko Unguja, nadhani nimeeleweka hapa. Yaani huwenda wakawa na teknolojia ya kisasa zaidi mchakato utakapokamilika kwa hiyo mitambo mipya ili wapate *digital.* Kama Mhe Waziri wa Fedha na Uchumi alivyosema kuwa fedha tayari zipo na hivi sasa tunaangalia utaratibu wa kupata hiyo mitambo ya *digital* badala ya kubadilisha tena *antenna* zile zilizokuwepo za *analogy*, tuweke mtambo mwengine wa *analogy*, ili Mhe. Bi Raya na yeye aweze kuona, itakuwa ni ngumu. Kwa hivyo, hili tunalishughulikia Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo nitowe majibu hayo kwa lugha ya kawaida ili nieleweke.

Mhe. Mwenyekiti, zamani kama itakuwa inakumbukwa, hata hapa Zanzibar tulikuwa tukipata TV basi TV nyengine zilikuwa hazitoi sauti, TV nyengine mpaka zikawekwe crustal kwanza, TV nyengine mpaka ziwe *multy-system*,

kwa sababu kuna *pall*, kuna NTAC, kuna secom, kuna mess secom na kadhalika. Sasa *digital* teknoloji ni teknoloji ya kisasa. Wenzetu wa Afrika ya Kusini wameshaanza na wameanza siku ile walipoanza kombo la dunia, kama mtakuwa mnatizama kombe la dunia basi mtaona kidogo mchezaji akicheza nyuma yake unawaona wale watu kama wako nyuma yake halisi, ile ni digital teknoloji ambayo imeshaanza kutumika na wale wenye picha za *digital* wanamuona mchezaji mbali, yaani wenye TV za *digital* wanamuona mchezaji mbali na uwanja uko kama nyuma yake, wanaita 3d inaweza kuonekana katika teknolojia hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kuna suala la BASAZA kutoa elimu ya maadili na wao pia kuezeshwa na kadhalika. Naweza kusema kwamba wako kwenye hatua za mwisho za kukamilisha mambo yao ambayo yataonekana hivi karibuni na hapa yatazungumziwa katika Baraza lako tukufu. Lakini wakati huo huo, nadhani maadili ni yetu sote na jukumu hili tunalo sote katika mambo mbali mbali, hususan katika hizi sanaa ambazo zinaoneshwa kwenye vipindi mbali mbali vilivyokuwepo.

Vile vile suala la uwazi, kuaminiana na kuondosha hizi dhana zilizokuwepo na kadhalika. Naamini tulikotoka sio sasa hivi hapa tulipo, hivi sasa naamini tuko mbali sana. Bahati nzuri kile kipindi maarufu cha Mhe. Abdalla Mwinyi pamoja na Mzee wetu Bakar Abeid kilitajwa, naamini yeye ana-*compilation* yake, naamini pia pale TVZ kuna *record* zote zile na hili tumelipokea na hivyo vipindi vimeshaanza kuonesha, vinaonesha hivi ndivyo tulivyo, ambalo alilitaja Mhe. Zakiya Omar. Pia vipindi kama vya Dk. Ayoub vinaendelea kuoneshwa katika *cable TV*. Dk. Ayoub kimeshaoneshwa mara moja na tutawaambia wawe wanatoa mara kwa mara ili vipindi vile vilivyokuwa vinatengenezwa hapa na kuweza kuvienzi na kuvikuza vipaji vya wasanii wetu hapa tuweze kuviendeleza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya fani ya sanaa ina *NGO* chache sana ndani yake. hivi sasa tuna *NGO* tatu tu naweza kusema kwa hapa Zanzibar. Moja ni DCMA Dau Country Music Academy, ambapo hawa wanajitahidi sana na tunawapa pongezi nyingi sana kwa sifa zao kubwa. Kwa sababu juzi tu hapa tulikuwa tunawaaga vijana wanakwenda China kuiwakilisha Zanzibar katika music. Pamoja na wengine ambao wamekwenda Poland, vijana wa pale pale ambao wamesoma fani ya music kutoka kwa wale wazee waliokuwa wanaelewa kama Maalim Iddi Farahan na wengine. Kuna kijana mdogo pale anaitwa kijana wa Marehemu Maalim Ali Salum Basalama, yeye huyu amekwenda Poland hivi sasa na anaiwakilisha Zanzibar huko katika fani ya music wa Zanzibar. Lakini ninachotaka kusema ni kwamba tunashajihisha *NGO* zifunguliwe nyingi zaidi.

NGO ya pili ni ZIFF na *NGO* ya tatu ni BUSARA. Hizi *NGO* zimekuwa zikituletea sifa kubwa sana hapa Zanzibar. Nampongeza Mhe. Nassor Ahmed Mazrui kuwa muanzilishi mmoja wapo wa ZIFF. Nakumbuka aliwahi kuzawadiwa mara moja, zawadi maalum ya ZIFF na mimi pia nilibahatika kuchaguliwa kuwa Balozi wa ZIFF pamoja na Mhe. Samia Hassan Suluhu na Mwenyekiti, wake bahati nzuri yuko wizarani kwetu ndugu Hassan Mitawi ndio Mwenyekiti wa ZIFF.

Mhe. Mwenyekiti, utakuta *NGO* zinahitajika nyingi zaidi ili kuweza kuweka matamasha mengi zaidi ili kuweza kuibua vipaji zaidi. Tusizielekeze *NGO* zote kwenye mambo ya UKIMWI, mambo ya mazingira siku hizi na kwengineko, lakini hata huku kwenye music ziko pesa. Kama wale wanaofuata kule basi na huku pia zipo.

Kwa hivyo, hayo nimejaribu kuelezea kidogo na kufafanua kwa upande wa Mhe. Zakiya Omar ambaye alikuwa anaeleza pamoja na masuala ya vyombo vya habari.

Mhe. Mwenyekiti, mawazo ya Mhe. Nassor Ahmed Mazrui yamepokelewa. Lakini ningependa kuongezea katika yale aliyoeleza kwa sababu na yeye muda wake ulikuwa ni mchache naamini alikuwa na mengi sana ya kutupa, na anaweza akatukabidhi baadae katika maandishi. Sasa hivi mbali ya kuwa na *cultural tourism* au *environmental tourism* au *tourism* nyengine wanaita *water sports tourism*. Lakini sasa hivi duniani pia kuna *sports tourism* watu huwa wanasafiri kwa ajili ya kwenda kutazama michezo au kufanya michezo mbali mbali.

Vile vile na hilo wazo lake la Uwanja wa Amani tumelipokea na hatuna hofu ya kuangalia michakato mbali mbali. Wenzetu Tanzania Bara walipofungua Uwanja wao wa Taifa, walialika kampuni kadhaa, nadhani walipata kampuni 9 nakumbuka nilisoma kwenye gazeti ambazo walikuwa wana nia ya kukodi ule uwanja wao wa taifa, lakini baadae walipoona kwamba kuna fedha nyingi sana zinazoweza kupatikana, ndio wakasema, hapana. Tujaribuni kuanya sisi wenyewe, ili hawa wasipate makato makubwa. Wale walikuwa wanataka asilimia karibu 50, yaani kugawana asilimia 50 na asilimia 50 kati ya serikali na makampuni binafsi. Kwa hivyo, katika mchakato naamini hilo pia litaangaliwa na tutaweza kuja na mambo mengine mengi mazuri kwa ajili ya kutunisha mfuko wa serikali nao pia.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na michango aliyotoa Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, na mimi naomba nichangie hapo hapo. Kuna suala la redio mbali mbali alilolizungumzia. Lakini naomba nifafanuwe hapa kwamba kuna *public radio,* ambayo ni redio ya nchi au ya serikali ambayo sera zake ni za kiserikali na

kutoa taarifa kwa wananchi. Kuna *commercial radios*, hawa huwa wanatoa muda mwingi sana kwa matangazo binafsi na matangazo ya makampuni mbali mbali na kadhalika. Kuna *community radio* kama hiyo ya Micheweni niliyoelezea ambayo inaweza kupata vipindi zaidi vya semina kama za Mhe. Subeit Khamis, kuna *religious radios* yaani redio za kidini, ambazo wao huwa mara nyingi wanatangaza masuala ya kidini. Kwa hivyo, hilo naomba niliweke wazi kwamba kila redio inakuwa na miongozo yake na maadili yake ya kutoa taarifa zake.

Mhe. Mwenyekiti, suala la 'Mkongwe Hagewa' pia liliguswa. Hivi sasa naomba nimjulishe Mhe. Mwenyekiti, kwa kupitia kwako niwajulishe Mhe. Mazrui na waheshimiwa wengine wote kwamba 'Mkongwe Hagewa' hivi sasa linataka kugeuzwa kama ni tamasha maalum ambalo litakuwa linafanyika kila mwaka tukijaaliwa. Mwaka wake wa kwanza litakuwa ni kumuenzi marehemu mzee wetu Mzee Ali Omar Baramia, kwa sababu yeye ndio chanzo cha kuanzisha usiku huo wa 'Mkongwe Hagewa'. Kwa hivyo tunaamini huko tunakoelekea halitokuwa tena 'Usiku wa Mkogwe Hagewa' litakuwa ni tamasha la 'Mkongwe Hagewa' nalo nia kuu na dhamira yake itakuwa ni kuwaenzi wasanii, kuwatazama wale hali yao iliyokuwa dhofu, wale waliokuwa wanaumwa na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, suala la *local content* pia lilizungumzwa kwa michezo yetu ya hapa. Naomba niseme kwamba na jamii pia ina mahitaji yake. Mara nyingi tunapofanya uchunguzi wa vyombo vya habari na uchunguzi wetu tulikuwa tumeshaufanya. Bahati nzuri Zanzibar *Broadcast Commission*, lilishafanya uchunguzi wake kwa vyombo vyote vya habari vya hapa Zanzibar. Mara nyingi chunguzi hizo huwa zinatoa matokeo mbali mbali.

Lakini tumefanya uchunguzi mmoja mdogo tu kwangu mwenyewe Mhe. Mwenyekiti. Mimi mara nyingi nikitaka kutazama mpira huwa sipati, kwa sababu kuna hii michezo miwili ambayo mimi huwa siitazami wala kuifuatilia, lakini nimeijua tu kwa sababu ya mazingira ya kwangu yalivyo. Mchezo mmoja unaitwa *dont play with an engel*. Huu najua watu wengi sana wanautazama.

Mhe. Mwenyekiti: Unaitwa *dont mess with an angel*
Mhe. Naibu Waziri Habari, Utamaduni na Michezo: Ina maana Mhe. Mwenyekiti, na wewe unautazama mchezo huu. Ahsante sana.

Mchezo wa pili unaitwa *shade of scene*. Kuna mafunzo mbali mbali kwenye michezo ile kwa jamii, ina maadili yake na inatoa mafunzo kwa watoto. Kwa sababu mimi mwanangu mdogo huwa ananiambia kila mara habari ya huyo mchezaji mmoja anaitwa Mery Chui namsikia anataja sana habari na habari za

ndoa, kwa hivyo huwa ananiuliza maswali, lakini mimi namjibu kwa haya ninayoyajua, sio kwa michezo hiyo.

Lakini ninachotaka kusema hapa ni wana jamii ndio wanaojadili au wanaokuwa na matakwa ya kitu gani au kipindi gani kinachohitajika katika jamii. Sasa leo ukiondosha mchezo huu pamoja na matangazo yake, basi naamini jamii itakuwa na masikitiko yake kwa wale wanaotazama. Kwa sisi tunaotazama mpira, mimi imenibidi ninunuwe hiyo TV ya 50,000/- niliyowaambieni ni ndogo tu hapo Mlandege *used*. Nimevuta ule ule waya wa *cable* mwenyewe bila ya kuvunja sheria, kwa sababu mwenye *cable* nimemjulisha pia kwamba naunganisha TV ya pili ili niweze kutazama ule mpira.

Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kusema ni kwamba na wasanii wetu pia ni changamoto kwao wao kuzalisha kitu kama hiki, kwa sababu ukitazama kipindi cha hapa. Kuna kipindi kimoja huwa nakitazama dunia, unakuta kati ya tendo moja mpaka tendo jengine linachukua muda mrefu sana. Lakini katika michezo hii *dont mess with an angel* pamoja na ile *shade of scene*, unakuta hapo hapo inakuondosha hapa inakupeleka hapa na mwisho wa ule mchezo wewe maisha lazima siku ya pili utataka uendelee wala usiukose na ikifika wakati ule watu wote wanaacha kula, kusoma na kila kitu wote wako kwenye TV. Kwa hivyo ni jamii yenyewe jinsi inavyokwenda kwa michezo hiyo. Kwa hivyo ni changamoto kwa wasanii wetu na wao kuzalisha vitu kama hivyo. Mhe. Mwenyekiti, na kwa bahati nzuri kwa sababu sasa hivi kuna utandawazi watapata kusoma kutokana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mambo hayo hayo ya michezo. Mhe. Ali Abdalla naye alizungumzia kuhusu ule mchezo wa yule *staring* Ray na mafunzo mbali mbali yanayotoka katika mchezo ule. Ndio kama nilivyosema Mhe. Mwenyekiti, ni changamoto na ni kwa jamii yetu.

Mhe. Ali Denge Makame naye alilalamika kuwa wasanii wanalalamika kuwa vipindi vyao havirushwi kwa wakati, wakati mwengine havipo. Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjulishe Mhe. Mjumbe kwamba wasanii nao wanatakiwa watumie zile *production house*, wale wazalishaji vipindi wao wawe wazuri ili vile vipindi visiwe vichafu kwa kwenda kwenye TV. Nakusudia vichafu sio kimaadili, hapana, ni vichafu kwa ile picha yenyewe, yaani ile picha yake iwe safi ambayo inaweza kushindana na vipindi vyengine. Kama sio hivyo basi na wao hawatakuwa katika ushindani. Kwa hivyo, hilo ni muhimu sana katika kuzalisha vipindi ambavyo ni vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, wapo na ma-*promoter* wengine, kuwa na *promoter* ni kitu muhimu sana. Nilimtaja mmoja ambaye ni marehemu Chuchu alikuwa ni *promoter*, pia ni mzalishaji wa vipindi hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti: Nakuomba umalizie.

Mhe. Naibu Waziri Habari, Utamaduni na Michezo: Nimalizie. Nina mengi kweli. Haya.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala ambalo Mhe. Raya aligusia juu ya kivazi maalum cha Mzanzibari, naomba nimjulishe kwamba kuna kampuni moja ambayo inaitwa *explore Zanzibar* wao wanafanya maonesho ya kivazi cha Mzanzibari ambayo yanafanyika hapa na mara nyingi huwa tunakwenda kutazama kivazi hicho baada ya kutoa matangazo mbali mbali. Kuna michezo iliyokufa kama mchezo wa ng'ombe, naomba tushirikiane pamoja na Mhe. Omar Ali Jadi, ili mchezo huo kuufufua kwa sababu ni mchezo mzuri sana. Kwa kule Spain unapendwa sana mchezo huu. Nina amini wale ng'ombe bado wako Pemba, naamini hivyo. Kwa sababu nilibahatika kutembelea katika Jimbo la Mhe. Abass Juma Muhunzi, nikaambiwa pale ngoma ya Kiyumbizi pamoja na mchezo huo ndipo unapochezwa, nikaoneshwa mpaka ule uwanja. Nikawaomba watendaji wetu kule, kwamba tuandae basi kitu kidogo hapa, angalau na sisi tuburudike, lakini hatujafanikiwa. Sasa naomba tukija tena ziara *Inshaallah* Mhe. Shamuhuna akishafanikiwa mchakato wake tutakuja huko kwenye kampeni, basi naamini tutaweka mchezo huo ili kuvutia pale watu wengi zaidi kuja kwenye mchezo huo ili tuweze kuona sote kwa pamoja na itakuwa ndio tunamalizia tena katika kuweka mambo sawa katika wizara yetu hii ya Habari, Utamaduni na Michezo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba dakika mbili au tatu tu nimalizie ya mwisho kabisa. Mhe. Hamad Masoud Hamad alizungumzia kuhusiana na hii *Bong Flavor* au *Zenj Flavor*, lakini Mhe. Hamad Masoud vijana siku hizi wamekuja na kitu kinachoitwa *fusion* yaani wanachanganya yale ya kisasa na ya zamani. Kwa hivyo, utakuta katika hiyo hiyo *Zenj Flavor* unakisikia kile kinanda cha zamani na mlio wa zamani ule ule. Kwa hivyo, nyimbo zile zile za zamani wanapiga kwa mitindo ya kisasa.

Kuhusu gharama nyingi za ZFA hilo limeshachukuliwa linafanyiwa kazi ili kupunguza gharama na wale wachekeshaji wawili leo niliwapata lakini bahati mbaya hawakuweza kufika hapa, kwa sababu nilitaka kuwaleta hapa kidogo ili na wewe upate kucheka, lakini hawajaweza kufika. Kwa hivyo, tutapanga programu nyengine maalum ya wao kuweza kuja, tutamuomba Mhe. Mwenyekiti, aweze kuwatambulisha tu kwa Baraza la Wawakilishi, ni wadogo sana, lakini Mwenyezi Mungu amewajaalia vipaji vikubwa sana vya kuchekesha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kabisa naomba niseme kwamba kuna michezo ambayo imetajwa na Mhe. Subeit Khamis, ule mchezo wa taro na ule

mchezo wa ngware, kama sijakosea. Hii michezo itatazamwa tena upya kwa sababu hatutaki michezo ya watu kuumizana mpaka tena wakauwana na wasiweze kushtakiana, hapana. Lakini tutatizama tena michezo hii ili tuweze kuona nini tunaweza kufanya.

Kwa hayo machache tu Mhe. Mwenyekiti, naomba niunge mkono hoja hii ya Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, nadhani tumejitahidi kuzungumzia maeneo mengi. Kwa hivyo Mhe. Waziri mwenyewe atakuja kuyaweka sawa mengine yale tuliyoyasahau kwa upande wetu, kwa sababu yeye ni ndiye kiongozi wetu na tunapata busara pamoja na hekima kutoka kwake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache naomba kuunga mkono kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mpendae kwa asilimia mia moja *(Makofi)*.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri, kwa umahiri mkubwa umeweza kujibu hoja nyingi ambazo zimetolewa hapa. Kwa hivyo, nategemea Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, kwa hekima, busara, maarifa pamoja na uzoefu hatoyarudia yale. Kwa kweli alikuwa bosi wangu katika Wizara ya Kilimo *(Makofi)*.

Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kwa ajili ya kufanya majumuisho ya michango wa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Vile vile nimepata faraja Mhe. Mwenyekiti, kwamba wakati nilipotoa hotuba yangu ulikuwepo na sasa nafanya majumuisho bado upo na Mwenyezi Mungu atakupa umri mrefu utakuwepo na sisi kila siku *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo amenisaidia sana takriban amejibu maswali yote yale ya *highly technical*, pengine hata ningeyajibu yasingeweza kufahamika kama alivyoyajibu yeye na yakafahamika ninahakika hiyo.

Sasa napenda niwatambue wale waliochangia hotuba yangu jumla ni Waheshimiwa Wajumbe 22 ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Ali Suleiman Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii,
2. Mhe. Najma Khafan Juma (Waziri Kivuli wa Wizara ya Habari, Utamduni na Michezo),
3. Mhe. Hija Hassan Hija,

4. Mhe. Haji Faki Shaali,
5. Mhe. Said Ali Mbarouk,
6. Mhe. Zakiya Omar Juma,
7. Mhe. Nassor Ahmed Mazrui,
8. Mhe. Abubakar Khamis Bakary,
9. Mhe. Ali Abdalla Ali,
10. Mhe. Ali Denge Makame,
11. Mhe. Raya Suleiman Hamad,
12. Mhe. Omar Ali Jadi,
13. Mhe. Asha Moh'd Hilal,
14. Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja,
15. Mhe. Hamad Masoud Hamad,
16. Mhe. Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi,
17. Mhe. Haji Mkema Haji,
18. Mhe. Subeit Khamis Faki,
19. Mhe. Salim Abdalla Hamad,
20. Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi,
21. Mhe. Zahra Ali Hamad na
22. Mhe. Suleiman Hemed Khamis.

Mhe. Mwenyekiti, Waheshimiwa wawili wa mwisho wamechangia kwa maandishi. Kwa kweli ninawashukuru sana wajumbe hawa kwa michango yao mizuri na wengi wameshauri na tunaupokea ushauri wao na wengine wamekosoa, pia tunayapokea na tutayafanyiakazi na wengine wamenipongeza *(Makofi)*.

Nataka nitoe kauli kwa wale wengi walionipongeza na *Inshaallah* midomo yao iwe ya heri kwa siku ya leo na Mwenyezi Mungu akitaka na akiwasikiliza kwa jinsi walivyonipongeza, basi nitafanikiwa *Inshaallah (Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, umeniongoza na kuninasihi nisirejee. Kwa hivyo, majibu ya Ali Suleiman Ali (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii), zaidi ya kuzipokea shukurani zake na yaliyobakia Mhe. Naibu Waziri ameyajibu na hali kadhalika na Mhe. Najma Khalfan Juma (Waziri Kivuli wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo).
Kutokana na hali hiyo, nataka niongeze kidogo kwa Mhe. Najma Halfan Juma kuhusu masikitiko yake ya kukawia kupata kitabu. Mhe. Naibu Waziri ameyazungumza vizuri, isipokuwa nataka niseme kwamba hakuna aliyepata kitabu mapema kuliko jana au juzi, yaani vitabu vyote vimetolewa vyote kwa wakati mmoja tena siku moja, vilitolewa kwa ajili ile tarehe 4 na 5 ya uwasilishaji wa bajeti yangu.

Kutokana na mabadiliko ndio naweza kusema kimechelewa kwa siku moja na badala ya kukipata siku mbili kabla, basi kimepatikana siku moja kabla. Kwa hivyo, sidhani kama wizara hii tunabagua kiasi hata cha kutoa kitabu wengine tuwape na wengine tusiwape, kwa sababu vitabu sisi tunapeleka Baraza la Wawakilishi na hilo ndilo lenye kugawa vitabu na wala sio wizara *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba radhi na kama bado hakuridhika na kukerwa kwake, lakini hali halisi ni hiyo.

Mhe. Mjumbe mwengine aliyechangia ni Mhe. Hija Hassan Hija, nadhani ameridhika na yale majibu yaliyotolewa na Mhe. Naibu Waziri. Lakini nataka nizungumzie suala moja ambalo Mhe. Naibu Waziri hakuligusia nalo limechangiwa na Wajumbe kama wawili watatu, kwa nini sisi wa CCM wakati tunapokea na kurejesha fomu na CUF hawakuoneshwa.

Tatizo ni dogo tu sisi wa CCM hatufichi mambo yetu, kwa kweli hatukupata taarifa kwa Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad siku gani ambayo alikwenda kuchua na kurejesha fomu, kwa sababu yale ni mambo ya ndani ya chama chao. Nadhani kama wangetuarifu, basi tungefanya hivyo kama tulivyowafanyia wale wa CCM *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu tusaidiane katika kutekeleza haya malengo tuliyoyazungumza hapa ya kuweka usawa. Kwa hivyo, kinapotokea cha CUF tuambiwe na tuweze kuki-*cover* na vile vile kikitokea cha CCM tukiambiwa basi tutaki-*cover*, mkificha msilalamike maana ndio mmekificha *(Makofi)*.

Baraza la Kiswahili aligusia na kusema mwanzoni mwa mwaka juzi na jana tuliambiwa kwamba kuna matayarisho ya Kamusi za Lahaja za Kitumbatu na Kimakunduchi, leo tunaambiwa tunatayarishiwa Kamusi la Lahaja za Kipemba. Sasa hizi za Kitumbatu na Kimakunduchi zimefika wapi? Jibu lake tumeshaziandika bado kuzichapa, ndio maana sasa tunakwenda kwenye kundi la tatu la Lahaja za Kipemba. Kwa hivyo, jibu lake ndio hilo na wala sidhani kama kuna haja ya kunipigia mguu.

Academy ya Michezo itamalizika lini? Kwa kweli hivi sasa tuko katika hatua ya kutengeneza uwanja wa michezo na nyumba tayari zimeshamalizika na tukimaliza kazi hiyo na wala siahidi, lakini huenda tukamaliza kabla ya kuondoka. Matumaini yangu makubwa mwaka huu haumaliziki *Academy* ya Michezo itakuwa iko tayari.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile wengi waliuliza kuhusu Hoteli ya Uwanja wa Amani, mbona tumejenga uwanja tu, lakini hoteli hatukuifikiria. Kwa kweli hoteli ile haikuwemo kwenye mpango wa kukarabati uwanja ule, lakini sisi

wenyewe tulikuwa tumejitayarisha na sasa kazi ya kuikarabati hoteli ya uwanjani tayari imeshaanza.

Kwa mfano, ukipita kwa barabarani huwezi kutofautisha kati ya uwanja na hoteli, yaani vyote vina sura ya aina moja. Kwa hivyo, kazi iliyobakia sasa ni kuweka vifaa vya ndani, kama vile *cooker*, *refrigerator* na kadhalika. Kutokana na hali hiyo, muda si mrefu tutakapoanza mchakato wa matumizi ya bajeti hii, nafikiri kazi imebakia thuluthi moja na tutaimaliza.

Lakini hatukukaa na kujivisha koti zuri na suruali inaviraka, hapana tunafanya kwa wakati mmoja. Mhe. Mwenyekiti, nadhani tukubali kwamba Rome haikujengwa kwa siku moja, tutafanya kidogo kidogo na mpaka tutafika pale ambapo tumekusudia *(Makofi)*.

Vile vile jengine ambalo halikuguswa ni kuhusu majengo ya watu binafsi yalioko upande wa Mashariki ya Uwanja wa Amani. Kwa kweli majengo yale tuliyakuta na wanavyo vibali na wala hatuwezi kusema sasa tuyaondoshe, ingawa majengo yale yamo kwenye eneo la Uwanja wa Amani. Lakini kwa bahati mbaya kibali kimeshatoka na ujenzi umefanyika mpaka hatua ile iliyofikia hakuna namna, isipokuwa tustahamiliane na tufumbe macho.

Mhe. Haji Faki Shaali namshukuru sana kwa michango yake. Nadhani ametoa michango mizuri sana kwa sababu yeye ni mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, ndio maana michango yake ikawa mizuri, kwani ya ndani anayafahamu.

Mhe. Mwenyekiti, nitazungumzia kuhusu mambo mawili au matatu. Kwanza kuhusu mashindano ya mawizara na mashirika, Mhe. Mjumbe aliyaona hayana *impact* kubwa kwa shughuli zetu za kikazi, yanaweza kupelekea kuitumia bajeti yetu vibaya kwa kushughulikia michezo zaidi kuliko kazi.

Mhe. Mwenyekiti, mtazamo wangu, wa wizara pamoja na wananchi walio wengi kuwepo michezo ile, *infact* michezo ile tunaifufua, kwa sababu ilikuwepo zamani na kushamiri sana na baadaye ikafa. Kwa hivyo, hivi sasa katika juhudi za kurejesha michezo ya zamani yenye maana ifufuliwe ndio huu tumeufufua.

Kwa kweli mimi mwenyewe juzi kwa kuithamini michezo hii nilitoa kikombe kizuri sana, ili kikombe hiki kishindaniwe katika mashindano ya mchezo huu. Utaratibu wa kushindaniwa wenyewe wahusika wataupanga, ikiwa atakayeshinda mara moja au tatu kitakuwa chake, watajua wao wenyewe.

Lakini nimefanya hivyo kwa kuthamini kwamba michezo tuliyokuwa tunaiendesha zamani, sasa wametokea watu wenyewe kwa ridhaa zao na kusema irudishwe na wizara ikaunga mkono na sasa tunaurejesha. Kwa hivyo, asiwe na wasi wasi kwa sababu bajeti inatolewa kwa kasma au vifungu na Mhe. Waziri katika wizara inayohusika atakuwa *very careful* katika kuzitumia fedha hizi.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Redio Jamii Micheweni ametupongeza na tunazipokea pongezi zake. Vile vile amesema tutafute wataalamu kutoka nje wa kuzifanya *programs* zetu ziwe bora zaidi.

Ushauri tunaupokea lakini nataka niseme kwamba kwanza tunafanya juhudi za sisi wenyewe kuwapeleka wanahabari hawa Sengerema. Sengerema ni sehemu nyengine ambayo redio kama hii ipo, wenzetu wameendelea sana, kwa sababu wao wameanza kiasi miaka miwili iliyopita.

Hivi sasa *programs* zao zinatoa maelezo hata za bei Soko la Sengerema kwa bidhaa mbali mbali. Kwa hivyo, ningependa na sisi Micheweni tukatoa taarifa za Masoko yetu ya pweza, samaki na kadhalika, lakini wao wameanza zamani ndio wamefika huko na sisi tumeanza juzi. Kutokana na hali hiyo, nakuombeni sana mtupe muda.

Mhe. Mwenyekiti, Redio hii ni ya Jamii na sio Redio ya Serikali *perse*, isipokuwa ni Redio Jamii ya Watu wa Micheweni. Sambamba na hili najibu na wale waliosema tukiweka *antenna* moja kubwa Mhe. Salim Abdalla Hamad alisema tukiweka *antenna* moja kubwa, basi ile redio inaweza kufika mpaka Mtambwe pamoja na sehemu nyengine mbali mbali na watu wengi wakapata faida.

Kwa hivyo, nasema tusiwaone choyo watu wa Micheweni, kwa kweli watu wa Micheweni wamebahatika kwa sababu wamekubalika kwamba wako nyuma sana kimaendeleo. Kutokana na hali hiyo, ndio maana tumeweka redio jamii, ili iwarutubishe mawazo ya kimaendeleo, kilimo, mifugo, maisha na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, hii ni *specifical* kwa Micheweni na wala si kwengineko kokote, bado redio tunayo hivi sasa ya *MW 50 Kiliwatts*, ambayo inasikika kila pahala *almost 24 hours*, basi turidhike na kisikiliza redio hiyo, lakini hii Redio Jamii ya Micheweni tuwaachie wenyewe jamii ya Micheweni.
Chuo cha Uandishi wa Habari Mhe. Mjumbe alishtuka kwamba hadi leo bado hatujajiunga na hiyo *NACTE*, kwa kweli bado hatujajiunga, kwa sababu yapo masharti ya kujiunga, kwa bahati nzuri masharti tumeshayatimiza. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa tunasubiri waje watukague tu na ninahakika

watakapotukagua basi watatupa *certificate* na kuweza kujiunga, baada ya kujiunga *diploma* iko tayari.

Kwa hivyo, tumechelewa lakini kwa sababu, kwa kweli huko tunakotoka tusingeweza kujiunga kwa kuwa tunategemea kwa asilimia 80 walimu wa *parttime* na wala sio wa kudumu. Hivi sasa idadi hiyo imepungua na tumeongeza idadi ya walimu wa kudumu yenye *qualification*, yaani sifa za kutosha, ingawa bado tunao walimu wa *part time*, lakini wengi ni wa kudumu.

Pamoja na mambo mengine ambayo yalikuwa hayajakamilika hivi sasa yamekamilika, ninahakika wakija hao *NACTE* watatupa *certificate* na kuweza kusajili, tukisajili maana yake vyeti vyetu vitakuwa vinatambulika *East Africa* nzima.

Vile vile alizungumza kuhusu kucheleweshwa kwa vyeti vya kuzaliwa na Idara ya Upigaji Chapa (*Press*). Mhe. Mwenyekiti, *Press* haicheleweshi vyeti vya kuzaliwa, isipokuwa inasubiri kupata maombi na inapopata maombi basi inatengeneza hapo na inawakabidhi watu wa Afisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo, sasa wao kama kuvitoa kwa siku ile ile au utaratibu mwengine wowote inakuwa ni juu yao. Lakini sisi hivi sasa tunavyozungumza hatuna ombi la kutengeneza vyeti vya kuzaliwa na tunapolipata hilo ombi basi kazi hiyo inafanywa.

Suala jengine kuhusu Sherehe za Kijeshi hazifanywi tena Uwanja wa Amani zitafanywa wapi? Mhe. Mwenyekiti, imeundwa kamati ya kutafuta maeneo. Kwa kweli kamati tayari imeshafanyakazi yake na imepata maeneo mawili moja ni Bungi la pili ni Dole *(Makofi)*.

Kwa hivyo, wahusika wakeshakuchagua lipi linalofaa kazi ya kulitengeneza hilo eneo litafanywa na hapo ndipo patakuwa eneo rasmi pa kufanyia Sherehe zetu za Kitaifa inazohusu majeshi. Kwa hivi sasa tutaendelea kutumia Uwanja wa Gombani *(Makofi)*.

Mhe. Said Ali Mbarouk, nimepokea pongezi zako, lini tutaanzisha *ZBC*. Mhe. Mwenyekiti, tunajaribu kama inavyowezekana kwenda kwa *path* zetu wenyewe bila ya kumuiga mtu, si vibaya kuiga kilichokuwa kizuri. Kwa bahati nzuri wizara zetu mbili za habari zinao ushirikiano wa karibu sana, kwa kweli tunasaidiana, kuazimana pamoja na kushirikiana.

Mhe. Mwenyekiti, hivi ninavyosema wenzetu wanazo *cameras* zetu mbili kati ya zile sita ambazo tulizoziagiza, tumewaazima *cameras* mbili kwa ajili ya kufanyia baadhi ya vipindi vyao. Kwa kweli hizi *cameras* zetu ni za kisasa

kabisa, yaani *digital* tena ni nzuri sana na walipoziona wao wenyewe wamestaajabu. Lakini lazima kwa kuwa kuna upungufu huo basi tumewaazima.

Vile vile na wao wametukumbusha kwamba wanaushirika na Kampuni ya Kichina kwa ajili ya kushughulikia suala la utangazaji wa kileo kabisa *Multiplus Operation or Operator*. Mhe. Mwenyekiti, wametuelekeza badala ya kutumia fedha nyingi sana kwa kukamilisha shughuli za *digitalization*, basi tukiungana na mtambo ule tutaweza kufika Afrika nzima katika hali sawia sana ya yale tunayoyaona kutoka *TBC*, kwa sababu wao sasa wanatumia kifaa hicho.

Mhe. Mwenyekiti, hivi juzi tumepeleka wataalamu wetu na tayari tumekubaliana. Sasa hiyo ndio faida ya kufanyakazi kwa pamoja, pengine nayo litatuondoshea tatizo la televisheni Pemba. Kwa kweli tulikuwa tununue *transmission* au *transmitter* maalum kwa ajili ya Kituo cha Pemba, huenda tukaona haina haja na hata ile ya Unguja kutokana kutumia kifaa hiki cha *Multiplus Operator*.

Kutokana na kwamba hivi sasa umeme Pemba *Alhamdulillah* upo na wala sidhani kama tutapata tabu za *fluctuation* za juu kwa juu na kuweza kuunguza mitambo yetu, itakuwa tumesalimika.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mhe. Mjumbe amezungumza kuhusu masuala ya sanaa ametoa mfano wa Nigeria na kwengineko, ushauri tumeupokea. Vile vile Wete hakuna viwanja vya mpira, Afisa Mdhamini yupo hapa na amelisikia hilo tutashirikiana pamoja na Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Wete kwa ajili ya kutafuta eneo mbadala au kusaidia pamoja na kushirikiana kutengeneza hicho kiwanja.

Kwa hivyo, tukiacha yale majibu ya Mhe. Naibu Waziri aliyoyatoa nadhani Mhe. Mjumbe ameridhika na mchanganua wangu.

Mhe. Nassor Ahmed Mazrui namshukuru pamoja na kumpongeza. Kuhusu pendekezo la kukibinafsisha Kiwanja cha Amani ah! Hivi majuzi tulikuwa na kiwanja kibovu mbona pendekezo hili halikuja. Kwa hivyo, tunataka kukibinafsisha Kiwanja cha Mao-Tse-Tung ama kukibinafsisha kwa asilimia mia moja, au kukibinafsisha kwa *joint ventures* au kukibinafsisha kwa kukikodisha *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, tunamuomba Mhe. Nassor Ahmed Mazrui ama yeye mwenyewe aje au atutafutie wawekezaji binafsi na kiwanja kiko *available* na tutakitoa *immediately* na mikataba ya kubinafsisha ikiwa mizuri, basi kiwanja hicho kipo. Lakini Kiwanja cha Amani tukiache kwanza na kiwe mikononi

mwetu na tuangalie tutakavyokilea na kitakavyodumu na ikifika wakati wa kukibinafsisha basi tutapokea wazo lako.

Kuhusu suala la michezo Mhe. Mjumbe ametuambia michezo imekufa *on the contrary* michezo imefufuka, tena imefufuka kwa nguvu sana na tunashinda medali nyingi sana. Kwa mfano, hivi karibuni nilikutana na Watu Wenye Ulemavu wa Akili wanatokea michezoni, wakati mmoja nilikutana nao wakiwa na medali sita na hivi juzi nimekutana nao tena wanazo medali 27.

Miongoni mwa hizo medali nyingi za dhahabu, zinafuatia za fedha na chache ni za *brown* michezo jamani ndio imekufa hivyo, maana tumeingia mpaka kwa Watu Wenye Ulemavu, kuhakikisha na wao wanapata haki yao *(Makofi)*.

Mhe. Mwenyekiti, labda nimhesabie ile michezo ambayo tumefufua na ipo na inaendelea. *Squash* tunashinda mara nyingi sana michezo ya Afrika ya Mashariki. Vile vile *Badminton, Basketball, Athletics, Judo, Netball, Football, Golf.*

Mhe. Mwenyekiti, hivi majuzi mchezaji wetu wa *golf*, yaani miezi minne iliyopita ameshinda namba moja Tanzania na mara ya pili ametokea mshindi wa pili. Hivi sasa tumeshawapa *assignment* watu wa *golf* na tumewapa kiwanja kwa ajili ya kukikagua, watakapokikubali wataanza kutengeneza ramani zao pamoja na utaratibu wao, basi tutawakabidhi kiwanja chenye hadhi ya kimataifa kwa ajili ya kucheza *golf. (Makofi)*

Sasa kulinganisha na idadi ya michezo tuliyoifufua na medali tunazozichukua, Mhe. Mwenyekiti nakata kusema michezo imekufa, isipokuwa michezo haijafa na ninamuomba Mhe. Mjumbe tusaidiane kwa lengo la kuifufua. Kwa hivyo, yeye mwenyewe ni mwanamichezo, basi apitie kwenye hizi sehemu na tuweze kushirikiana katika kukosoana na wapi tukaze kamba, ili michezo ifufuke kwa nguvu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Gazeti la Zanzibar Leo linaendeshwa kibiashara, nakubali. Lakini mpaka sasa Zanzibar Leo nusu ni Shirika, nusu ni Gazeti la Serikali. Kwa hivyo, tunajitahidi kulilea na tumewaachia makusanyo yao yote. Kwa mfano, tukiangalia kwenye kitabu sehemu ya mapato Zanzibar Leo zero, yaani hapana kitu, kwa sababu tumewapa nafasi kile wanachokipata wakitumie, ili kujipa nguvu zaidi na kufufua.

Kwa kweli lazima tuweke *target* mpaka lini, nadhani kwa muda wa miaka mitano tunaweza kuwaachia wenyewe wakajiendesha. Mhe. Mwenyekiti, hili nahakika nalo wataweza kulifanya.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary. Nadhani ile dua niliyoiomba imesibu Mhe. Nassor Ahmed Mazrui usende kumwita. Lakini majibu ya maswali yake tunayo na ninapenda nieleze kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kitabu chetu hakijaandika kazi nzuri iliyofanywa na Rais Amani na Maalim Seif Sharif Hamad ya kutuletea amani na utulivu na kuelekea katika mchakato wa kura za maoni, mimi kama ni Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo sikuona haja wala sababu iwe ni kosa kutokufanya hivyo, lakini masuala haya tumeshayazungumza sana na kazi hii ya kutamka tamka kila wakati iliachiwa Tume ya Uchaguzi.

Nadhani Tume ya Uchaguzi sasa hivi kazi hii imekabidhi kwa vyama vya siasa, sasa Mhe. Abubakar Khamis Bakari kama ni kiongozi wa upinzani yeye alipaswa kutumia nafasi yake ya kulihubiri suala hilo hata kama ndani ya Baraza la Wawakilishi kwa wakati wake unaofaa, lakini hata nje. Na sisi wenzake tunafanya hiyo kazi tena kwa nguvu zetu zote.

Mhe. Mwenyekiti, naomba tusinyoosheyane vidole kwamba wewe unataka wewe hutaki, wewe umesema wewe hukusema hebu turudi kwenye Ma-*hansard* yetu yanasemaje katika michango yetu tulipochangia tulisema nini, lakini juzi wakati nilipokwenda kuchukua fomu nilionana na waandishi wa habari hili suala lilikuja tena. Bwana tukikupa urais utafanya nini nikasema nitadumisha yale yote yaliyoamuliwa na Chama changu tena yale ya mchakato wa serikali ya mseto kama vile yalivyoamuliwa kule Butiama Tanzania Bara, na kama tulivyoamua kwenye Baraza la Wawakilishi yule bwana hakutosheka.

Mhe. Mwenyekiti, akaniuliza wewe binafsi unasemaje mimi nikasema binafsi nitasema kura ya ndio kwani kuna tatizo gani, nikaona pana kutegeyana tegeyana ndio maana Mhe. Hamza Hassan Juma alipokuja hapa akasema hili suala linataka katika moyo wetu litoke katika moyo, kuandika, kusema, kuzungumza, kuhubiri itasaidia. Kama likitoka katika moyo ndio hilo tunalolitaka sasa mimi naona sikuona uzito mkubwa kwamba kitabu changu hakikuandika hivyo kuwapongeza Rais Karume, lakini *introduction* ya kitabu changu inampongeza Rais wangu tena inampongeza sana kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kuleta amani na utulivu nchini kwetu si inatosha hiyo.

Lakini jambo jengine alilolizungumza akasema hivi kumpa nafasi Moh'd Raza kuzungumza katika Radio yetu ya Taifa na huku wamekata kipindi cha Baraza la Wawakilishi akasema kwa ukali sana kwamba anataka maelezo ya kina mpaka aridhike, vyenginevyo huenda akazuia kifungu, namuomba sana hana haja ya kuzuia kifungu kwa maelezo nitakayoyatoa na kama anasikia na kama hakusikia ataambiwa. Hapa tunafungua kipindi cha maswali na majibu *live*

kuanzia saa 3.00 mpaka saa 4.30 kwa kawaida na masuala haya ya kuchukua fomu tumeweka kwenye Redio FM.

Juzi kwa bahati mbaya kipindi cha Maswali na majibu kilikwisha mapema sana kama kilivyokwisha jana na leo, kilichotokea baada ya maswali na majibu kumalizika kipindi cha redio MW kikafungwa mwenye kutoa vipindi hivi vya kupokea na kurudisha fomu akaondoka hapa akenda Afisi kuu ya CCM kwenda kusubiri watakaokuja ili awarikodi ndivyo kilivyofanyika. Hakuna kipindi cha Televisheni au Redio kilichokatwa na tusingeweza kufanya hivyo hata siku moja, kosa tulilolifanya hapa Mhe. Hamza Hassan Juma amelijibu tunamzungumza Moh'd Raza hatuzungumzi mantiki ya Moh'd Raza kwenda kuchukua fomu.

Moh'd Raza kwenda kuchukua fomu ni sahihi kama alivyokwenda kuchukua fomu Mhe. Waziri Kiongozi, Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na wengine wote watu kumi na moja walioshiriki, sasa hapa tunazungumza kitendo hatuzungumzi nani kenda kuchukua fomu kimantiki cha redio na Televisheni, kwa hivyo tulichokifanya ni sahihi na halali kumfanyia Moh'd Raza kama nilivyofanyiwa mimi Ali Juma Shamhuna na wengine wote. Nasisitiza hakuna kipindi cha redio cha maswali na majibu kilichokatwa hapa kwa kuzima redio yetu kwenda kumpelekea Moh'd Raza hatukwenda kumpelekea Moh'd Raza lakini tumekwenda kumpelekea mgombea wa Urais wa Zanzibar.

Nadhani aliyotaka niyajibu ni hayo nakwenda kwa Mhe. Ali Abdalla Ali yeye ametupongeza, ametushauri, amepongeza ZFA kwa kuleta kocha wa Kiingereza akatuuliza kama serikali inajua suala hili jibu lake tunajua tulikutana na wao ZFA tukazungumza tukaangalia mkataba wao na hii ni kampuni moja kubwa iliyojitolea kuidhamini ZFA kimchezo wa mpira, sio kocha tu lakini watawapa jezi, vifaa vya michezo na kadhalika. kwa hivyo serikali inajua na imetoa baraka zake.

Mhe. Spika, Uwanja wa watoto mwaka juzi tulisema, mwaka jana tukasema tena na mwaka huu ndio bahati nzuri tunamalizia suala hili nadhani halitokuja tena, uwanja wa Kariakoo na Tibirinzi umebinafsishwa sasa kama tunazungumza ubinafsishaji maana yake ndio maendeleo basi maendeleo ndio haya na tumevibinafsisha viwanja hivi kutokana na ushauri wenu wenyewe mliokuwa mnatupa, kwamba kama hamuviwezi kuhudumia vibinafsisheni tumefanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, bustani ya Jamhuri Garden hii haiko katika dhamana yetu Wizara ya Habari Utamaduni na Michezo haihusiani na kuimarisha bustani na kwa hivyo busatani hii watafutwe wenyewe waliyonayo ili tuwashauri. Lakini kutokana na michango iliyotolewa hapa nadhani wamesikia na ile kauli ya

kutumia kiwanja cha Michenzani badala ya ule basi sisi tuliokuwa hapa tumepokea na tutawaplekea wahusika na pia hiyo kauli yenu kuwa kiwanja kinakufa tutawapelekea ili hili suala liwe limefika kwa wahusika.

Mhe. Mwenyekiti, masuala mengine tumeshajibu, masuala ya rangi yameshajibiwa, kiwanda cha kuchapia magazeti cha Mchina nasema suala hili lilikuwa Mahakamani limeshamalizika aliyechukua fedha ameshafungwa na karibu atafunguliwa na hiki kiwanda kwa sasa hivi ni tabu sana tena kufufuliwa.

Mhe. Ali Denge Makame namshukuru sana kwa mchango wake na nakubali yote aliyoyasema na kutupongeza.

Mhe. Raya Suleiman Hamad kwanza nadhani pongezi zetu umezipata kutoka kwa Naibu Waziri za mtoto wetu tumeomba ukampelekee salamu zetu na lile suala la huyu jamaa aliyesema tumuajiri haraka ameshaajiriwa, nadhani hapa tumeshajibu masuala ya Mhe. Raya.
Mhe. Omar Ali Jadi amezungumza viwanja vya michezo nimeshajibu Tibirinzi na Kariakoo sasa ni binafsi haziko tena katika Wizara yangu. Idara ya upigaji chapa tumeshajibu.

Nataka nikumbushe tena kwamba wizara yangu imepata *Reduction ya twenty percentage* ya bajeti ya mwaka jana, kwa hivyo mwaka huu bajeti yetu iko chini kwa *Twenty five per centage* tumevumilia kwa kujua kwamba serikali yetu ina majukumu makubwa sana hapo mbele tena siku za karibu zijazo. Sisi sote tuliomo humu tungependa wakati tunaagana na cheki zetu tunaondoka nazo, serikali yetu kwa fedha au uwezo iliyokuwa nao tusingeweza kufanya makubwa. Lakini tukiangalia *program* zetu za wizara hii zile kubwa tulizozikusudia a*lmost ninety five percentage* zimeshakamilika kwa hivyo sisi hatukuona kasoro kubwa bajeti yetu kupunguziwa kwa *twenty five percentage* ili tuweze kudunduliza pesa za kulipa mafao wakati wa kustaafu sisi waheshimiwa.

Suala la michezo tumeshajibu michezo haifi inakua, mchezo wa ng'ombe nakubaliana na mawazo yako tutajitahidi kuufufua.

Mhe. Asha Moh'd Hilali aliuliza tunaondoka Amani tunahamia wapi kwa sherehe zetu za kitaifa nimeshaeleza ama Gombani tutaendelea, tukimaliza Dole au Bungi tutachagua pamojawapo tutafanya sasa pahala makusudi.

Ajira kwa watoto zinapindukia mpaka jukumu hili sijui kama ni letu au letu sote na wazazi au la Wizara inayohusika lakini tumelipokea na tutalifanyia kazi inayohusika.

Idara ya Upigaji chapa nimeshajibu, sanaa zikuzwe na zihamishiwe maskulini ushauri sio mbaya, lugha imechanganyika changanyika ni kweli basi tujitahidi sio Wizara peke yake lakini ni sisi sote maana na sisi tumo tunaozungumza English Kiswahili tunachanganya changanya.

Mhe. Mustafa Moh'd Ibrahim napokea pongezi pamoja na dua, pongezi kwa Amani Stadium napokea, michezo ni hasara tena nakubaliana na wewe sana kwamba michezo ni hasara ukitaka kucheza lazima ujifunge kibwebwe kama hujajifunga kibwebwe huchezi, kwa hivyo kweli michezo ni hasara. Lakini hasara hii kidogo nitatofautiana na wewe ya kupunguza mapato ya serikali ili tucheze, kwa mfano kupunguza kodi na mambo mengine, mara nyingi madai haya yanakuja na tunapoyatekeleza kwa mfano sijui nani anafaidika walengwa au wafanya biashara, tunapunguza kodi baadhi ya vifaa sukari, mchele, unga lakini wao wanapouza bei zao zinabakia pale pale au zinakwenda juu kizingizio *stock* hii ni ya zamani ya kodi ile iliyopita.

Lakini hata ikiingia *stock* mpya tunabakia pale pale sasa jamani hili suala la kupunguza punguza kodi hili linahitaji zaidi mchakato zaidi wa kuliamua vizuri zaidi, lakini kimantiki nakubaliana na wewe kama tukipunguza kodi za bidhaa hizi basi zitauzwa kwa bei ya chini ili wachezaji na viongozi wamiliki na kuweza kuendeleza michezo yao.

Mhe. Mwenyekiti, imeelezwa habari ya sanaa inatoa vibali vya muda mrefu madisko yanapigwa, ngoma zinachezwa watoto hawasomi nani tumpe jukumu hili, maana hawa sanaa wao wanatafuta pesa wanatoa vibali kwa kutafuta pesa, sasa walezi tufanye nini tuwalaumu watu wa sanaa wanaotoa vibali au tuwalee watoto wetu kuwapa muda wa kucheza na kuwapa muda wa kusoma nalo hili halina jibu la mkato, tukae pamoja na tulizingatie ingawa ulisema tusikujibu na unaunga mkono kwa asilimia mia moja lakini kwa faida ya tuliokuwepo hapa na wasikilizaji niliona nisema hayo.

Mhe. Hamad Masoud Hamad hapa hayupo lakini mpelekeeni salamu zangu tumependa kweli kweli mchango wake ni *first class* ya yote aliyoyasema na aliyotushauri tutayazingatia na pale itakapowezekana tutayatekeleza. Suala la *hall wood*, suala la Nigeria pengine na sisi tunaweza baadae tukaanzisha filamu yetu hapa Zanzibar na *hall wood* ikahamia Zanzibar sio kwa namna ile ilivyo *hall wood* sisi vipaji tunavyo labda tuvikuze zaidi na hilo tutalitengenezea utaratibu.
Mhe. Mzee Ali Ussi ushauri wako tumeupokea. Mhe. Haji Mkema haji ushauri wako tumeupokea, Mhe. Salum Hamad kwa kiasi fulani nimeshajibu zile hoja zako na mashauri yako yote uliyotoa tumeyapokea, umetushauri kuhusu kukuza

riadha lengo la kujenga ule uwanja wa amani tukaweka ile tatan lengo lake ni kukuza riadha.

Kwa niaba yenu nataka niwashukuru viongozi wa riadha hata tulipokuwa tatan yetu mbovu wanafanya mazoezi hapo hapo na wanapokwenda bara wanashinda vizuri sana, wanachukua medali za dhahabu, fedha, shaba wanatokea wa kwanza wameanguka wa pili kwa hivyo bado riadha haijaanguka na sasa tumetoa agizo makusudi hata rais alipokuwa anaupokea ule uwanja alituagiza sisi tuwape nafasi za kutosha wanariadha wautumie vizuri uwanja ule, tumeshaagiza viongozi wa riadha wafanye hivyo.

Mhe. Hamza Hassan Juma nakushukuru sana kwa mchango wako umetusaidia kujibu hoja mbili tatu ambazo waheshimiwa walikuwa wamezitoa, ile hoja ya kwamba kitabu hiki hakimuandika kumsifu Rais wetu kwa kufikia katika masuala ya muafaka nadhani nimejibu vizuri, hotuba ya Waziri kivuli imempongeza na kumsifu Balozi wa Norway haikusema chochote kuhusu Rais wa Zanzibar kwa jitihada yake ya kutafuta misaada kutoka kwenye serikali yake SMZ dola milioni kumi, SMT dola milioni tano ili mchango wa Zanzibar ukamilike kusibakie kuna vikwazo maana hivyo vilikuwa ni vikwazo, sasa na sisi pia tunasema tumsifu Mnorway sawa tena tumshukuruni sana, lakini tumsifu Rais wetu kwa juhudi zake za kutuletea maendeleo na mimi nasema sasa Pemba imekomboka tuutumie sasa umeme kwa kujiletea maendeleo.

Kama nilivyosema kuna wachangiaji wawili nao ni Mhe. Zahra Ali Hamad na Mhe. Suleiman Hemed michango yao wote ilikuwa zaidi katika kutushauri na kutuelekeza na sema tumepokea maelekezo na ushauri wao, na sasa kwa heshima na taadhima naomba kutoa hoja.

Mhe. Mwenyekiti. Hoja imetolewa waheshimiwa wajumbe sasa niwahoji wale wanaoafikia hoja hii wanyanyue mikono na wasioafiki wanyanyue mikono, walioafiki wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hoja ya bajeti ya waziri wa Habari Utamaduni na Michezo, sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama kamati ya Matumizi ili kupitisha vifungu vya matumizi ya Wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 42 WIZARA YA HABARI UTAMADUNI NA MICHEZO

Kifungu 05	- Sauti ya Tanzania Zanzibar	73,000,000
Kifungu 06	- Idara ya Televisheni Zanzibar	73,000,000
Kifungu 08	- Idara ya Upigaji Chapa	133,604,000
	JUMLA YA FUNGU	**282,604,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 42 WIZARA YA HABARI UTAMADUNI NA MICHEZO

Kifungu 03	- Afisi Kuu Pemba	417,436,000
Kifungu 04	- Mipango na Sera	664,225,000

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru kwa busara na mwanamke kumbe anaweza, katikasiku ambayo nimefurahi kwa leo kwa Mhe. Waziri wa Habari

Ashura13
imesahihishwa
Mhe. Salim Abdalla Hamad: (Anaendelea) katika kifungu nam. 6 kilichopo ukurasa wa 36 kinahusiana na malengo yatakayotekelezwa na 2010/2011. kifungu kinasema kuwa ni kuendeleza maombi ya ujenzi wa viwanja vya michezo vya ndani katika uwanja wa Amani kwa msaada wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China.

Mimi nilitaka kujua kiwanja kama kile cha Gombani ambacho kimeshaanza matengenezo na nilisema kuwa kiwanja hichi katika kujengwa kwake kilikuwa na ramani ambayo haikumalizika. Je, Wizara ina mpango gani wa kukihuisha kiwanda kile kwa mambo chungumzima ikiwa ni pamoja na hoteli ambayo ilikusudiwa kujengwa na viwanja vyengine vya michezo. Hili sikupata jibu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, naomba radhi kweli nili *skip* kutoa jibu hilo lakini ni kwamba hivi sasa namuomba Mheshimiwa akitoka hapa wakati anarudi Pemba apite achungulie pale Gombani atazikuta *activities* za nje na ndani za kufanya marakebisho kwa ndani ya kuweka nyasi bandia.

Nilisahau kutoa jibu wakati ule hizi nyasi bandia hazikuliwa na ng'ombe ziko safi mpaka leo. Hili lilikuwa ni *hear say* na si vizuri mtu kuchukua *hear say*

akaileta hapa na wala Makalibela hakula zile pesa zote zimekuwa *committed* na FIFA na FIFA wameleta wajumbe wawili kuanza hiyo kazi wajumbe wamefika siku tuliyokuwa tunazindua umeme wa Pemba. Nimewaona wamekuja tukaamkiana. Juzi niko Pemba nimekwenda kuangalia kiwanja kimeshavurugika kazi ilisita kwa sababu ya mvua. Lakini nimeuliza nimeambiwa kazi inaendelea kwa nguvu zake zoe na majani yameshakuwa *transported* yapo njiani. Walituletea orodha ya majani na vifaa vilivyokuja tukawarejeshea tukawambia watuletee *billl of lading* ili tuanze kuomba *exemption* ya ushuru kabla hata vifaa havijafika. Kwa hivyo hakuna kilichopotea, hakuna kilicholiwa, hakuna kilichoibiwa na kwa hivyo uwanja wa Gombani nyuma nje sasa hivi umo katika harakati na tuache. Mchina atusaidie kwa *indo games* ya Unguja na baadaye tutamuomba twende Pemba kama tulivyofanya polepole.

Mhe. Salim Abdalla Hamadi: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru Mhe. Mwenyekiti, kajitahidi sana kujibu mambo ambayo tulikwisha kuzungumza na yamo katika kitabu chetu. Hayo mambo ya nyasi, mambo ya umeme, sasa hivi tunangojea waje wafunge. Mimi nilichosema kile kiwanja hapo kilipojengwa mwanzo hakikumalizika plani yake, kuna mambo yaliachwa kwa sababu tulikitumia kabla ya kukabidhiwa, ikiwa ni pamoja na kujengwa hoteli na viwanja nyengine vya michezo. Kwa sababu hiki kiwanja Mheshimiwa tujue mpaka kikitiwa nyasi za bandia ina maana kitumike ukweli kimataifa.

Kimataifa Pemba hakuna chochote wala hakuna lolote zaidi ya ule uwanja yale mambo ambayo kuwa yalikuwa yajengwe kwa manufaa ya uwanja ule na sisi wenyewe vipi Mheshimiwa kayaweka katika utaratibu gani sio mambo ya nyasi kama alivyonieleza.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Nasema nyasi bandi zimo ndani ya uwanja, matengenezo yanayofanywa nje ya uwanja ndiyo hayo yaliyokubaliwa na wenzengu waliopita, mimi nayatekeleza naendelea nayo. Hoteli itajengwa na indo stadium zitajengwa huko ambapo kulikubaliwa na hiyo kazi imeshaanza, udongo wote unaotoka ndani sasa unatiwa kule.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kweli Mhe. Waziri kaelekea kupata urais. Ahsante sana. (*Vicheko*)

Kifungu 09 Idara ya Michezo	367,023,000
Kifungu 10 Idara ya Utamaduni	392,415,000
Jumla ya Fungu	**3,934,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko *yoyote)*

FUNGU 42 – WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO

Kifungu 04 Mipango na Sera	30,000,000
Kifungu 08 Idara ya Pigaji Chala	220,000,000
Kifungu 09 Idara ya Michezo	120,000,000
Kifungu 10 Idara ya Utamaduni	130,000,000
Jumla ya Fungu	**500,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Naibu Waziri Kiongoz na Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi ijadili na kupitisha makafirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko sasa naomba kutoa haja kwamba Baraza liyakubali makisio hayo. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii: Naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nikushukuruni tena kwa mashirikiano yetu mazuri ambayo yamatufikisha kukamilisha uwasilishwaji pamoja na kukubalika kwa Hotuba hii ya Mhe. Naibu Waziri Kiongozi na Waziri wa Habari Utamaduni na Michezo. Na kwa taratibuu za leo tumeshafikia mwisho kwa hiyo baada ya kurekebisha Kanuni ya Baraza, nachukua nafasi kuahirisha Kikao cha Baraza hili mpaka hapo Kesho siku ya Ijumaa tarehe 2/7/2010, saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 1:00 Usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 02/07/2010 Saa 3:00 Asubuhi)